Mfululizo wa Vitabu vya Maarifa ya Kisiasa

S. Gililov

Mkabala wa Lenin Kuhusu Suala la Mataifa

Progress Publishers

Mfululizo wa Vitabu vya Maarifa ya Kisiasa

S. Gililov

Mkabala wa Lenin Kuhusu Suala la Mataifa

Progress Publishers

Moscow

Shirika la Huduma za Maktaba Tanzania

Imetafsiriwa na Husein Abdul-Razak

Библиотека политических знаний

С. Гилилов

ЛЕНИНСКАЯ ПРОГРАММА РЕШЕНИЯ НАЦИОНАЛЬНОГО ВОПРОСА

на языке суахили

ПОГАШЕНО
2027 1999.
ВСЕСОЮЗНАЯ ГОСУДАРСТВЕННАЯ
БИБЛИОТЕКА
ИНОСТРАННОЙ ЛИТЕРАТУРЫ

© Progress Publishers, 1985

Г 0302030600-354
014(01)-85 287-85

YALIYOMO

Utangulizi 5

Sura ya Kwanza. MPANGO WA CHAMA KUHUSU SUALA LA MATAIFA KAMA ULIVYOFAFANULIWA NA KUFAHAMISHWA NA MABOLSHEVIKI CHINI YA UONGOZI WA LENIN 22

Misingi ya Kinadharia ya Mpango wa Chama cha Kikomunisti Kuhusu Suala la Mataifa . . 22

Madai Makuu ya Mpango wa Mabolsheviki wa Uhusiano Baina ya Mataifa 35

Mwongozo wa Ushikamano wa Kimataifa wa Matengenezo ya Chama 36

Dai la Haki ya Mataifa Kujiamulia Mambo Yao Wenyewe 39

Ukosoaji wa Mpango wa Kigeugeu wa Kujitawala Wenyewe Kitaifa na Kiutamaduni . . . 45

Mapambano ya Kupinga Aina Zote za Mtindo wa Kibwanyenye wa Kujibagua Kitaifa . . . 48

Uelimishaji wa Wananchi Wafanyao Kazi Kwa Ari ya Umoja wa Kimataifa 55

Sura ya Pili. MAONGOZI YA LENIN KUHUSU MAMLAKA YA KISERIKALI YA KITAIFA NA UTEKELEZWAJI WAO MNAMO KIPINDI CHA KWANZA CHA UTAWALA WA KISOVIETI 60
Dai la Mpango wa Chama Lililotungwa Katika Sheria 60
Mkabala Halisi wa Kihistoria 70
Misingi ya Mgawanyo Mpya wa Maeneo ya Utawala 81
Utaratibu wa Kujiendesha Wenyewe kwa Mambo ya Ndani Juu ya Msingi wa Utawala wa Wafanyakazi na Wakulima 85

Sura ya Tatu. AWAMU KUU KATIKA UUNDIKAJI WA DOLA LA KISOVIETI LILILOTANGAMANA LA MATAIFA MENGI . . . 111
Muungano wa Kijeshi-Kisiasa wa Mataifa . . 112
Uhusiano wa Ki-mkataba 129
Muungano wa Kidiplomasia 141
Uundwaji wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti 145

Sura ya Nne. USOSHALISTI PEKEE NDIO UWEZAO KUTANZUA TATIZO LA UHUSIANO WA MATAIFA 156
Msingi Unaotokana na Hali Halisi wa Ustawi na Ukaribianaji wa Mataifa Yote 156
Usawa wa Kimatendo wa Mataifa 162

Sura ya Tano. WANANCHI WA KISOVIETI–MJUMUIKO MPYA WA KIJAMII NA WA KIMATAIFA WA WATU 178
Umoja wa Wafanyakazi wa Kimataifa Ndio Msingi na Mtokezo wa Ushindi wa Sera ya Lenin Juu ya Uhusiano wa Mataifa . . . 190

TAMATI 205

UTANGULIZI

Suala la mataifa ni mojawapo la yale yaliyotatanika mno katika maisha ya siku hizi na historia ya jamii ya binadamu.

Mnamo muda wa karne kadhaa, mataifa na makabila mbalimbali yalikuwa yakipigana vita kwa ajili ya kukomesha ugomvi baina yao, na jitihada zo zote za kutafuta muundo wa kijamii wa busara zilikumbana na ukinzani mkali wa nguvu za uhafidhina, pia desturi zilizokomaa na fikira fupi za kipumbavu. Hata maendeleo chapuchapu ya uzalishaji mali, sayansi na utamaduni wakati wa mapinduzi ya shughuli za viwanda katika Ulaya hayakuleta mabadiliko yo yote ya maana katika tabia yenyewe ya uhusiano baina ya mataifa. Kinyume chake, kwa kadiri mabwanyenye walivyozidi kuendelea na utanuzi wa kikoloni, ndivyo vivyo hivyo pia upande wa ukandamizi wa kikabila na wa kitaifa ulivyozidi kuongezeka, pamoja na vita vya mara kwa mara zaidi baina

ya nchi. Ukuaji wa ubepari katika daraja yake ya ubeberu, ulipelekea kuugeuza ubeberu kuwa mfumo wa dunia, na ulimwengu ukagawanyika katika kundi dogo la nchi kandamizi za kibeberu na mataifa zilizoyatia utumwani, ambayo yalikuwa ndio wingi mkubwa sana wa walimwengu wote.

Kwa kuzingatia mwelekeo huo wa mambo ya uhusiano wa kimataifa, maoni ya kijamii ya dunia mnamo karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 yalimiliki zaidi upande wa fikira ya kutarajia shari kwamba uhasama baina ya makabila ulikuwa hauepukiki. Wachunguzi wa kibwanyenye walizielezea tofauti za kitaifa na za kikabila kama ndiyo sababu ya vita visivyokwisha, ambavyo hupelekea mamilioni ya watu kupoteza roho zao. Pia walizieleza kama ndio mzizi usiong'oleka wa uhasama baina ya mataifa mbalimbali.

Lakini, sababu hasa ya migogoro ya kimataifa ni hiyo tabia ya uhasama ya jamii ya kibepari ambayo hupelekea kuzuka migongano baina ya nchi, na pia baina ya watu wa makabila na mataifa mbalimbali ndani ya nchi moja, hasa kwa sababu ya maslahi ya kiuchumi ya kinyang'anyi ya matabaka yake ya kinyonyaji.

Ili kukomesha uhasama baina ya mataifa na unyonyaji wa baadhi ya madola na mataifa kwa mengine, ni lazima kufanya mapinduzi siyo tu katika akili za watu (ili kuwakomboa kutokana na desturi na fikira fupi zilizokwisha zake ambazo zilifanya iwe rahisi zaidi kuwanyonya), bali hasa katika muundo wenyewe wa mahusiano ya kijamii, yaani, mapinduzi yenye kuukomesha mfumo

wa kinyonyaji, miliki ya kibinafsi ya nyenzo kuu za uzalishaji mali.

Huo ndio uamuzi uliofikiliwa na Marx na Engels, waanzilishi wa usoshalisti wa kisayansi, mnamo katikati ya karne ya 19. Katika waraka wa mwanzo wa maongozi kwa Wakomunisti ulioandikwa nao, uitwao *Manifesto ya Chama cha Kikomunisti*, wao waliainisha kwamba uhasama baina ya matabaka ndani ya taifa unavyokuwa unatoweka, basi vivyo hivyo ndivyo pia uhasama wa taifa moja kwa jingine utakavyokoma. Uamuzi wao kwamba wananchi wafanyao kazi wa makabila na mataifa mbalimbali hawana wala hawawezi kuwa na sababu zo zote za kuchukiana na kuhasimiana ulionyesha mkabala mpya kabisa kimsingi kwa uhusiano baina ya mataifa.

Marx na Engels walionyesha njia na nyenzo za kupata amani ya kitaifa katika kila nchi na ushirikiano wa usawa wa kimataifa ulimwenguni kote. Ili kuweza kupata ukombozi wa kitaifa, tabaka la wafanyakazi, ambalo laongoza umma wa wananchi watumiao jasho lao, lazima likomeshe aina zote za ukandamizi wa kijamii. Walifahamisha kwamba ilivyokuwa mabwanyenye ni nguvu ya kimataifa, na kuwanyonya watu wafanyao kazi siyo katika nchi yao wenyewe tu, bali pia wakazi wa makoloni na nchi tegemezi, tabaka la wafanyakazi na watu wengine watumiao jasho lao katika nchi mbalimbali lazima waungane. Kwa hivyo basi, Marx na Engels waliihitimisha *Manifesto ya Chama cha Kikomunisti* kwa kutoa mwito huo: "Wafanyakazi wa Nchi Zote, Unganeni!". Tabaka la wafanyakazi na harakati za

kuania ukombozi zilivyozidi kukua na kupanuka, ndivyo umuhimu wa umoja wa wafanyakazi wa kimataifa ulivyozidi kuwa mkubwa kwa kutegemea kawaida za kimaumbile.

Isimu ya "suala la mataifa" ilizuka kihistoria kama suala la uhusiano baina ya mataifa makandamizi na yale yanayokandamizwa, kama suala la kukomesha mkandamizo wa kitaifa, kudhaminia usawa baina ya mataifa, makundi ya kikabila na ya kitaifa, na kusababisha hali za kustawisha maendeleo yao huru.

Mafunzo ya Marx na Lenin yanayakadiria mataifa kama ni zao lisiloepukika na umbo lisiloepukika la kuwako kwa jamii katika dahari ya maendeleo ya kibwanyenye. Mataifa yaliumbika kwa uchomozaji wa jamii ya kibepari na uundwaji wa soko la ndani la kitaifa. Kwa hivyo basi, mataifa yalichomoza kama mijumuiko ya kibwanyenye, ikiwaunganisha ndani ya nchi moja wanyonyaji na wanyonywaji, ambao maslahi yao ni yenye kuhitilafiana kabisa. Mabwanyenye waliyawakilisha maslahi yao wenyewe ya kitabaka ati kama yale ya taifa zima, huku wakiimarisha utawala wao na kufanya juu chini ili kuhifadhi fikira fupi za kujifungia kitaifa miongoni mwa umma. Ilivyokuwa mabwanyenye walijitokeza nafsi zao kama ni wenye kuwakilisha taifa zima, siasa yao ya kikoloni ilipelekea kuzuka chuki miongoni mwa mataifa yanayokandamizwa kwa taifa zima lenye kukandamiza.

Tatizo la uhusiano baina ya mataifa ni gumu sana kulitanzua kwa sababu mijumuiko ya kitaifa ni madhubuti sana. Lenin alitilia mkazo uma-

dhubuti wao usio wa kawaida, akiainisha kwamba tabia zenye kuyapambanua mataifa hazina budi kubaki kwa muda mrefu sana, hata katika jamii mpya isiyo na matabaka. Wakati huo huo, Lenin aliainisha tabia ya kupita kihistoria ya taifa, akikataa katukatu majaribio yo yote ya kudumisha mipambanuo ya kitaifa. Mathalan, aliikataa hiyo "kawaida" ya kujiendeleza kwa mataifa iliyotungwa na Otto Bauer (mtungaji nadharia wa mrengo wa Kulia wa harakati za kisoshalisti za kidemokrasi), ambaye alitabiri mpambanuo usiokoma wa mataifa chini ya usoshalisti, pamoja na kuongezeka kwa tofauti za utamaduni wa mambo yao ya kirohoni na kutengana kwao zaidi na zaidi.

Lenin alionyesha njia na nyenzo za kuwakomboa watu wafanyao kazi kutokana na masalio ya mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa, kutokana na fikira fupi za kitaifa, na kufahamisha kwamba inayumkinika kuupambanisha mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa na siasa ya umoja wa kimataifa ya tabaka la wafanyakazi yenye kulingana na maslahi makuu ya umma wa watu watumiao jasho lao wa mataifa na makabila yote.

Jambo lenyewe lilikuwa ni vipi kuyageuza mataifa ya kibwanyenye, pamoja na uhasama unaoandamana nayo, kuwa mataifa ya kisoshalisti, ambayo hayawezi kuwa ya ubakuzi kwa maumbile yake, wala kuwa na uhitilafiano usiopatanishika baina ya maslahi ya matabaka ya mataifa hayo, kwa maneno mengine, kuwa mataifa yanayopambanulika kwa umoja wa maslahi

yao, yenye kuheshimu uhuru na usawa wa mataifa yote, na kuwa na hamu ya kufanya kazi pamoja na mataifa yote mengine ili kukomesha ukandamizi wa kijamii na wa kitaifa na kudhaminia amani ulimwenguni kote.

Ni chama cha kimapinduzi tu cha tabaka la wafanyakazi, kikiandaliwa kwa maarifa ya kawaida za maendeleo ya kijamii na kuongozwa na kanuni za usoshalisti wa kisayansi, ndicho kiwezacho kuliwasilisha na kulitanzua barabara suala la uhusiano wa mataifa. Katika hali ngumu zilizokuwako nchini Urusi chini ya utawala wa mfalme, chama kama hicho kilitokezea kuwa kile cha Mabolsheviki kilichoongozwa na Vladimir Ilyich Lenin, mtengenezaji hodari wa kisiasa na kiongozi wa umma, na bingwa mkuu wa nadharia ambaye aliyaendeleza mafunzo ya Marx na Engels.

Chini ya uongozi wa Chama cha Mabolsheviki* mataifa ya Urusi, na hasa tabaka la wafanyakazi la Urusi, yalikuwa ndiyo ya mwanzo kulikabili jukumu hilo kubwa la kukomesha ukandamizi wa kijamii na wa kitaifa nchini na kuweka uhusiano wa usawa kikweli baina ya mataifa. Katika jitihada za kutanzua matatizo hayo, ambazo zilihitaji bidii kubwa na mihanga mingi, wananchi wa Kisovieti walipata ushindi dhidi ya ulimwengu mkongwe, ulimwengu wa migogoro ya kitaifa na ya kijamii.

Utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa katika nchi hii au ile una tabia mahsusi zake wenyewe zenye kutokana na mazingira ya maen-

* Sasa kinaitwa Chama cha Kikomunisti.– *Mfasiri.*

deleo yake ya kihistoria, mpangiko wa kitaifa wa wakazi wake, muundo wake wa kijamii, na kiwango cha maendeleo yake ya kiuchumi na ya kiutamaduni.

Chama cha Kikomunisti cha Urusi kilibidi kufanya kazi katika hali ya kihistoria ya mtataniko. Kililikabili suala la uhusiano wa mataifa na kutafuta njia ya kuanzisha aina mpya ya uhusiano baina ya mataifa juu ya msingi wa nadharia ya kimapinduzi ya maongozi ya Marx, iliyofafanuliwa na kutumiwa kielekevu katika hali halisi za kihistoria za Urusi. Usahihi wa njia hii umepitia mitihani ya matendo halisi na kuthibitishwa na maisha yenyewe. Hiyo ndiyo maana kwa nini maarifa ya Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti katika upande huo yakawa ni yenye umuhimu wa kihistoria kwa dunia nzima.

Urusi ya kabla ya Mapinduzi ya Kisoshalisti ya Oktoba 1917 ilikuwa na muundo wa mtataniko wa mataifa mengi, na pia pengo kubwa katika viwango vya kiuchumi baina ya maeneo ya kati ya nchini na yale ya pembezoni mwake, pamoja na aina nyingi mbalimbali za mifumo ya kijamii, mambo ya utamaduni na hali za maisha ya kila siku. Baadhi ya mataifa yalikuwa yameshaingia katika kipindi cha maendeleo ya kibepari, ilhali mataifa na makundi mengine mengi yalikuwa yangali bado katika kipindi cha maendeleo ya umwinyi nusu au hata yale ya ujima wa kikabila, na kwa hakika hasa kukabiliwa na hatari ya kuangamia kabisa. Hiyo ndiyo maana kwa nini maarifa ya nchi hii ya Kisovieti katika kufanya

mageuzi ya kisoshalisti yanayohusiana na mataifa, makabila na makundi mbalimbali ya kitaifa, jitihada za kutokomeza hali ya kutokuwa sawa baina ya mataifa iliyodumu kwa makarne kadhaa, zikawa ni zenye kuvutia sana nadhari ya madola yaliyoendelea halikadhalika na nchi ambazo maendeleo yao yanakinzwa na ubeberu na ukoloni.

Kikiwaunganisha pamoja watu wafanyao kazi wa mataifa na makabila yapindukiayo 100, Chama cha Kikomunisti kilionyesha usahihi wa mawazo ya Marx na Lenin juu ya uhusiano wa kidugu baina ya watu wa mataifa na makabila mbalimbali wakitiwa moyo kwa malengo yao ya pamoja. Mataifa mbalimbali, yakiwa na desturi zao za kihistoria na tabia zao za kipekee za utamaduni za makarne kadhaa, mataifa yaliyokuwa hapo kabla yamefarakana kwa migawanyiko mikubwa sana ya kidini, yameunda muungano usiovunjika kamwe.

Katika 1914, yaani kabla ya kuzuka Vita Vikuu vya Kwanza, watu milioni 33.2 kati ya milioni 169.4 wakaao katika mamlaka ya mfalme wa Urusi, walikuwa wakiishi katika sehemu za pembezoni mwa nchi hiyo zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni. Kiasi watu 43 kati ya kila mia walikuwa ni Warusi, ilhali 57 waliosalia walikuwa ni watu wa mataifa mengine, ambao wanatumia zaidi ya lugha 150 za kienyeji. Wale wasiokuwa Warusi walinyimwa haki ya kuwa na mamlaka yao wenyewe ya kiserikali, na mara nyingi walinyimwa pia haki ya kukuza lugha na utamaduni wao. Utawala usiopakika wa mfalme ulifuata

sera ya kupepelea kiburi cha utaifa kwa madhumuni ya kuchochelea uhasama baina ya mataifa na kupanua zaidi pengo lililokuwako baina ya wananchi wafanyao kazi wa Urusi.

Uundaji na ustawishaji wa mamlaka ya kiserikali ya kitaifa kwa maumbo mbalimbali chini ya utawala wa Kisovieti, uchomozaji wa uhusiano wa ushikamano wa kimataifa kikweli baina ya mataifa makubwa na madogo pamoja na ukadiriaji barabara wa tabia za kipekee za kitaifa umekuwa na unaendelea kuwa na umuhimu mkuu kwa kutanzua kimatendo tatizo la uhusiano wa mataifa. Maarifa ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti yanaonyesha kwamba mataifa ya kisoshalisti yenye kujenga jamii mpya kwa ushirikiano wa kidugu si kama tu hufikilia ustawi usio na kifani, bali pia hujongeleana karibu zaidi na zaidi.

Jamii ya kisoshalisti iliyojengwa katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti yaonyesha kwa mara ya kwanza katika historia nini maana ya uhusiano wa usawa na wa kidugu kimatendo. Nchi ya Kisovieti ilikuwa ndiyo maabara kuu ya mwanzo ulimwenguni wa kujaribia nadharia ya Marx na Lenin kuhusu utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa.

Maongozi ya Lenin juu ya sera ya uhusiano wa mataifa yalitoa msingi wa kinadharia kwa kazi yote ya Chama cha Kikomunisti na Serikali ya Kisovieti ya kuunda na kuimarisha dola la kisoshalisti la mataifa mengi.

Kikiongozwa na mafunzo ya Lenin kuhusu mataifa, kadhalika kuhusu njia ya kuyageuza mataifa ya kibwanyenye kuwa yale ya kisoshalis-

ti, kuhusu maendeleo ya hayo ya pili kwa kulingana na misingi ya kimaumbile, na pia juu ya tabia ya uhusiano baina yao, Chama cha Kikomunisti kilidhaminia ukomeshwaji wa mkandamizo wa kitaifa na uanzishwaji wa dola lenye mataifa mengi juu ya msingi wa usawa na urafiki baina ya mataifa.

Baada ya kwisha kujumlisha maarifa ya mwanzoni ya ujenzi wa dola katika Urusi ya Kisovieti, Lenin alikanusha maoni yaliyokwisha zake katika hali mpya ati kwamba shirikisho halifai kama umbo la uhusiano baina ya mataifa katika kipindi cha ukiukaji kutoka ubepari kuingia katika usoshalisti na chini ya usoshalisti wenyewe. Kwa hivyo alichukua mkabala wa kielekevu kwa utanzuaji wa suala la mtataniko kabisa la ujenzi wa usoshalisti na kutoa mchango muhimu katika nadharia ya maongozi ya Marx.

Maongozi ya Lenin ya muundo wa mataifa chini ya utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi na kushiriki kwake moja kwa moja katika kuasisi Jamhuri za Muungano na zile zenye kujitawala kwa mambo yao ya ndani yalikuwa ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyopelekea kuundwa kwa muungano wa hiari wa mataifa ndani ya dola moja.

Mpango wa Lenin wa kuunda dola lenye mataifa mengi, ambalo lazingatia kuambatanisha maendeleo ya kila taifa moja na utekelezwaji wa majukumu ya pamoja kwa mataifa yote ya nchini, ulikiandaa Chama kwa silaha barabara katika mapambano dhidi ya mitokezo mbalimbali ya mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa na

kiburi cha utaifa wa dola kuu. Chama cha Kikomunisti kiliongozwa na mashauri ya Lenin ya kuweka hadhari kuhusu suala la mataifa, pamoja na kukadiria vilivyo tabia za kipekee zenye kulipembua kila taifa moja mbali.

Mawazo ya Lenin juu ya vipi kukomesha hali za kutokuwa sawa kimatendo hasa baina ya mataifa, kustawisha viwanda na utamaduni wa kisoshalisti katika kila eneo la kitaifa, na kuwafunza makada wa kitaifa kutoka miongoni mwa tabaka la wafanyakazi na wasomi yalikuwa ni yenye umuhimu mkuu kwa kuimarisha urafiki baina ya mataifa ya Kisovieti na kuliwezesha tabaka la wafanyakazi la Urusi kupata imani ya mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla na utawala wa mfalme wa Kirusi.

Lenin alitoa mchango mkuu katika uundwaji wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti. Alionyesha haja inayotokana na hali halisi ya kuamua misingi yake mikuu na kufafanua misingi hii kwa mujibu wa mazingira maalumu ya kihistoria ya nchi hiyo na majukumu ya ujenzi wa usoshalisti.

Kikiongozwa na mawazo ya Lenin, Chama cha Kikomunisti kilifanya jitihada kuu kuimarisha urafiki baina ya mataifa, kuyang'oa mabaki ya mtindo wa kujibagua kitaifa, na kuwaadilisha wananchi wafanyao kazi kwa ari ya ushikamano wa kimataifa. Sera iliyotegemezwa juu ya maongozi ya Lenin kuhusu suala la mataifa yenye kuendeshwa na Serikali ya Kisovieti chini ya uongozi wa Chama cha Kikomunisti iliushajiisha umma kutoa juhudi nyingi za usanii zisizokuwa

na mfanowe katika historia, ikilifungulia kila taifa na kabila la Nchi ya Kisovieti fursa zilizo na kikomo kwa maendeleo ya uchumi na utamaduni.

Mojawapo la matokeo makuu ya sera ya Lenin kuhusu mataifa ni kwamba mataifa ya Mashariki ya Kisovieti yameongozea katika usoshalisti ulioendelea moja kwa moja kutoka katika mfumo wa kimwinyi, kadhalika yamejipatia mamlaka yao ya kiserikali ya kitaifa ikilinganishwa na hali yao ya zamani ya ukosefu wa haki, na pia yamefikilia kiwango cha juu cha uchumi na utamaduni ikilinganishwa na hali yao ya zamani ya kuzorota na kutojua kusoma na kuandika. Maarifa haya halisi ni yenye umuhimu mahsusi – kinadharia halikadhalika na kimatendo – kwa nchi zilizoanza hivi karibuni kushika njia ya maendeleo huru ya kitaifa.

Bila ya shaka, nchi changa zenye kuongozea katika usoshalisti hazikabiliwi moja kwa moja na jukumu la kuyageuza mataifa ya kibwanyenye kuwa ya kisoshalisti, kwani kwa jumla, mataifa ya kibwanyenye hajaumbika vilivyo bado huko. Jukumu lao sasa ni kuunda taifa lililotangamana wakati wa ukiukaji kwendea katika usoshalisti kwa kupitia daraja kadhaa za mfuatano, pasina kubidi kupitia daraja ya maumivu ya maendeleo ya kibepari.

Katika kadhia hii, mataifa ya kisoshalisti yanaundwa kwa mujibu wa kawaida za kimaumbile zilizo za kipekee kwa nchi hizo. Lakini matendo yenyewe hasa na kawaida za kimaumbile za kijumla za uundwaji na ustawishwaji wa jamii zote za kikabila, pamoja na mataifa ya kisoshalis-

ti yaliyotokana na mataifa ya kibwanyenye, ni muhimu sana katika kuamua njia za uundwaji wa mataifa ya aina ya ukiukaji na yale ya kisoshalisti katika nchi zinazoongozea katika usoshalisti kwa kuuepuka ubepari. Kati ya kawaida hizi za kimaumbile ni jukumu la uamuzi litwaliwalo na hali za kiuchumi katika uundwaji na ustawishwaji wa aina zote za kihistoria za mijumuiko mbalimbali ya umma; jukumu la uongozi la mambo ya kijamii kwa kulinganisha na yale ya kikabila; mfuatano wa maumbo ya kihistoria ya mijumuiko ya kikabila, na kadhalika.

Wakijumlisha maarifa ya Mashariki ya Kisovieti katika kutanzua tatizo la uhusiano wa mataifa, na pia maarifa ya mwanzoni ya maendeleo ya mataifa katika nchi zilizojipatia uhuru wao karibuni, wachunguzi wa Kisovieti wametoa mashauri kadhaa kuhusu njia na kawaida za kimaumbile zionekanazo katika mabadiliko ya kimaendeleo ya mataifa yaliyokuwa yamezorota kuja kuwa ya kisoshalisti wakati wa ukiukaji kwendea katika usoshalisti kwa kuepukana na daraja ya ubepari.

Inatiliwa mkazo hasa kwamba kabla ya kuchomoza kwa nchi za kisoshalisti, mataifa yaliyozorota katika nchi tegemezi yasingeweza kuepukana na daraja ya ubepari. Uundwaji wa mfumo wa kisoshalisti wa kwanza ulimwenguni ulifungulia matazamio halisi kwa mataifa yaliyozorota kuweza kuendelea kuja kuwa ya kisoshalisti.

Katika nchi zisizoendelea, uundwaji wa mataifa ya kisoshalisti kwa kawaida hutanguliwa na kipindi cha kuimarika kitaifa-kidemokrasi, kijamii-

kisiasa na kiitikadi kwa taifa na kukua kuja kuwa taifa la aina ya ukiukaji. Taifa huungana chini ya beramu ya mapambano ya kuwania ukombozi wa kitaifa na ya kidemokrasi-kimapinduzi, na umoja wake wa kiitikadi na wa kisiasa hupatikana kwa msaada wa siasa na itikadi ya chama cha kimapinduzi.

Mamlaka ya kiserikali ya kitaifa ni jambo mojawapo kuu sana katika uimarikaji wa mataifa yaliyozorota ambayo yameepukana na daraja ya ubepari. Mataifa ya kisoshalisti yanaumbika katika nchi hizi kama mjumuiko wa kiuchumi juu ya msingi wa miliki ya kijamii na uchumi wa kitaifa ulioshikamana kama kitu kimoja kizima. Kama maarifa yaliyopatikana na mataifa ya Kaskazini na Mashariki za nchi hii ya Kisovieti yalivyoonyesha, uundwaji wa mwambatano uliotangamana wa dola zima unachanganyika pamoja na tabia za kipekee za kiuchumi za kila eneo moja la kitaifa, pia ukadiriwaji wa tabia mahsusi za muundo wa kiuchumi wa kila kundi la kitaifa na la kikabila uliokuwako kabla ya mapinduzi, kadhalika mazingira ya kimaumbile na mengineyo.

Kama historia inavyoonyesha, mataifa yaliyoepukana na daraja ya ubepari hayawezi kuendelea kuja kuwa mataifa ya kisoshalisti pasina kuunda na kulikuza tabaka la wafanyakazi la taifa, na kwamba maendeleo ya kijamii-kikabila huwa chapuchapu zaidi katika nchi zile ambako vikosi vya kitaifa vya wafanyakazi wa viwandani vinaundwa katika daraja za mwanzoni.

Umoja mkubwa zaidi, usaidiano, na upeanaji wa misaada ya hali na mali baina ya mataifa, ba-

ina ya makundi mbalimbali ya kitaifa katika nchi yenye mataifa mengi ni jambo muhimu sana linalopelekea mataifa yasiyoendelea kustawi kuja kuwa matabaka ya kisoshalisti. Ushikamano wa kimataifa unatokezea kuwa ndio msingi wa mapambano dhidi ya kiburi cha utaifa, upingaji maendeleo na mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa.

Uhuru kamili wa kutumia lugha ya kienyeji kwa kila taifa, uondoshwaji wa mapendeleo kwa lugha fulani mahsusi na, wakati huo huo, upatikanaji wa umoja madhubuti wa lugha ni sharti muhimu kabisa kwa uundwaji wa mataifa ya kisoshalisti.

Utamaduni wa kitaifa wa pamoja ni mojawapo ya dalili kuu za kuumbika kwa taifa. Katika kuumbika kwake juu ya msingi wa kisoshalisti kunatukia badiliko kuu katika tabia na jukumu la kijamii la mitokezo ile ya mtataniko sana kama fahamu ya kujitambua kitaifa, hisia ya kitaifa, tabia ya kitaifa, mila na desturi za kitaifa, n. k.

Utamaduni wa kitaifa wa pamoja hupatikana katika hali ya mapambano makali ya kupinga masalio ya matabaka ya kinyonyaji, ya kupinga mabaki ya kimwinyi ya kikale na ya kidini akilini mwa wananchi, pia katika hulka na maisha yao ya kila siku, ya kupinga itikadi na matendo ya kujibagua kitaifa, kutojua kusoma na kuandika, na mirathi mingine mibaya ya siku za nyuma.

Kwa hivyo basi, ukuaji wa mataifa haya kuja kuwa ya kisoshalisti una tabia zilizo za kipekee kwayo na shida zisizopata kuhisiwa na watu waliojumuika kama mataifa hata kabla ya mapin-

duzi ya kisoshalisti. Kwanza kabisa, mataifa yanayoepukana na daraja ya ubepari katika maendeleo yao hayana budi kuchukua muda mrefu zaidi kuyageuza mahusiano ya kijamii-kiuchumi kimsingi kwa sababu ya uzorotaji wao mkubwa sana. Mathalan, katika sehemu za Mashariki za Nchi ya Kisovieti ardhi, mifugo na mali nyinginezo za matabaka ya kinyonyaji zilitaifishwa baadaye zaidi kuliko ilivyokuwa katika Urusi ya Kati. Kwa muda mrefu sana hata baada ya mapinduzi ya kisoshalisti, mataifa mengi ya sehemu za Mashariki za Nchi ya Kisovieti hayakuwa na mahali pao pa ukazi wa daima na yaliendelea kuhamahama na mifugo au kufanya maskani kwa sehemu tu ya maisha yao, jambo ambalo lilikinza kustawisha chapuchapu uzalishaji mali wa kijamii.

Mambo yote haya yenye tabia za kipekee nchini Urusi yatajadiliwa kwa urefu zaidi baadaye, kitabuni humu.

Vikizingatia maarifa yao wenyewe, pamoja na hali mahsusi za nchi zao wenyewe, ambako mataifa hayakupitia daraja ya ubepari katika maendeleo yao, kadhalika kwa kuzingatia maarifa ya nchi za kisoshalisti na maongozi ya usoshalisti wa kisayansi, vyama vya kimapinduzi vya kidemokrasi vinavyotawala katika nchi zilizoshika njia ya maendeleo ya kitaifa ya kujitegemea wenyewe vimekadimisha fikira hiyo ya taifa moja, watu wamoja kama mchanganyiko wa makundi yote ya kikabila, na utamaduni wa kitaifa wa aina moja wenye kuendelezwa kwa athari ya utamaduni wa dunia, pamoja na desturi za utamaduni za ki-

maendeleo za taifa lililokuwa likitawala hapo kabla, na vimeanza kutanzua tatizo la uundaji wa taifa kama hilo ambalo hatimaye lingekuja kugeuzwa kuwa la kisoshalisti. Utumiaji kwa welekevu wa maarifa ya Nchi ya Kisovieti waweza kuwa na msaada mkuu katika utanzuaji wa matatizo haya. Nadharia ya Lenin kuhusu suala la mataifa, mkabala uliotegemezwa juu ya maongozi ya Lenin kwa mitokezo ya mtataniko na yenye kuhitilafiana katika maisha ya mataifa mbalimbali, ni silaha madhubuti kwa vyama hivi ambayo inaviwezesha kuichunguza mienendo ya kitaifa kwa utaratibu wa kisayansi na kuvisaidia kudhihirisha maudhui yao na kuamua mwelekeo wa maendeleo yao.

MPANGO WA CHAMA KUHUSU SUALA LA MATAIFA KAMA ULIVYOFAFANULIWA NA KUFAHAMISHWA NA MABOLSHEVIKI CHINI YA UONGOZI WA LENIN

Misingi ya Kinadharia ya Mpango wa Chama cha Kikomunisti Kuhusu Suala la Mataifa

Wanaitikadi wa kibwanyenye wanaipotoa maana yenyewe hasa ya suala la mataifa, yakijaribu kuthibitisha kwamba ni vyanzo vya kitaifa, wala siyo vya kitabaka, ndivyo vilivyo muhimu katika maisha ya kila taifa, kwamba hulka ya kitaifa na fahamu ya kujitambua kitaifa ndizo ati zilizo na milele, za kiasili na zisizobadilika, ambazo ni zenye kuamua tabia ya binadamu. Ni ukabila, wanadai, ndio unaoamua uhusiano baina ya watu wa mataifa mbalimbali. Na hiyo ndiyo sababu ya watu wafanyao kazi kubandikizwa uamuzi huo kwamba mapambano ya kitabaka hayawezi kamwe kuigeuza hali ya mataifa, kwamba migawanyiko ya kitaifa baina ya watu itaselelea milele, na kwamba suala la uhusiano wa mataifa haliwezi kutanzuliwa kamwe. Propaganda kama hiyo imekusudiwa kuficha isijulikane na watu wafanyao kazi kwamba ukandamizi wa kitaifa umetia mizizi katika jamii ya kibepari,

katika uhusiano wa miliki ya kibinafsi ya nyenzo za uzalishaji mali.

Mafunzo ya Marx na Lenin yanategemeza hoja zake juu ya ufafanuzi wa kisayansi wa maana ya neno hilo "taifa" kama isimu ya kijamii-kihistoria yenye kulingana na daraja maalumu ya maendeleo ya jamii ya binadamu, na kuona kwamba mataifa huchomoza katika dahari ya ubepari unaoendelea. Nadharia kuhusu taifa iliyotegemezwa juu ya mafunzo ya Marx na Lenin yaikanusha dhana ya kibwanyenye isiyokuwa ya kisayansi ambayo inayafananisha mataifa na makabila na pia na watu wa rangi mbalimbali. Makabila ni isimu ya kiethnografia. Yalichomoza katika jamii iliyokuwa haijagawanyika katika matabaka bado, ambapo yalikuwa ni makundi yaliyojifungia yenye kujitegemea yenyewe pamoja na utaratibu wa aina moja wa mambo ya uchumi. Hiyo ilikuwa ni mijumuiko ya jamaa au, kwenye daraja ya juu zaidi ya mfumo wa ujima wa zama za mwanzoni, miungano ya makabila, yaani, makabila yenye muundo wa kijamii wa mtataniko zaidi.

Kwa maendeleo zaidi ya nguvu za uzalishaji mali na uchomozaji wa miliki ya kibinafsi, mfumo wa ujima wa zama za mwanzoni uliipisha njia jamii iliyogawanyika katika matabaka. Makabila yalichanganyika pamoja na kukachomoza mijumuiko mipya ya kijamii: makundi ya watu wenye nasaba moja, eneo moja la ukazi na lugha moja. Fungamano za kiuchumi na kiutamaduni zilikuwa zingali hafifu kwa kiasi baina yao, lakini wakati fungamano za lugha, eneo la ukazi na ma-

husiano ya kiuchumi yalivyokuwa yakiimarika zaidi, jadi zinazotokana na nasaba moja zikaanza taratibu kupoteza umuhimu wake, na miundo mipya ya kijamii ikachomoza, yaani mataifa.

Mfumo wa utumwa, ukiwa na nguvu za uzalishaji mali zisizoendelea, mfumo ulioyaunganisha pamoja kwa nguvu makabila na watu wengi wenye tabia mbalimbali pasina kuwa na fungamano za kiuchumi zilizoendelea, haukuweza kuwa ndio msingi wa kuchomoza kwa mataifa. Uchumi wa kimwinyi wa Zama za Kati, ukiwa umetawanyika na wenye madhumuni ya matumizi tu pekee, uliwakinza watu kujongeleana karibu zaidi, na miundo ya Zama za Kati – pasina kujali dai linalotokana na hali halisi la kutaka paweko mgawanyiko zaidi wa kazi, kadhalika mapambano yaliyoendeshwa na wakulima dhidi ya mamwinyi, na uchomozaji wa makazi ya vijijini, yanayoshughulikia kazi maalumu za kilimo, na jamii za wasanii za aina ya mijini ambazo hazikuwa chini ya utegemezi wa mamwinyi – ilikinza ukuzwaji wa mahusiano ya kisokoni, yaani ya ununuzi na uuzaji bidhaa.

Kwa ustawi wa uzalishaji bidhaa na mahusiano ya ubadilishanaji bidhaa kwa pesa yanayotokana na uimarikaji wa utawala wa mabwanyenye, mwamko wa fahamu ya kitaifa ukazinduliwa na mataifa yakaumbika.

Wakati wa kuimarika kwa jamii ya kibepari, mabwanyenye walitenda kazi ya kimaendeleo, wakiyavunja mahusiano ya kimwinyi, wakiwakomboa watu waliokandamizwa na kupigania kuundwa kwa mataifa ya kibwanyenye. Lakini

baada ya kwisha kuingia katika daraja ya ubeberu ya maendeleo yake, ubepari ukawa siyo tena wa kimaendeleo, lakini wa kupinga maendeleo zaidi na zaidi, ukiyatia utumwani na kuyanyonya kikatili madarzeni ya mataifa na kuendesha vita visivyokwisha vya kuwania ugawanyaji upya wa dunia. Katika hali hizi, suala la mataifa lilikuja kuwa ni lile la mataifa na makoloni.

Akilichambua suala la mataifa katika dahari ya ubeberu, Lenin alionyesha kwamba ubepari ulikuza nguvu za uzalishaji mali kwa kiasi kikubwa sana hata jamii ya binadamu ikakabiliwa na chaguo la ama kuingia katika usoshalisti au kuhilikika kwa miaka na hata makumi ya miaka ya mapambano ya kisilaha baina ya madola "makuu" kwa ajili ya kuuhifadhi ubepari kwa njia isiyo ya kimaumbile kwa msaada wa makoloni, makampuni ya kuhodhi, fursa za umbele na ukandamizi wa kitaifa wa kila aina.

Basi, ilikuwa ni maisha yenyewe, mwelekeo wa kihalihalisi wa maendeleo ndio ulioiwasilishia sehemu kubwa zaidi ya jamii ya binadamu – yaani mataifa yakandamizwayo – suala kuu na la hima kuhusu njia za kujipatia ukombozi na ustawi wa kitaifa wa kimaendeleo, kadhalika haja ya lazima ya kutanzua tatizo la uhusiano baina ya mataifa.

Marx na Lenin walifichua kiini cha tatizo la uhusiano baina ya mataifa na kuonyesha kwamba chini ya ubepari, chini ya utawala wa kibeberu, tatizo hili haliwezi kutanzuliwa. Ukandamizi wa kitaifa hauwezi kuondoshwa isipokuwa kwa uondoshwaji tu wa miliki ya kibinafsi ya nyenzo za uzalishaji mali, kwa ushindi wa usoshalisti.

Akiyatatanua mashauri hayo yaliyotolewa na Marx na Engels, Lenin alithibitisha kwamba kwa kutengeneza uzalishaji mali bila ya ukandamizi wo wote wa kitabaka, bila ya unyonyaji wa binadamu kwa binadamu mwenziwe, na kwa kuwajongeza karibu zaidi watu wafanyao kazi walio huru kutokana na unyonyaji kwa kutegemea maslahi ya pamoja, usoshalisti unaondosha ukandamizi wa kitaifa (na ukandamizi wa kisiasa kwa jumla), wadhaminia ushirikiano na fungamano kubwa zaidi baina ya mataifa.

Wakati huo huo, mafunzo ya Marx na Lenin yanatoa hoja kwamba mabadiliko makuu ya kijamii hayayumkiniki bila ya kuzingatia barabara suala la mataifa katika mahusiano baina ya watu. Ingawa harakati za kitaifa siyo shabaha ya hatimaye ya tabaka la wafanyakazi, hata hivyo zinatumika kwa uhalisi kama daraja ya katikati ya mapambano ya kuwania demokrasi, yenye kufanya iwezekane kwendea katika usoshalisti. Juhudi za kupigania usoshalisti si kitendo cha mara moja tu cha mapambano ya kitabaka dhidi ya mabwanyenye, dhidi ya ubeberu, bali ni mwenendo wenye daraja za katikati, na harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa ni daraja mojawapo muhimu kabisa kati ya hizo.

Mafunzo ya Marx, yakiwa kama ni mtokezo wa kisayansi wa maslahi muhimu kabisa ya tabaka la wafanyakazi, yamekuwa daima yakichukua msimamo usiopatanishika dhidi ya aina zote za ukandamizi wa kitabaka na wa kitaifa, dhidi ya kiburi cha utaifa, mtindo wa kukataa utaifa, na ukanyaji mtupu katika suala la mataifa. Lakini,

kutokana na haya isieleweke kwamba tabaka la wafanyakazi na chama chake cha kimapinduzi huunga mkono harakati zo zote zile za kitaifa. Tabaka la wafanyakazi haliwezi kuziunga mkono harakati zile za kitaifa ambazo zimekusudiwa kupinga maslahi ya mataifa yapendayo uhuru, na dhidi ya mapambano ya kimapinduzi ya kukomesha mkandamizo wa kijamii na wa kitaifa.

Marx na Lenin walisisitiza kwamba maudhui ya suala la mataifa siku zote yanahusika na hali halisi na, kama Lenin alivyofahamisha, haiwezi kuwa vyo vyote vingine isipokuwa kubainisha tu tabia halisi za kipekee za suala la mataifa na harakati za kitaifa zinazotokea katika nchi hii au ile mnamo dahari hii au ile.

Lenin alisema: "Chama cha Kikomunisti, kikiwa kama ni mwakilishi mwenye fahamu timamu wa mapambano ya tabaka la wafanyakazi ya kuwania kuupindua utawala wa mabwanyenye, yapasa kitegemeze siasa yake, katika suala la mataifa vile vile, siyo tu juu ya maongozi ya kimawazoni na ya kijuujuu tu, bali ... juu ya tathmini barabara ya hali mahsusi ya kihistoria na, kwanza kabisa, hali za kiuchumi ...".

Lenin alifahamisha kwamba tabaka la wafanyakazi lina hamu kuu ya kupata utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa na halitoweza kufuzu isipokuwa lishike njia ya mageuzi ya kimapinduzi ya jamii. Hiyo ndiyo maana kwa nini tabaka la wafanyakazi likaliweka suala la mataifa chini ya maslahi yake ya kitabaka: uondoshwaji wa mfumo wa kinyonyaji na ukiukaji kuingia katika usoshalisti. Kwa hivyo basi, ushikamano wa

kimataifa ni kitu cha mwanzo kabisa kupita vyote kwa tabaka la wafanyakazi, kwa sababu ni silaha madhubuti kabisa inayowezesha kukomesha mkandamizo wa kijamii halikadhalika na ule wa kitaifa. Katika kupambana na wageugeu ndani ya harakati za tabaka la wafanyakazi, Lenin aliyaendeleza mbele zaidi mawazo ya Marx na Engels kuhusu suala la mataifa na kutunga nadharia juu ya mapinduzi ya kuwania ukombozi wa mataifa na makoloni katika dahari ya ubeberu; alilifungamanisha suala la mataifa na lile la ukombozi kutokana na ukandamizi wa kibeberu, akiziona harakati za kuwania ukombozi za mataifa yakandamizwayo kama ni sehemu isiyotenganishika ya mapinduzi ya kisoshalisti ya dunia.

Wazo lililotegemezwa juu ya mafunzo ya Marx na Lenin kuhusu mielekeo miwili ya kihistoria katika suala la mataifa ni chanzo muhimu kabisa cha kinadharia kwa mpango wa Chama cha Kikomunisti katika upande wa uhusiano baina ya mataifa.

"Ubepari unaoendelea wajua mielekeo miwili ya kihistoria katika suala la mataifa", Lenin alifundisha. "Wa kwanza ni mzinduko wa maisha ya kitaifa na harakati za kitaifa, juhudi za kupinga aina zote za mkandamizo wa kitaifa, na uundwaji wa madola ya kitaifa. Wa pili ni ukuzaji na uzidishaji wa kila aina ya maingiliano ya kimataifa, uvunjaji wa mapingamizi yenye kuyatenganisha mataifa, uundaji wa umoja wa kimataifa wa rasilmali, wa mambo ya kiuchumi kwa jumla, wa siasa, sayansi, n. k.

"Mielekeo yote hiyo miwili inatokezea kuwa

ndiyo kawaida ya ubepari ulimwenguni kote. Wa kwanza unatamalaki mwanzoni mwa maendeleo yake, na wa pili wamithilisha tabia ya ubepari uliopevuka ambao unaelekea katika ugeukaji wake kuwa jamii ya kisoshalisti."

Mielekeo yote hiyo miwili ni ya kimaendeleo na imefungamana sana baina yao. Wa kwanza umelengewa dhidi ya mahusiano ya kimwinyi na mkandamizo wa kikoloni, unayashajiisha mapambano ya mataifa dhidi ya muungano wa kushurutishwa, na kuukadimisha umma wa watu wanaopambana na mkandamizo wa kitaifa kwenye uwanja wa kihistoria. Mwelekeo wa pili watokeza kiini cha mahusiano baina ya mataifa, waonyesha kawaida ya kimaumbile ya kiuchumi ya ukuaji wa nguvu za uzalishaji mali, wasaidia kuendeleza mgawanyo wa kazi wa kimataifa unaohitajika kwa mujibu wa hali zenyewe halisi, na kufanya iwe rahisi zaidi kwa watu wafanyao kazi wa nchi mbalimbali kuungana katika mapambano dhidi ya adui yao wa pamoja, yaani, ubeberu.

Chini ya ubepari kwa jumla na hasa ubeberu, mielekeo hii miwili katika suala la mataifa inakuwa haitimiliziki na kutokezea kama ni uhasama usiosuluhishika. Hii ni kwa sababu ukandamizwaji wa mataifa fulani, huku kukiwa na mapendeleo na fursa za umbele kwa mengine, ni kawaida ya kimaumbile kwa ubepari, na mabwanyenye wanajaribu kuitumia mielekeo yote hiyo miwili kwa madhumuni haya hasa. Hiyo ndiyo maana kwa nini chini ya ubepari mwelekeo wa maendeleo huru ya mataifa wajitokeza katika ha-

mu ya mataifa yanayokandamizwa kutaka kujitenga mbali na kuunda madola huru ya kitaifa. Ilivyokuwa ubeberu watumia nguvu kuyakinza yasifanye hivyo, basi nayo pia hujibiza kwa harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa, na suala la mataifa linakuwa kali mno.

Katika Ulaya ya Mashariki, Asia na maeneo mengine yenye kukabiliwa daima na hatari ya kuvamiwa na adui wa nje, madola yenye serikali moja kuu yaliundwa hata kabla ya ustawi wa ubepari na uchomozaji wa mataifa. Ilikuwa ni matabaka yanayotawala ya mataifa yenye nguvu zaidi ndiyo yaliyounda madola haya, yakiyaweka mataifa dhaifu zaidi chini ya amri yao na kwa hivyo kuyafanya yatete. Lakini katika kipindi cha ubepari ukweao, suala la mataifa kwa vikubwa sana lilifungika mnamo mipaka ya dola.

Ubepari ulivyoendelea kuja kuwa ubeberu, daraja yake ya juu zaidi, suala la mataifa liligeuka kuwa lile la baina ya madola. Ubeberu wautumia mwelekeo wa kimaendeleo utegemeao hali halisi wa kuifanya rasilmali kuwa ya kimataifa kwa maslahi yake wenyewe ya kichoyo, nayo ni kuyatia utumwani mataifa mengine, kwa hivyo kuuzuia usongaji mbele wa mwelekeo huu wa kimaendeleo na kuyapotoa maendeleo ya nguvu za uzalishaji mali katika nchi tegemezi. Mabwanyenye hawawezi kamwe kupata mkabala barabara kwa utanzuaji wa tatizo la uhusiano baina ya mataifa kwa sababu ya tofauti za uhasama zisizopatanishika baina ya mchanganyiko wa kiuchumi wa kimaendeleo wa mataifa na mbinu zipingazo maendeleo zinazotumiwa na ubeberu katika ku-

fanya mchanganyiko huo. Usoshalisti ndio mfumo pekee ambao waweza kuipatanisha mielekeo hiyo miwili, ukidhaminia mamlaka na usawa wa mataifa yaliyoanzisha uhusiano mwema baina yao, ubadilishanaji wa kila aina, na kushiriki katika mgawanyo wa kazi wa kimataifa.

Nadharia ya Lenin kuhusu ubeberu yasaidia kupata uelewaji mkubwa zaidi wa mielekeo mikuu ya matukio ya mambo ulimwenguni. Ubeberu, kama Lenin alivyouelezea, umegeuka kuwa mfumo wa dunia wa mkandamizo wa kikoloni na ukabwaji kifedha wa mataifa mengi zaidi duniani kwa upande wa kikundi kidogo cha nchi "zilizosonga mbele". Suala la mataifa limegeuka kuwa lile la baina ya madola kwanza kabisa kwa maana hiyo kwamba juhudi za madola ya kibeberu kutaka kuyaweka mataifa mengine chini ya amri yao na kujipatia masoko ya kikoloni ya kuuzia bidhaa zao, pia vyanzo vya malighafi na nguvukazi rahisi zimekuwa ndiyo mojawapo ya sababu kuu za kufumuka kwa vita vya dunia kwa ajili ya kugawana upya dunia iliyokwisha gawanywa. "Ubeberu wamaanisha ukandamizwaji unaozidi kuwa mkubwa wa mataifa ya dunia kwa upande wa Madola Makuu machache," Lenin aliandika. Uitifaki wo wote ule wa nchi za kibeberu, "jumuiya" yo yote ile "ya mataifa" waiundayo si cho chote si lo lote isipokuwa ni mapatano tu baina ya serikali za kibeberu kuzidisha ukandamizi kwa tabaka la wafanyakazi lao wenyewe na njama ya kuyakandamiza kwa pamoja mataifa yaliyoko chini ya utawala wa kikoloni.

Wakati huo huo, hilo jambo kwamba chini ya

ubeberu suala la mataifa linageuka kuja kuwa ni lile la baina ya madola halimaanishi kwamba limeshapoteza umuhimu wake wa ndani. Kinyume chake, nchi zote za kibepari zenye mataifa madogo madogo zingali bado zinakabiliwa na tatizo la uhusiano baina ya mataifa, lile la mapambano ya kuwania usawa kwa mataifa yote.

Pamoja na hayo, pasina kujali hilo jambo kwamba siasa ya kibeberu yazuia maendeleo ya kiuchumi ya makoloni na nchi tegemezi, mabwanyenye na wafanyakazi wao wenyewe huchomoza katika nchi hizi vile vile. Mabwanyenye hawa wa kitaifa, ambao huwa wanadhiliwa na makampuni ya kuhodhi ya kigeni na wana hamu ya kupata maendeleo ya kiuchumi nchini mwao wenyewe, si kama huendeshá tu mapambano ya kuwania ukombozi wa kitaifa dhidi ya ubeberu, lakini katika hali fulani hata huyaongoza hasa. Lakini ilivyokuwa wanataka kudumisha na kuimarisha mastakimu yao kama tabaka, katika kipindi cha mapambano ya kufa kupona (hasa wakati umma mkubwa unapokuwa umeshavutiwa kushiriki katika mapambano haya na kuhatarisha kuutokomeza utaratibu mzima wa unyonyaji) wao huanza kuyumbayumba na kupendelea zaidi kufanya mapatano na mabeberu na wapinga maendeleo wa ndani. Tabaka la wafanyakazi tu ndilo linalotokezea kuwa mpiganaji halisi na thabiti mpaka mwisho katika kuwania ukombozi wa kitaifa na usawa wa kitaifa katika dahari ya ubeberu.

Kawaida iliyovumbuliwa na Lenin ya kuwako mielekeo miwili ya kihistoria katika suala la ma-

taifa imekuwa ndio msingi wa siasa ya uhusiano wa mataifa ifuatwayo na tabaka la wafanyakazi na jeshi lake la mbele, yaani, chama chake cha kisiasa. "Mpango wa wafuasi wa maongozi ya Marx juu ya uhusiano wa mataifa wazingatia mielekeo yote miwili na kutetea, kwanza, usawa wa mataifa na lugha na kutoruhusika kuwako *mapendeleo* yo yote katika upande huu (na pia haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe...); pili, mwongozo wa ushikamano wa kimataifa na mapambano yasiyopatanishika dhidi ya mtindo wa kuliambukiza tabaka la wafanyakazi maradhi ya kibwanyenye ya kujibagua kitaifa, hata kwa njia ya kistaarabu kabisa", Lenin alisisitiza.

Nadharia ya Lenin kuhusu mielekeo miwili ya kihistoria katika suala la mataifa ni silaha madhubuti katika kupambana na uenezaji wa mtindo wa kukataa utaifa unaotetewa na wataalamu wa kibwanyenye wa elimujamii na Wasoshalisti wa mrengo wa Kulia ambao wanaipinga fikira ya mamlaka ya kitaifa na kudai kwamba mapambano ya kuwania ukombozi wa kitaifa ni yenye kupinga maendeleo na kusababisha ati kuzuka mtindo wa kujipendelea kitaifa. Wakati huo huo, mwendo wa kimaendeleo wa kujongeleana karibu zaidi kwa mataifa na uvunjikaji wa mapingamizi yanayotenganisha mataifa waweza kutumika, Lenin alisema, kama nguvu kuu ya kuugeuza ubepari kuwa usoshalisti, mradi tu mwendo huu usitegemee mabavu.

Lenin alipambanua pande mbili za siasa ya tabaka la wafanyakazi kuhusu mataifa: wito wa haki ya kujiamulia wenyewe kitaifa na wito wa

umoja wa mataifa yote. Tabaka la wafanyakazi linapigania usawa kamili na umoja wa mataifa yote. Wakati huo huo, tabaka la wafanyakazi na chama cha kimapinduzi linajiwekea shabaha wa kutetea umoja wa mapambano ya wafanyakazi na jumuiya za wafanyakazi pasina kujali jitihada za mabwanyenye za kutaka kuleta utengano baina ya mataifa.

Lenin aliweka nadhari kubwa sana juu ya tatizo la uhusiano baina ya mataifa yanayokandamizwa na yale yanayokandamiza. Alifichua tofauti iliyoko baina ya aina mbili za utaifa (ile ya mataifa yanayokandamizwa na ya mataifa yanayokandamiza) na maoni mbalimbali ya tabaka la wafanyakazi kuhusiana nazo. Utaifa wa mataifa yanayokandamiza dhahiri ni wenye kupinga maendeleo, wa kikoloni na usiopatanishika kamwe na maslahi ya demokrasi. Unajitokeza kwa umbo la kiburi cha dola kuu na ubaguzi wa rangi. Taifa kandamizi linatumia tofauti za lugha, dini na desturi kama kisingizio cha kuyadidimiza mataifa madogo na dhaifu zaidi kwa ajili ya kujikumbia mafaida ya uhodhi, huku likijitahidi kuliingiza tabaka la wafanyakazi katika mkondo mkuu wa siasa yake. Kinyume chake, utaifa wa mataifa yanayokandamizwa ni wenye kupinga ubeberu na una chipukizi za demokrasi, ukitokena mageuzi ya kimaendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Madai Makuu ya Mpango wa Mabolsheviki wa Uhusiano Baina ya Mataifa

Kwa mujibu wa maongozi makuu ya kinadharia ya suala la mataifa kama yalivyotungwa na Marx na Lenin, vyama vya kifanyakazi vinafafanua siasa yao wenyewe ya uhusiano baina ya mataifa na kutoa miito yao wenyewe kuhusu jambo hili ikitegemea juu ya tabia ya majukumu ya kijamii-kiuchumi na ya kisiasa yanayozikabili nchi zao katika kila kipindi kimoja maalum.

Kabla tabaka la wafanyakazi halijatwaa madaraka nchini Urusi, Chama cha Mabolsheviki kilishughulikia mara tatu kazi ya kuufafanua na kuusahihisha mpango wake kuhusu suala la mataifa. Katika kadhia ya kwanza, ilihusika na uundwaji wa Chama, wakati mpango wake wa kijumla ulipokuwa ukitungwa. Katika maandishi na makala zake kama vile *Nani "Marafiki" wa Umma na Jinsi Wanavyowapiga Vita Wademokrati wa Kisoshalisti; Maendeleo ya Ubepari Nchini Urusi; Kuhusu Ilani ya "Umoja wa Wademokrati wa Kisoshalisti wa Kiarmenia"; Suala la Mataifa Katika Mpango Wetu,* na nyinginezo zilizoandikwa toka 1894 mpaka 1903, hadi wakati wa Mkutano Mkuu wa Pili uliopitisha Mpango wa Chama, Lenin alitoa mashauri muhimu juu ya maana yenyewe hasa ya mataifa, kawaida za uchomozaji wao na maendeleo yao, na majukumu ya tabaka la wafanyakazi kuhusu suala la mataifa.

Baadaye, Chama kiliyaainisha majukumu haya kabla na wakati wa kutukia kwa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, ambapo suala la mataifa

lilifanywa kuwa kali hasa na ambapo usoshalisti wenye kiburi cha utaifa ulienea sana ndani ya harakati za tabaka la wafanyakazi. Mnamo miezi 18 kabla ya vita na katika mwaka wake wa mwanzo (yaani, toka 1912 mpaka 1914), Lenin aliandika makala na maandishi mengine mbalimbali yapatayo 15 kuhusu suala la mataifa. Maandishi muhimu zaidi kati ya hayo yalikuwa ni *Tabaka la Wafanyakazi na Suala la Mataifa*; *Tasnifu Kuhusu Suala la Mataifa*; *Haki ya Mataifa Kujiamulia Mambo Yao Wenyewe*, na *Maelezo ya Ukosoaji Kuhusu Suala la Mataifa*. Mikutano miwili ya Chama ilifanywa ili kujadili suala hili.

Baada ya Mapinduzi ya kibwanyenye-kidemokrasi ya Februari 1917 katika Urusi, kikishika njia ya kuyageuza mapinduzi haya kuwa ya kisoshalisti, Chama kiliweka nadhari kuu juu ya suala la mataifa.

Mwongozo wa Ushikamano wa Kimataifa wa Matengenezo ya Chama

Mkutano Mkuu wa Pili wa Chama cha Kisoshalisti cha Kidemokrasi cha Wafanyakazi cha Urusi (cha Mabolsheviki) – CKKWU(Mab.) * – ambao ulipitisha Mpango wa Chama, hasa kuhusu suala la mataifa, uliweka nadhari kubwa juu ya jina la Chama na kanuni za matengenezo. Kama Lenin alivyoelezea, yapasa Chama kishikilie

---

* Hivyo ndivyo Chama cha Kikomunisti cha Urusi kilivyokuwa kikiitwa mpaka 1918.– *Mfasiri.*

msimamo wa umoja wa kimataifa siyo tu kwa tabia na muundo wake, bali pia kionekane kuwa ni hivyo. Ili kuondosha fikira yo yote yenye kuonyesha kuwa chajibagua kitaifa, Chama kilijiita kuwa cha Urusi (*Rossiiskaya*) wala siyo cha Kirusi (*Russkaya*).

Kwenye mkutano mkuu huo, kulizuka mgongano baina ya maongozi mawili yasiyopatanishika kuhusu msingi wa kimatengenezo wa Chama: mwongozo wa umoja wa wafanyakazi wa kimataifa ambao chini yake wafanyakazi wa mataifa yote waliweza kuwa wanachama wa jumuiya zilizoshikamana za Chama, na ule wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa, ambao ulitilia mkazo zaidi juu ya umoja wa taifa kuliko wa tabaka.

Kwa kutofautiana na Lenin na wenzake, ambao walishikilia kwamba wafanyakazi wa mataifa yote lazima waungane ndani ya jumuiya moja yenye uongozi mkuu, wana-*Bund* (wanachama wa jumuiya ya wafanyakazi wa Kiyahudi ambao walijiunga na CKKWU) waliita paweko jumuiya yenye kujiendesha yenyewe kwa mambo yake ya ndani na, kwa hakika hasa, walitaka kuwafarakisha wafanyakazi kwa mujibu wa taifa au kabila lao. Wana-*Bund* walijitokeza mbele kupinga uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi, mwongozo mkuu wa kimatengenezo wa Chama kifuatacho mafunzo ya Marx, wakidai kwamba jumuiya za kifanyakazi hazina budi kutenganishwa kwa mujibu wa mataifa yao na kwamba CKKWU kigeuze muundo wake kuwa kama jumuiya ya shirikisho ya vyama vya Kisoshalisti vya Kidemokrasi vya kitaifa.

Chama kiliyakataa madai haya. Lenin aliandika: "...Yatupasa tutende kama jumuiya shupavu iliyoshikamana na yenye uongozi mmoja mkuu, tuwe na tabaka zima la wafanyakazi nyuma yetu, pasina ubaguzi wa lugha au kabila, tabaka la wafanyakazi ambalo umoja wake unaimarishwa kwa utanzuaji wa pamoja wa mfululizo wa matatizo ya kinadharia na kimatendo, wa mbinu na matengenezo; wala haitupasi kuunda jumuiya ambazo zingesonga mbele mbalimbali, kila moja ikishika njia yake yenyewe; haitupasi kuidhoofisha nguvu ya shambulio letu kwa kufarakana katika vyama mbalimbali chungu nzima vya kisiasa; haitupasi kuleta mfarakano na utengano na kisha kutubidi kuponyesha maradhi ya kujitakia wenyewe kwa kutumia hizo dawa za kubandika zivumazo sana ziitwazo 'shirikisho'."

Mabolsheviki, wakiongozwa na Lenin, walishikilia maongozi ya umoja wa kimataifa ya Chama cha aina mpya, wakiendesha mapambano ya kishupavu ya kuwania ushikamano wa jumuiya za Chama, kwa ajili ya kuimarisha umoja wake wa kimataifa.

Mapambano hayo hayakuwa na umuhimu unaohusika na mambo ya ndani tu ya Chama. Yalifungulia njia kwa mapambano ya kutandaa na hata ya mtataniko zaidi ambayo ilikibidi Chama kiyaendeshe ili kuwaunganisha pamoja wananchi wafanyao kazi wa Urusi na kuchanganyisha jitihada za kimapinduzi za wafanyakazi wa mataifa yote.

Dai la Haki ya Mataifa Kujiamulia Mambo Yao Wenyewe

Wakichukua msimamo wa kupinga mkandamizo wa kitaifa na kuwania usawa wa mataifa yote, Mabolsheviki walitoa mkururo wa mapendekezo ya vitendo, ambayo yalikuwa ni sehemu ya mpango wao kuhusu suala la mataifa wakati wa mapambano ya kupigania mapinduzi ya kidemokrasi ya kibwanyenye. Kilichokusudiwa kwa hayo kilikuwa ni kuziunga mkono harakati za kimapinduzi dhidi ya utawala wa mfalme, kuliunga mkono taifa dogo lo lote linalokandamizwa, dini yo yote inayodhiliwa na kundi lo lote la kijamii linalonyanyaswa katika juhudi zake za kuwania usawa.

Mabolsheviki walidai usawa kwa raia wote, pasina kujali jinsia, dini, rangi wala kabila.

Dai la kutaka usawa wa mataifa lilifungamana sana na haja ya kuanzisha mfumo wa kijamhuri ulio wa kidemokrasi vilivyo.

Kati ya madai yote halisi yenye kuhusiana na juhudi za kuwania usawa wa mataifa, katika hali hiyo ya siasa ya kikoloni ya utawala wa mfalme na ubaguzi kwa zaidi kuliko mataifa na makabila 100, madogo kwa makubwa, Lenin alilipembua dai la haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe kama ndilo lililo muhimu na la lazima kabisa kwa Chama kifuatacho maongozi ya Marx.

Wageugeu mbalimbali walimshutumu Lenin kwa hilo jambo kwamba dai la haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe ati lilikusudiwa

kuligawanya dola zima la Urusi.

Lakini kweli, dai hilo lilikusudia kwamba wafuasi wa maongozi ya Marx walitaka dola hilo zima lenye mataifa mengi ligawanyike? Hasha! Lenin na Mabolsheviki waliufahamisha umma kwamba mbali na kutaka kuona dola hili kubwa lenye mataifa mengi likigawanyika katika vijidola vidogo vidogo vya kitaifa, wafuasi wa maongozi ya Marx wanaamini kwamba madola makubwa yanatoa fursa njema zaidi kwa mapambano ya kitabaka ya wananchi wafanyao kazi. Lakini hayo hayawezi kutukia isipokuwa paweko imani baina ya wananchi wafanyao kazi wa mataifa mbalimbali mnamo mipaka ya dola moja. Na njia pekee ya kuondosha hali ya kutuhumiana baina ya mataifa, iliyokuwako wakati ule, ni kulipatia kila moja lao haki ya kuamua mustakbali yao wenyewe. Kwa hali hii, mataifa yenyewe si lazima kuwa yatataka kujitenga. Akiikataa shutuma hiyo ati kwamba Mabolsheviki wanataka kuliangamiza dola la Urusi, Lenin alisema kwamba ni wapinga maendeleo na maharamia wa magenge ya shari tu, ndio waliokuwa kwa hakika hasa wakijaribu kuiangamiza, kwani siasa yao ya kukandamiza mataifa ndiyo iliyopelekea kuiseleleza Urusi katika hali ya kuzorota na uhasama baina ya mataifa yake, ilhali utambuliwaji wa haki ya kujiamulia wenyewe ulipunguza hatari ya kugawanyika. Urusi haiwezi kuwa dola kuu na lililosonga mbele isipokuwa mataifa yake yaungane juu ya msingi wa usawa na demokrasi.

Katika kipindi cha ukweaji mpya wa harakati za kimapinduzi wakati wa mkesha wa Vita Vi-

kuu vya Kwanza, Chama kwa mara nyingine tena kiliainisha msimamo wake na kutoa nyongeza zaidi kuhusu haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe. Azimio la Mkutano wa Kamati Kuu ya CKKWU (Mab.) katika 1913 lilitilia mkazo kwamba kwa haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe wafuasi wa Marx walikusudia haki ya kujitenga na kuunda dola huru. Maelezo hayo yalionyesha ari iliyo ya kidemokrasi vilivyo ya Mabolsheviki, ambao madai yao katika suala la mataifa hayakufungika kwa kuchukua hatua nusunusu tu, kwa kutofautiana na zile zilizochukuliwa na kila aina ya wapepeleaji kiburi cha utaifa na wale wanaopendelea kujibagua kitaifa.

Na ingawa Wakomunisti walitambua kwamba utanzuaji kamili wa suala la mataifa wategemea juu ya ukomeshwaji wa mfumo wa kinyonyaji, wao waliona kuwa inayumkinika kupata maendeleo makubwa katika upande huu hata chini ya ubepari kwa kuwania demokrasi ya upeo mpana zaidi na kupinga hatua za ubaguzi zichukuliwazo dhidi ya baadhi ya mataifa na mapendeleo kwa mataifa mengine.

Katika maandishi yake, *Haki ya Mataifa Kujiamulia Mambo Yao Wenyewe*, Lenin alifahamisha kwamba ukataaji wa dai la kutaka haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe unahitilafiana na mwelekeo wa maendeleo huru ya mataifa, unapelekea kuzidisha uhasama baina ya mataifa na, hatimaye, unausukumiza umma wa wananchi wafanyao kazi kwa mabwanyenye wao wenyewe, ukizidisha tuhuma kwa wafanyakazi wa Ki-

rusi na Chama cha Mabolsheviki miongoni mwa wananchi wafanyao kazi wa maeneo yakaliwayo na watu wa mataifa na makabila mengine. Kinyume chake, utolewaji wa dai hilo wasaidia kuwaelimisha wananchi wafanyao kazi wa mataifa yanayokandamizwa kwa ari ya ushikamano wa kimataifa, kuziunganisha pamoja nguvu za kimapinduzi chini ya uongozi wa tabaka la wafanyakazi la mataifa yanayokandamiza na kuupanua msingi wa mapinduzi ya kijamii.

Katika kutoa dai hilo, tabaka la wafanyakazi linakuja kuongoza harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa, likitwaa mahali pa mabwanyenye wa kitaifa wanaoyumbayumba, ambao wanaogopa mapinduzi. Kama matokeo yake, harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa zinachanganyika na harakati za tabaka la wafanyakazi katika mkondo mmoja wa kimapinduzi.

Lakini, azimio la mkutano wa Kamati Kuu ya Chama uliotajwa hapo kabla lilitilia mkazo kwamba haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe, pamoja na haki ya kujitenga mbali, isibabaishwe na suala la kama kujitenga mbali kunafaa. Dai lenyewe hasa lamaanisha utambuliwaji kamili wa haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe. Vyama vifuatavyo maongozi ya Marx havipendekezi kujitenga mbali, bali vyaitambua tu haki ya kufanya hivyo, sawa na haki yo yote ile nyingine ya kidemokrasi. Ama kuhusu kujitenga kwenyewe hasa kwa taifa na kuunda dola mbali la kitaifa, kwategemea juu ya hali zenyewe halisi, juu ya kama hayo yanatosheleza maslahi ya tabaka la wafanyakazi na wa-

nanchi wote wengine wafanyao kazi, maslahi ya ustawi wa kimaendeleo wa taifa, kwanza kabisa maendeleo yake ya kiuchumi, na maslahi ya mapambano ya kitabaka ya wafanyakazi dhidi ya kila aina ya unyonyaji. Vyama vifuatavyo maongozi ya Marx vyachukulia kwamba kila taifa lina matabaka mbalimbali, ambayo maslahi yao katika masuala ya kujitenga mara nyingi ni yenye kuhitilafiana kabisa. Mbinu zitumiwazo na chama kifuatacho maongozi ya Marx katika suala la mataifa, uungaji mkono wake wa harakati hizi au zile za kitaifa, na maumbo yenyewe halisi ya mamlaka ya kiserikali ya mataifa huamuliwa kwa msaada wa ukadiriaji wa pande zote wa maslahi ya maendeleo ya mapinduzi ya kisoshalisti, uchambuzi wa mambo yote ya kijamii-kihistoria ya ndani na ya nje.

Chama kifuatacho maongozi ya Marx chaweza kuunga mkono jitihada ya taifa kutaka kujitenga mbali katika kipindi maalumu cha kihistoria, lakini papo tu hali ya mambo ikibadilika chaweza kupinga kujitenga mbali. Ikiwa mamwinyi na mabwanyenye wanajaribu kuwagawanya wananchi wafanyao kazi kwa mujibu wa mataifa yao kwa mwito wa kujiamulia wenyewe kwa mataifa, basi tabaka la wafanyakazi na chama chake linapambana na msimamo huu upingao maendeleo kwa juhudi za kupigania muungano wa kimataifa wa watu wote wafanyao kazi. Historia mara nyingi imeona utanzuaji upingao maendeleo wa suala la kujitenga, wakati mabwanyenye wa kibeberu pamoja na mabwanyenye wa kitaifa na kikundi cha juu cha mamwinyi walipopania kuun-

da "madola ya kitaifa" ili kuzididimiza harakati za umma katika madola haya na kuweka utawala wao wenyewe wa kitabaka.

Wakati huo huo, azimio la Mkutano uliotajwa hapo kabla lilitilia mkazo kwamba kwa mataifa yale yasiyotaka kujitenga na serikali kuu, Chama kilipendekeza yapatiwe madaraka makubwa ya kujitawala kwa mambo yao ya ndani na kujiendesha wenyewe kienyeji kwa njia ya kidemokrasi, na mipaka ya maeneo yao kuamuliwa juu ya msingi wa makadirio ya wakazi wenyewe wa huko kuhusu hali za kiuchumi na za maisha katika kila eneo hilo linalohusika na mpangiko wa kitaifa wa wakazi hao.

Ikiwa kabla ya Mapinduzi ya Februari 1917, Lenin alifungamanisha utekelezaji wa haki ya kujiamulia wenyewe na mapinduzi ya kibwanyenye-kidemokrasi, basi baada ya mapinduzi hayo, na hasa baada ya Mkutano wa Aprili, 1917 wa Chama, ambao ulijadili suala la mataifa, alikuja kuufungamanisha vilivyo ukombozi wa mataifa yanayokandamizwa pamoja na uwekwaji wa utawala wa wafanyakazi na wakulima. Mawazo ya Lenin yaliyoelezewa katika makala yake *Majukumu ya Tabaka la Wafanyakazi katika Mapinduzi Yetu* (uhuru kamili wa kujitenga, kujitawala wenyewe kienyeji na kitaifa, dhamana za kinaganaga kwa haki za mataifa madogo) yalikuwa ndio msingi wa maazimio ya Mkutano wa Aprili 1917. Kwa mara ya mwanzo, Lenin aliingiza katika mpango wa uhusiano baina ya mataifa majukumu ya sikuzijazo ya siasa kuhusu mataifa (Chama cha tabaka la wafanyakazi "kinawania *kuyajongeza* matai-

fa *karibu zaidi*, na kuleta *muungano mkubwa zaidi*") na kufafanua waziwazi masharti ya utekelezaji wa mpango huo (muungano huru wa kidugu wa wafanyakazi na watu watumiao jasho lao wa mataifa yote). Chama kilikuwa sasa kimeshaandaliwa kwa mpango wa kisayansi wa kwendea katika mapinduzi ya kisoshalisti.

Ukosoaji wa Mpango wa Kigeugeu wa Kujitawala Wenyewe Kitaifa na Kiutamaduni

Kwa kutofautiana na dai la kutaka haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe, kama lilivyotolewa na Mabolsheviki, wageugeu walidai kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani ya kitaifa na kiutamaduni.

Maana hasa ya dai hilo la wageugeu ilikuwa ni kwamba kila taifa linaloishi katika dola la mataifa mengi linakuwa ni kama kundi mbali lenye kujitawala lenyewe. Watu wa kila taifa, pasina kujali mahali wanakoishi, wanaingizwa katika orodha ya pamoja, na kwa kutegemea orodha kama hizo kunachaguliwa Mabaraza ya Kitaifa ili kushughulikia masuala ya lugha na utamaduni wa kila taifa. Kwa hakika hasa, dai la kutaka kujitawala wenyewe kitaifa-kiutamaduni lilijumlikia kuwa ni haki ya kuanzisha shule za kitaifa na kutumia lugha ya kitaifa.

Kwa hivyo basi, kujitawala wenyewe kulipendekezwa siyo kwa eneo maalumu lenye wakazi ambao kwa vikubwa sana ni wa jadi moja na wenye fungamano madhubuti za kiuchumi (ka-

ma wafuasi wa Marx walivyodai), bali kwa muungano wa watu wa taifa hili au lile pasina kujali mahali wanakoishi. Miungano kama hiyo, watetezi wake wanadai, haipasi kupewa madaraka ya kisiasa, bali ihusike na mambo ya utamaduni tu pekee.

Lenin alifahamisha kwamba nadharia hiyo ya kujitawala wenyewe kitaifa na kiutamaduni katika Urusi iliazimwa kutoka Austria, ambako viongozi wa Chama cha Kisoshalisti cha Kidemokrasi, ambao walionekana kama mabingwa wakuu wa nadharia ya suala la mataifa na pia kama watekelezaji wake wakuu kwa vitendo, walitunga mpango wa mageuzi madogo madogo wa mbaguano wa mataifa (kujitawala wenyewe kitaifa-kiutamaduni), ambao uliyasaidia matabaka yanayotawala kuwagawanya wananchi wafanyao kazi wa Austria-Hungary yenye mataifa mengi na kuhifadhi mastakimu yao ya kinyonyaji.

Mpango huo wa mbaguano wa mataifa ulinyakuliwa na wana-*Bund*, Wademokrati wa Kisoshalisti wa Poland, Mamensheviki, na baadaye na makundi mengine yapendeleayo kujibagua kitaifa katika vikosi mbalimbali vya kitaifa vya harakati za tabaka la wafanyakazi.

Lenin alionyesha kwamba nadharia ya kujitawala wenyewe kitaifa-kiutamaduni ilikuwa si ya kisayansi, isiyofaa kisiasa, na yenye madhara kwa harakati za tabaka la wafanyakazi na za ukombozi wa kitaifa. Mpango huo wa kujitawala wenyewe kitaifa-kiutamaduni unakwenda kinyume na kawaida za kimaendeleo za ustawi wa kijamii na mwelekeo wa mataifa kujongeleana pamoja kuribu zaidi.

Dai kuu la mpango huo ni kuhifadhi "utamaduni wa kitaifa wa namna moja". Dai hili pia si la kisayansi wala halitekelezeki, kwani mataifa ya kibwanyenye yamegawanyika katika matabaka mawili makuu yenye kuhasimiana, na kwa hakika hasa kila moja lao lina utamaduni wake wenyewe wa kitaifa, ambao mwelekeo wake wa kiitikadi watofautiana na ule wa jingine. Lenin alitilia mkazo kwamba kuna mataifa mawili katika kila taifa la kisasa na aina mbili za utamaduni katika utamaduni wa kila taifa: ule wa tabaka linalotawala na wa tabaka linalokandamizwa. Hiyo ndiyo maana kwa nini haimpasi mtu kuupambanisha utamaduni mmoja wa kitaifa na mwingine (mtokezo wa kujibagua kitaifa), bali utamaduni wa kifanyakazi wa kidemokrasi na ule wa kibwanyenye (mtokezo wa ushikamano wa kimataifa).

Badala ya dai la kigeugeu la "utamaduni wa kitaifa wa namna moja", Lenin alitoa mwito wa utamaduni wa kimataifa wa harakati za kidemokrasi na za kifanyakazi, mwito wa usoshalisti. Lakini pamoja na hayo, Lenin hakukanya utamaduni wa kitaifa kama hivyo ulivyo. Zaidi ya hayo, alitilia mkazo kwamba utamaduni hauwezi kuwa nje ya taifa, bali kwamba Chama kifuatacho maongozi ya Marx kinapokea kutoka katika *kila* utamaduni wa kitaifa vyanzo vile tu *pekee* ambavyo ni vya kidemokrasi na kisoshalisti. Wafanyakazi wa mataifa yote yana siasa moja tu ya elimu: uhuru kwa lugha ya kienyeji, na elimu ya kidemokrasi isiyofungamana na dini. Hiyo ndiyo maana kwa nini jukumu lenyewe likawa siyo

kuanzisha shule za kitaifa, bali kufundisha lugha za kienyeji katika shule za kawaida.

Mpango wa kujitawala wenyewe kitaifa-kiutamaduni kwa hakika hasa ulikuwa na azma ya kuyapatanisha matabaka yenye kuhasimiana kwa ajili ya ati "maslahi ya kitaifa ya pamoja". Akifichua hatari za mpango huo, Lenin alielezea maana yake hasa kama ni kujitenga, ambako kunapelekea kuwagawanya wananchi wafanyao kazi kwa mujibu wa mataifa yao, jambo ambalo halina budi kudhoofisha mapambano dhidi ya utawala wa mfalme na wanyonyaji wote kwa jumla.

Mapambano ya Kupinga Aina Zote za Mtindo wa Kibwanyenye wa Kujibagua Kitaifa

Ufichuliwaji wa kiini cha mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa na mapambano ya kupinga aina zake zote mbalimbali zilikuwa ni sehemu kuu zilizofungamana na siasa ya Mabolsheviki kuhusu mataifa, sharti lenye kuwawezesha wananchi wafanyao kazi kuuelewa mpango wa Lenin kuhusu suala la mataifa.

Kwa kutumia siasa yake ya kiburi cha taifa kuu utawala wa mfalme ulitaka kuigubika fahamu ya kitabaka ya wafanyakazi wa Kirusi, kuwageuza kuwa washiriki katika siasa ya kuyakandamiza mataifa mengine. Katika maeneo yakaliwayo na mataifa madogo, utawala wa mfalme uliuziba mtokezo wo wote ule wa fahamu ya kitaifa.

Ukandamizi ulikuwa siyo silaha pekee, iliyotumiwa na utawala wa mfalme kuupinga umma ambao ulijaribu kuteta dhidi ya mkandamizo wa kitaifa. Wakati huo huo, ulibandikiza kiburi cha taifa kuu "kutoka kwa juu", na katika kujibiza hayo kulizuka mtindo wa kujibagua kitaifa katika sehemu zikaliwazo na mataifa madogo, ambao mara nyingi uliendelea kuja kuwa kiburi cha utaifa dhahiri shahiri. Ili kuzuia mchemko wa kutoridhika kunakozidi kuwa kwingi miongoni mwa wananchi wafanyao kazi katika sehemu zikaliwazo na mataifa madogo, mabwanyenye wa Kirusi walishirikiana na vijitabaka vya kienyeji vilivyopata ufanisi.

Lakini suala la mataifa katika Urusi lilichukua mapeo makubwa sana hata hakukuwa na chama cho chote cha kisiasa ambacho kingeweza kulipuuza. Kila chama kilipendekeza njia zake wenyewe za utanzuaji wake kwa mujibu wa maslahi ya tabaka au kundi la jamii kinaloliwakilisha.

Mabwanyenye wa kiliberali wa Kirusi walijishaua kwa miito ya kidemokrasi, ilhali kwa hakika hasa maoni yao kuhusu suala la mataifa yalikuwa ni sawa na yale ya waliokuwa wakitetea utawala wa mfalme usiopakika. Lenin alionyesha kwamba mabwanyenye wą kiliberali wa mataifa yote, na kwanza kabisa mabwanyenye wa taifa la Warusi, walitaka mapendeleo kwa taifa lao na kushikilia mtindo wa kujibagua kitaifa.

Mabwanyenye wa kitaifa wa mataifa yanayokandamizwa, huku wakijiunga na utawala wa mfalme na mabwanyenye wa Kirusi katika kuzikandamiza harakati za kuwania ukombozi wa ki-

taifa katika sehemu zao, wakati huo huo walijaribu kuwashawishi kiitikadi wananchi wafanyao kazi, wakitoa miito ya kudai haki fulani fulani za uhuru wa kitaifa, mabaraza ya uwakilishi ya kitaifa, na haja ya kukuza lugha na utamaduni wao.

Wasomi wa kibwanyenye wenye kujibagua kitaifa wa Waukraina, Wapoland, Wayahudi, Wageorgia, Waarmenia, Walatvia na wa mataifa mengine walipalilia kiburi cha utaifa miongoni mwa watu wao wenyewe. Wakilitumia dukuduku la kutoridhika miongoni mwa umma, wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa walitaka kuwajaza sumu watu wao wawachukie Warusi na utamaduni wao. Waislamu wenye kujibagua kitaifa walieneza maoni ya kidini-kisiasa kwa msaada wa maongozi ya umoja wa Waislamu (*Pan-Islamism*), ambayo kwa mujibu wake, mataifa ya Kiislamu yanaweza kupata uhuru siyo kwa kuwapiga vita wanyonyaji, bali kwa kuungana kwa imani yao ya pamoja (wanyonyaji halikadhalika na wanyonywaji) ili kuyateka maeneo makubwa ya nchi na kuyaweka mataifa yasiyokuwa ya Kiislamu chini ya amri yao.

Katika sehemu ya Asia ya Kati iliyokuwa chini ya utawala wa mfalme wa Kirusi, wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa waliupaza mbinguni "ujumbe wa kustaarabisha" wa utawala wa mfalme na kujitokeza mbele kuwatetea makabaila (mabai) wa kimwinyi na mabwanyenye wa kienyeji wanaoanza kuchipuka.

Nadharia za kisoshalisti za uhange za vyama vya kibwanyenye uchwara zilikuwa na chipukizi

fulani za kidemokrasi zinazotokana na hamu ya kuondosha ubaguzi kwa mataifa yakandamizwayo. Lakini madai yao makuu kuhusu suala la mataifa yalionyesha kushikilia msimamo wa pamoja na wanaitikadi wa kibwanyenye. Ilivyokuwa viliufichiafichia msimamo wao kwa bendera ya maongozi ya Marx, maoni yao ambayo kimsingi ni ya mtindo wa kujibagua kitaifa yalikuwa ya hatari hasa kwa harakati za kimapinduzi za tabaka la wafanyakazi. Mtindo wa kujibagua kitaifa wa vyama vya kibwanyenye uchwara ulijitokeza katika huko kuwania kuwatenganisha wafanyakazi wa mataifa yao na wale wa mataifa mengine, kuunda jumuiya mahsusi za wafanyakazi kwa mujibu wa mataifa, na haya mtu akitaka asitake yalifalia hasa maslahi ya mabwanyenye wa mataifa makuu.

Kulikuwa na makosa makubwa na miyumboyumbo kuhusu suala la mataifa miongoni mwa Wademokrati wa Kisoshalisti wengi wa mrengo wa Kushoto pia, na hata baadhi ya wapiganiaji thabiti wa lengo la tabaka la wafanyakazi walipotoka kutokana na msimamo barabara kuhusu suala hili.

Kwa hivyo basi, kuhusu jambo hilo la haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe – dai kuu la Mabolsheviki katika suala la mataifa – Chama cha Kikomunisti kilikabiliwa na muungano mpana kutoka utawala wa mfalme na magenge yake ya shari ya kupinga maendeleo, vyama viungavyo mkono utawala wa mfalme hadi Wademokrati wa Kisoshalisti wa mrengo wa Kushoto, yaani, muungano wa pamoja wa wa-

fuasi wa mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa.

Katika hali ya mtataniko kama hiyo, ambapo mapambano ya kitabaka yaliendeshwa kwa kushirikiwa kwa juhudi na kuathiriwa na vyama vya kisiasa chungu nzima na mbalimbali, Lenin aliona kwamba jukumu muhimu zaidi la Chama kifuatacho maongozi ya Marx lilikuwa siyo tu kuyathibitisha zaidi maoni yategemeayo maongozi ya Marx kuhusu suala la mataifa, bali kuifichua mbele ya umma tabia isiyo ya kisayansi na ya hatari ya maoni yenye kutetewa na vyama na mielekeo isiyofuata maongozi ya Marx, na pia kiini chao kipingacho maendeleo na mapinduzi.

Akiukashifu ubovu wa kutokuwa na maudhui yo yote wa miito itolewayo na maliberali na wageugeu wote wajiitao nafsi zao kama wademokrati, Lenin alionyesha kwamba tangazo lo lote la "usawa wa mataifa" ambalo halizatitiwi kwa kuyaunga mkono mapambano ya kuwania ukombozi wa mataifa yakandamizwayo ni la uhadaifu mtupu na halina maana yo yote.

Wakiupiga vita mtindo wa mataifa makandamizi kujibagua kitaifa, Mabolsheviki hawakusahau haja ya kuupiga vita mtindo kama huo kwa upande wa mataifa yanayokandamizwa vile vile. Chama cha Mabolsheviki kiliilaani siasa ya kuonyesha kiburi cha utaifa na ya kuyakandamiza mataifa mengine iliyokuwa ikiendeshwa na utawala wa mfalme na mabwanyenye wa Kirusi, na mtindo wa kujibagua kitaifa wa vyama vya kibwanyenye uchwara katika kurasa za magazeti yake, katika hotuba za viongozi wake, na katika

kazi yake ya kisiasa miongoni mwa umma. Mabolsheviki waliijibiza hatua yo yote ya serikali yenye kuonyesha kiburi cha utaifa, wakilitumia vilivyo jukwaa la Duma la Serikali (bunge).

Wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, Lenin pamoja na Mabolsheviki wenzake walifanya mengi sana kuukashifu mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa.

Tarehe 1 Novemba, 1914, Mabolsheviki walitoa ilani yenye kichwa cha maneno: *Vita na Chama cha Kisoshalisti cha Kidemokrasi cha Urusi* ambayo ilielezea maoni ya Chama cha Mabolsheviki kuhusu vita na kuukashifu mtindo wa kujibagua kitaifa na usoshalisti wenye kiburi cha utaifa. Ilani hiyo iliandikwa na Lenin na kupitishwa na jumuiya za mitaani za Chama, na kusambazwa nchini kote Urusi kwa mamilioni ya nakala.

Wakipambana na mtindo wa kutilia mkazo mno mipambanuo ya kitaifa katika siasa na katika mapambano ya kuwania ukombozi wa watu wafanyao kazi, na kudai kwamba suala la uhusiano wa mataifa liwekwe chini ya lile la kushughulikia maslahi ya kitabaka ya watu wafanyao kazi, Lenin na Mabolsheviki wenzake waliendesha mapambano yasiyosita pia dhidi ya mtindo wa kukanya utaifa. Lenin alifahamisha kwamba maongozi ya Marx yanaheshimu hadhi ya kila taifa na kuenzi mapokeo yake ya kitaifa. Yanathamini na kulinda vilivyo mafanikio yote ya utamaduni yanayoselelea kuwa ya kimaendeleo. Aliamini kwamba kuziteremshia umuhimu harakati za kitaifa ziinukiazo, halikadhalika mapambano ya kupinga mkandamizo wa kitaifa ku-

wa ni kinyume na maongozi ya Marx. Kilichofanya mtindo wa kukanya utaifa kuwa hata wa hatari zaidi ni kwamba unakataa kutambua vita vya kimapinduzi vya haki viendeshwavyo na mataifa manyonge dhidi ya wakandamizi wao.

Lenin alisema kwamba maongozi ya Marx hayaukatai kabisa mwito wa "kuhami nchi ya uzalendo", lakini yanautambua kuwa si sahihi, wa uwongo na wa madhara katika vita vya kibeberu, na kuutambua kuwa sahihi katika vita vya haki, vya ukombozi vya kulihami taifa dhidi ya uvamizi kutoka nje au majaribio ya kutaka kulitia utumwani.

Katika makala yake *Kuhusu Fahari ya Kitaifa ya Warusi*, Lenin alifahamisha kwamba wanamapinduzi wafuatao maongozi ya Marx wanachanganyisha huba kwa nchi yao ya uzalendo na ari ya umoja wa wafanyakazi wa kimataifa na kwamba uzalendo halisi wamaanisha kwanza kabisa mapambano dhidi ya "utawala wa mfalme, makabaila na mabepari wa nchi yake *mwenyewe* mtu, yaani, maadui *ahasi kabisa* wa nchi yetu".

Lenin alitilia mkazo daima: ama utaifa wa kibwanyenye au umoja wa kimataifa wa kifanyakazi, wala hapawezi kuwako cho chote kingine katikati. Aliandika: "Utaifa wa kibwanyenye na umoja wa kimataifa wa kifanyakazi – hii ndiyo miito miwili yenye kuhasimiana pasina kupatanishika ambayo inalingana na kambi kuu mbili za kitabaka katika ulimwengu wote wa kibepari, na kuwakilisha sera *mbili* (zaidi ya hayo, aina mbili za maoni kuhusu ulimwengu) katika suala la uhusiano wa mataifa".

Uelimishaji wa Wananchi Wafanyao Kazi Kwa Ari ya Umoja wa Kimataifa

Katika kupambana na mtindo wa kujibagua kitaifa na kuwania kuchukua hatua za kuleta mabadiliko makuu dhidi ya mkandamizo wa kitaifa, Chama cha Mabolsheviki kilikuwa kikitekeleza jukumu kuu, ambalo lingedhaminia kuukomesha kabisa mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa na kutanzua vilivyo tatizo la uhusiano wa mataifa, nalo ni jukumu la kuwaunganisha wananchi wote wafanyao kazi katika umoja ulioshikamana barabara wa kuendesha mapambano dhidi ya matabaka ya kinyonyaji, na kuwaelimisha kwa ari ya umoja wa kimataifa.

Jambo kuu lilikuwa ni kulielimisha na kuliunganisha tabaka la wafanyakazi lenyewe. Katika Urusi, tabaka la wafanyakazi liliambata mataifa mengi, na lilikuwa na mapingamizi ya kitaifa chungu nzima yakiwekwa baina ya vikosi vyake mbalimbali ambayo yalitokana na mkandamizo wa kitaifa. Mmojawapo wa pande muhimu za shughuli za Chama kifuatacho maongozi ya Marx ulikuwa ni kuyabomoa mapingamizi haya yaliyoko baina ya wafanyakazi.

Hali ya kutokuwa sawa kitaifa baina ya makundi mbalimbali ya kitaifa ndani ya tabaka la wafanyakazi ilizusha daima ugomvi baina yao, ambao mara nyingi ulikuwa mkali sana. Mabwanyenye waliutumia ugomvi huu na kujaribu kuchochelea uhasama ndani ya tabaka la wafanyakazi. Hiyo ndiyo maana kwa nini ikawa ni muhimu sana kwa Mabolsheviki kuliunganisha

tabaka la wafanyakazi. Ilikuwa ndiyo njia kuu ya kuzichanganyisha harakati za tabaka la wafanyakazi na zile za kuwania ukombozi wa kitaifa, njia ya kushajiisha mapambano ya ukombozi. Kilichofanya kazi hii kuwa rahisi zaidi kilikuwa ni hilo jambo kwamba wafanyakazi wa Kirusi, ambao walifaidia fursa fulani za umbele kwa kulinganisha na wawakilishi wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa, walikuwa hata hivyo wakinyonywa pasina huruma na kuendesha mapambano yasiyosita kwa ajili ya utengeneaji wa hali zao za maisha.

Lenin na Mabolsheviki wenzake waliweka nadhari kubwa juu ya kulielimisha tabaka la wafanyakazi la Urusi kwa ari ya umoja wa kimataifa, kwani lilikuwa ndilo shina kuu la wafanyakazi wa viwandani, wingi mkubwa wa wafanyakazi wenye ujuzi katika maeneo mengi zaidi yakaliwayo na mataifa madogo, wakiongoza mapambano ya kimapinduzi katika maeneo haya. Hoja za Mabolsheviki zilikuwa ni kwamba kufuzu kwa lengo zima la tabaka la wafanyakazi, pamoja na mapambano ya kuwania ukombozi wa kitaifa kulitegemea juu ya ari ya wafanyakazi wa Kirusi kushikilia msimamo wa umoja wa kimataifa, kuheshimu kwake haki za wananchi wafanyao kazi wa mataifa mengine, na kuwa tayari daima kuyaunga mkono mataifa yanayodhiliwa katika mapambano yao na kuyatetea maslahi yao.

Lenin alifahamisha kwamba tabaka la wafanyakazi la taifa kandamizi yapasa kwanza kabisa lifunzwe kuhami na kutetea uhuru wa mataifa yanayokandamizwa kuweza kujitenga mba-

li, huku wafuasi wa maongozi ya Marx wa mataifa yanayokandamizwa wakitilia mkazo katika kazi yao ya uelimishaji juu ya kuungana kwa hiari kwa mataifa. Chama kilieneza tasnifu ya Lenin kwamba kuna miongozo miwili, misimamo miwili katika suala la uhusiano wa mataifa: mmojawapo kati ya hiyo unawania kulijumuisha tabaka la wafanyakazi na kuwaunganisha watu wote watumiao jasho lao chini ya uongozi wake, ilhali wa pili wataka "kulijumuisha taifa", yaani, kuuvunja umoja wa kimataifa wa tabaka la wafanyakazi, kulichanganyisha pamoja tabaka la wafanyakazi na lile la mabwanyenye "wao wenyewe" mnamo uzio wa "maslahi ya kiutamaduni", jambo ambalo linazifalia mno nguvu zote zipingazo maendeleo. Umoja wa kimataifa ni sharti kuu la kuweza kupata ushindi dhidi ya mabwanyenye wa kibeberu.

Magazeti ya Kibolsheviki na makaratasi yaliyotolewa na matawi ya Chama ya mitaani yalitenda kazi kuu katika kuwaelimisha wanachi wafanyao kazi kwa ari ya umoja wa kimataifa. Magazeti ya Kibolsheviki yaliitumia kila kadhia ya ubaguzi wa kikabila ili kuonyesha kwamba njia pekee ya kuukomesha iko katika umoja wa kimataifa wa watu wafanyao kazi katika kumpiga vita adui yao wa pamoja, yaani, wanyonyaji. Matukio yaliyoonyesha sera ya uhusiano wa mataifa iliyotegemezwa juu ya ukandamizi kwa upande wa utawala wa mfalme yaliarifiwa kwa wingi sana katika magazeti ya Kibolsheviki, na kwa hivyo kusababisha majibizo nchini kote; kadhalika yalitengeneza kampeni za ushikamano

na mataifa yanayokandamizwa.

Jitihada za Mabolsheviki za kuhimiza ushikamano baina ya watu wafanyao kazi wa mataifa mbalimbali na wafanyakazi wanaogoma zilikuwa ni zenye umuhimu sana.

Mfano mmojawapo wa jinsi Mabolsheviki walivyokuwa wakiweza kuitumia kila hatua ipingayo maendeleo ichukuliwayo na utawala wa mfalme kwa ajili ya kuwaunganisha watu wafanyao kazi wa mataifa mbalimbali ulikuwa ni migomo ya wafanyakazi iliyofanyika Kiev, Kharkov, Tbilisi na miji mingine katika 1914 ili kuteta amri ya serikali ya kupiga marufuku sherehe ya kutumia miaka mia tangu siku ya kuzaliwa kwa Taras Shevchenko, mshairi na mdemokrati wa kimapinduzi wa Kiukraina. Midhahara ya kupinga serikali ilifanywa katika sehemu zote zikaliwazo na mataifa madogo.

Wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza, jitihada za Mabolsheviki za kuwaelimisha wananchi wafanyao kazi kwa ari ya umoja wa kimataifa zilisaidia kuvigeuza vita vya kibeberu kuwa vita vya nchini.

Baada ya Mapinduzi ya Februari 1917 (ya kibwanyenye-kidemokrasi), Mabolsheviki walitumia hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ya Muda (kukataa kuipa Ukraina uhuru wa kujitawala kwa mambo ya ndani, kufyatulia risasi maandamano ya amani ya wafanyakazi mjini Petrograd, kukataa kusitisha vita, n. k.) ili kuuonyesha umma kwamba mabwanyenye walionyakua utawala waliendelea na siasa ya kikoloni ya utawala wa mfalme.

Vyama vya kibwanyenye uchwara katika Masovieti (Mabaraza) ya Wajumbe wa Wafanyakazi na Maaskari viliiunga mkono moja kwa moja siasa iliyokuwa ikiendeshwa na Serikali ya Muda. Vyama kama hivyo ambavyo vilichipuka kwa wingi sana katika sehemu zikaliwazo na mataifa madogo, vilichelea mchemko wa kimapinduzi miongoni mwa umma na kwa hakika hasa viliendea upande wa mabwanyenye wa Kirusi ili kujiepusha na mapinduzi yaliyokuwa yanakaribia kufumuka. Mabolsheviki walionyesha njia barabara pekee ya kukomesha mkandamizo wa kitaifa, nayo ni kuwaunganisha watu watumiao jasho lao wa mataifa manyonge na tabaka la wafanyakazi la Urusi dhidi ya wanyonyaji wao wa pamoja. Katika mapambano baina ya mielekeo miwili katika harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa nchini Urusi (za kibwanyenye-kizalendo na za kimapinduzi-kidemokrasi) Mabolsheviki walizipatia ushindi nguvu za kimapinduzi-kidemokrasi.

Kwa hivyo basi, shughuli za Chama cha Mabolsheviki katika kutunga na kuueneza mpango wake wa uhusiano baina ya mataifa na kuikashifu sera ya kikoloni iliyokuwa ikiendeshwa na utawala wa mfalme na Serikali ya Muda (ya mabwanyenye), kadhalika kazi yake isiyosita miongoni mwa umma ili tabia inayokwenda kinyume na maslahi ya wananchi ambayo inatokezwa katika aina zote za mitindo ya kibwanyenye ya kujibagua kitaifa na kuelimisha watu wafanyao kazi kwa ari ya umoja wa kimataifa, zilikiwezesha kuujumuisha umma unaokandamizwa chini ya uongozi ya kisoshalisti.

MAONGOZI YA LENIN KUHUSU MAMLAKA YA KISERIKALI YA KITAIFA NA UTEKELEZWAJI WAO MNAMO KIPINDI CHA KWANZA CHA UTAWALA WA KISOVIETI

Dai la Mpango wa Chama Lililotungwa Katika Sheria

Upinduliwaji wa matabaka ya kinyonyaji kama matokeo ya Mapinduzi Makuu ya Kisoshalisti ya Oktoba na uwekwaji wa utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi ulikuwa ndilo sharti kuu la kukomesha mkandamizo wa kitaifa na uhasama wa kitaifa, la kudhaminia usawa na ushirikiano baina ya mataifa yote, na kuwawezesha wafanyakazi wa Urusi kupata imani ya ndugu zao wa mataifa mengine. Jukumu la tabaka la wafanyakazi lililotwaa madaraka lilikuwa ni kuyaunganisha mataifa mbalimbali ya Urusi juu ya msingi wa usawa halisi. Mabolsheviki walijiandaa vilivyo kwa mpango wa Lenin kuhusu suala la mataifa katika kulikabili jukumu hili.

Madai haya yaliyotolewa katika mpango huo yalikuwa siku zote yakifungamanishwa na haja ya kuyafanya mahusiano ya kijamii kuwa ya kidemokrasi na kutekeleza majukumu ya kitabaka ya wafanyakazi.

Hata kabla ya Mapinduzi ya Oktoba 1917, Lenin aliandika kwamba katika mapinduzi ya kiso-

shalisti tabaka la wafanyakazi litayaunganisha mataifa "*siyo* kwa nguvu ya pesa, *siyo* kwa nguvu ya rungu, si kwa utumiaji mabavu, bali kwa mapatano *ya hiari* na ushikamano wa watu wafanyao kazi dhidi ya wanyonyaji. Kwa mabwanyenye utangazaji wa haki sawa kwa mataifa yote umekuwa ni uhadaifu mtupu. Kwetu sisi utakuwa ni ukweli ambao utarahisisha na kuharakisha uvutiwaji wa mataifa yote upande wetu".

Tangu siku za mwanzoni kabisa za utawala wa Kisovieti, Chama cha Mabolsheviki kilianza kutekeleza dai kuu la mpango wake kuhusu suala la mataifa, kikiyapa mataifa yote haki ya kujiamulia mambo yao wenyewe, pamoja na kujitenga na kuunda madola huru, na kudhaminia usawa wa kisiasa kwa mataifa yote.

Mkutano Mkuu wa Pili wa Masovieti, ambao ulitangaza kupinduliwa kwa Serikali ya Muda na ukabidhiwaji wa madaraka mikononi mwa Masovieti (mabaraza ya uwakilishi), ulitoa ilani ya kulipatia kila taifa haki ya kuamua maumbo ya mamlaka yake ya kiserikali kwa uhuru pasina kushurutishwa kwa nguvu. Katika mwito *Kwa Wafanyakazi, Maaskari na Wakulima*!, ulioandikwa na Lenin, mkutano mkuu huo ulitangaza kwamba utawala wa Kisovieti utayadhaminia mataifa yote yakaayo Urusi haki halisi ya kujiamulia mambo yao wenyewe. Dikrii za Amani na Ardhi zilizopitishwa na mkutano mkuu huo ziliwakilisha maongozi ya sera kuhusu mataifa yaliyotakiwa kufuatwa na utawala mpya wa tabaka la wafanyakazi, kwa kulingana na maslahi muhimu kabisa ya mataifa yote ya Urusi.

Dikrii ya Amani ilitungwa kutokana na uelewaji wa Mabolsheviki wa haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe kama ni ukomeshaji wa ubakuzi wo wote wa maeneo ya nchi za kigeni, ukomeshaji wa hatua yo yote ya kujiunganisha au kulizuia taifa hili au lile ndani ya mipaka ya madola yaliyoko ya mataifa mengi, pasina kujali lini taifa hilo liliunganishwa kwa nguvu na dola linalohusika. Katika dikrii hiyo ya kwanza, Serikali ya Kisovieti ilitangaza ubatilishwaji wa mikataba yote ya kibeberu na kuahidi kuibainisha hadharani pasina kukawia, jambo ambalo lilifanywa mnamo miezi ya mwanzo kabisa ya utawala wa Kisovieti.

Dikrii ya Ardhi iliwaweka wakulima wote, pasina kujali taifa lao, katika hali sawa, na kwa hivyo kueneza mawazo ya usawa wa mataifa miongoni mwa umma.

Hatua iliyochukuliwa na mkutano mkuu huo ya kuunda Wizara ya Mataifa ilionyesha kwamba Chama cha Mabolsheviki na utawala wa Kisovieti ziliuona utekelezaji wa sera yao kuhusu mataifa kuwa ni muhimu sana.

Mashauri makuu ya mpango wa Chama kuhusu suala la mataifa yaliingizwa katika Tangazo la Haki za Mataifa ya Urusi, waraka wa kikatiba wenye umuhimu wa kihistoria uliopitishwa tarehe 2 Novemba, 1917.* Tangazo hilo lilisema

---

* Kabla ya 14(1) Februari, 1918, tarehe zote zinatolewa kwa mujibu wa kalenda ya zamani iliyokuwa ikitumika nchini Urusi wakati ule, na kuanzia tarehe 14 Februari, 1918, kalenda hii ya kisasa ikawa ndiyo inayotumika.– *Mhariri.*

kwamba ukombozi kamili na usiobatilika kamwe wa mataifa yaliyotiwa utumwani na utawala wa mfalme wa Kirusi na mabwanyenye wa kibeberu ulikuwa ndiyo shabaha kuu ya utawala wa Kisovieti. Kwa kutofautiana na sera ya ukandamizi wa mataifa inayojulikana sana kwa uovu wake, ambayo ilikuwa ikiendeshwa na utawala wa mfalme na kuendelezwa na Serikali ya Muda ya mabwanyenye kwa kificho cha kijoga, Tangazo hilo lilitoa sera ya muungano wa hiari na wa uaminifu wa mataifa ya Urusi. Ni muungano kama huo tu ndio ulioweza kuwaunganisha wafanyakazi na wakulima katika jeshi moja la kimapinduzi lenye uwezo wa kujibiza minyemeleo yo yote ile ya mabwanyenye wa kibeberu na kulihami na kuliimarisha dola la tabaka la wafanyakazi. Tangazo hilo lilisema kwamba Baraza la Mawaziri wa Umma litaendelea na shughuli zake katika upande wa suala la uhusiano wa mataifa juu ya msingi ya usawa na uhuru wa mataifa ya Urusi, haki yao ya kujiamulia mambo yao wenyewe pasina vizuizi vyo vyote, pamoja na kujitenga na kuunda dola huru; uondoshwaji wa mapendeleo na mapingamizi yote ya kitaifa na ya kidini; na maendeleo huru ya mataifa madogo na makundi yote ya kikabila yanayoishi nchini Urusi.

Tarehe 22 Novemba, 1917, Baraza la Mawaziri wa Umma lilitoa mwito *Kwa Waislamu Wote Wafanyao Kazi wa Urusi na Mashariki*. Serikali ya Kisovieti iliyaita mataifa yaliyozorota mno ya Urusi iliyokuwa ikitawaliwa na mfalme kuutupilia mbali mkatale wao wa makarne mengi, kuyaunga mkono mapinduzi ya kisoshalisti na Ma-

sovieti ya Wajumbe wa Wafanyakazi, Maaskari na Wakulima. Mwito huo ulisema kwamba mikataba ya kisiri ya serikali ya mfalme juu ya kuzigawanya Uajemi na Uturuki ilikuwa imeshabatilishwa papo hapo na milele. Uliyahimiza mataifa ya Kiislamu kuamua mustakbali wao wa kitaifa pasina vikwazo vyo vyote.

Serikali ya Kisovieti ilitangaza uhuru kamili wa imani na mila, kutodhurika kwa taasisi za kitaifa na za kiutamaduni za Waislamu, na kulinda haki za mataifa ya Kiislamu kwa upande wa Masovieti ya Wajumbe wa Wafanyakazi, Maaskari na Wakulima.

Lenin aliipa umuhimu mkubwa sana kazi iendeshwayo miongoni mwa Waislamu. Tarehe 17 Januari, 1918, Wizara inayohusika na mambo ya Waislamu wa Urusi ya ndani iliundwa kwa pendekezo lake, na tarehe 17 Juni, alitia saini azimio la serikali lenye kuyataka Masovieti ya majimbo yenye wakazi wengi wa Kiislamu kutengeneza upesi wizara zinazohusika na mambo ya Waislamu. Lenin aliweka nadhari kubwa sana katika kutoa dikrii na nyaraka nyinginezo muhimu za kiserikali kwa lugha za mataifa ya Kiislamu.

Ilibidi pia kuushinda urithi mwingine mbaya wa zamani: tuhuma ya mataifa madogo ya Urusi kwa Warusi. Wakulima walikuwa ndio wingi mkubwa wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla, ilhali tabaka la wafanyakazi la kimapinduzi la Kirusi lilikuwa linatokana na taifa kandamizi. Hiyo ndiyo maana kwa nini muungano baina ya tabaka la wafanyakazi na wakulima usingeweza kuwa wa kudumu isipokuwa tuhuma

iliyopaliliwa na utawala wa mfalme miongoni mwa wananchi wafanyao kazi wa mataifa mbalimbali kwa wawakilishi wa taifa linalotawala ikomeshwe kabisa.

Kiini cha kitabaka cha suala la mataifa nchini Urusi kilikuwa kimo katika uwekaji wa uhusiano barabara baina ya tabaka la wafanyakazi la taifa lililokuwa likitawala hapo kabla na wakulima wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa. Lenin alisema kwamba papo tu tabaka la wafanyakazi likishatwaa madaraka mikononi mwake, basi itakuwa si maneno bali ni vitendo ndivyo vitakavyoondosha tuhuma kwa taifa kuu la Warusi ambayo ilipaliliwa na utawala wa mfalme na mabwanyenye wa Kirusi. Alidai pachukuliwe hadhari kubwa kuhusiana na hisia za kitaifa za watu wa mataifa yale yaliyokuwa yakikandamizwa ili kuondoa sababu za kuzuka tuhuma za zamani na kupata muungano mkubwa zaidi wa hiari wa jamhuri za Kisovieti za mataifa yote.

Katika kuelezea majukumu ya maendeleo ya taifa yanayowakabili Wakomunisti wa taifa la dola kuu la zamani, Lenin alitilia mkazo kwamba haitoshi kuyapa tu mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa zamani haki ya kujitenga. Jambo muhimu ni kwamba yapasa tabaka la wafanyakazi la Urusi litoe jitihada kubwa sana za kufanya mipango ya kuyasaidia mataifa hayo yaliyojikomboa karibuni.

Shida mojawapo katika kutekeleza maongozi yaliyotangazwa na Chama lilikuwa ni kwamba baadhi ya Wakomunisti hawakuelewa kiini cha mwito wa Mabolsheviki kuhusu suala la mataifa

na kwa hakika hasa hayo yaliwafaidia mabwanyenye wapendeleao kujibagua kitaifa. Baadhi yao walisema kwamba yapasa kuuachilia mbali mwito wa kujiamulia wenyewe kwa mataifa, kwani ungeweza kupelekea kuvunjika kwa mamlaka ya zamani ya Urusi katika mkururo wa vijidola vitegemeavyo wenyewe. Baadhi ya viongozi wa jamhuri za kitaifa walikuwa na maoni kama hayo vile vile.

Lenin aliiona misimamo hiyo kuwa ni ya makosa, kuwa ni yenye kulipunguzia umuhimu suala la mataifa katika kipindi hicho. Aliziunga mkono kwa dhati jitihada za mataifa yakaayo pembezoni mwa Urusi za kutaka muungano na Jamhuri ya Shirikisho ya Urusi na kuwania umoja wa kushikamana dhidi ya adui wa pamoja, lakini wakati huo huo aliwahimiza Wakomunisti kuichambua hali ya mambo ilivyo na hisia za umma, na kufanya uamuzi barabara. Baadhi ya Wakomunisti wa mitaani walishindwa kutia maanani hilo jambo kwamba mabwanyenye wa kitaifa, ambao kabla ya Mapinduzi ya Kisoshalisti ya Oktoba 1917 walikuwa wakipinga uhuru wa aina yo yote ile kwa mataifa yao, sasa wameugeuza mwito huo kuwa ni chombo cha kuuchochelea umma na baadhi ya wakati walikitumia hata kwa kufaulu ili kuyatenganisha na Urusi ya Kisovieti.

Katika hali hizi, mabwanyenye wapendeleao kujibagua kitaifa wangeweza kutenganishwa na wananchi wafanyao kazi kwa kudhaminia usawa tu wa mataifa yote katika kila upande, pamoja na ule wa kujenga nchi.

Papo tu baada ya Mapinduzi ya Oktoba, Le-

nin binafsi alihakikisha utekelezwaji wa haki ya mataifa kujiamulia mambo yao wenyewe.

Tarehe 3 Desemba, 1917, Baraza la Mawaziri wa Umma la Jamhuri ya Shirikisho ya Urusi liliitambua haki ya Ukraina kujiamulia mambo yake yenyewe, pamoja na kujitenga mbali; uhuru wa kiserikali wa Estonia, Latvia na Lithuania ulitambuliwa tarehe 23 Desemba; na Armenia tarehe 29 Desemba.

Lenin aliandika kwamba "kila Urusi ikiwa huru zaidi, na kila jamhuri yetu ikitambua zaidi haki za mataifa yasiyo ya Kirusi kujitenga, ndivyo mataifa mengine *yatakavyovutika* kwa nguvu zaidi kujiunga nasi, ndivyo ugomvi utakavyokuwa haba zaidi, ndivyo huko kujitenga kwenyewe hasa kutakavyokuwa nadra zaidi, ndivyo muda wa kujitenga utakavyokuwa mfupi zaidi, na ndivyo muungano wa kidugu baina ya jamhuri ya wafanyakazi na wakulima ya Urusi na Jamhuri za mataifa yote mengine utakavyokuwa mkubwa na wa kudumu zaidi". Utabiri huo ulithibitishwa kikamilifu na maisha yenyewe. Hatua halisi zilizochukuliwa na Serikali ya Kisovieti za kutoa uhuru wa kiserikali kuyapa mataifa yaliyokuwa ndani ya mamlaka ya Urusi ya zamani ziliuyakinishia umma wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa kwamba sera ya utawala wa Kisovieti kuhusu mataifa ilikuwa ni ya unyoofu na thabiti, kwamba mabwanyenye "wao wenyewe" walikuwa wakichukiwa pamoja na serikali zao, na kwamba uhuru wa kitaifa hauwezi kutetewa pasina kuungana na tabaka la wafanyakazi la Kirusi, pasina utawala wa Masovieti.

Kwenye Mkutano Mkuu wa Tatu wa Urusi Nzima wa Masovieti mnamo Januari 1918, Lenin alisema juu ya umuhimu mkuu wa sera ya kimatendo iliyofuatwa na utawala wa Kisovieti, ambao uliwapa mataifa yote fursa kamili ya kujiamulia mambo yao wenyewe. Mkutano Mkuu huo ulihimiza kuendesha mapambano ya kuwania haki halisi ya kujiamulia wenyewe kwa kutegemea utawala wa Kisovieti, ukidhaminia tabia ya hiari ya muungano wa mataifa katika *Tangazo la Haki za Watu Wafanyao Kazi na Wanyonywao.*

Lenin alifahamisha kwamba wakati ule ilikuwa ni jambo la hatari na la madhara kabisa kuupambanisha mwito wa uhuru wa kitaifa na mawazo ya uongozi mmoja mkuu; aliwataka ndugu wa mitaani waichungue hali ya mambo kwa makini zaidi na kufanya uamuzi sahihi. Alikutana na kuongea na wengi wao na kuwafanya kuelewa jambo hilo barabara.

Wakomunisti wa Turkestan, Estonia, Latvia, Azerbaijan na Tataria hawakutoa papo hapo mwito wa kuunda jamhuri za kitaifa zenye mamlaka yao zenyewe. Msimamo wa Mabolsheviki wa Turkestan wa kukataa kuwasilisha suala la hima la kudai mamlaka ya kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kwenye Mkutano Mkuu wa Tatu wa Masovieti ya Turkestan katika Novemba 1917 ulitumiwa na wafuasi wa mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa ili kuunda serikali ipingayo mapinduzi. Baadaye Mabolsheviki walisahihisha kosa lao na kwenye Mkutano Mkuu wa Tano wa Masovieti ya Turkestan

katika Aprili 1918 walitangaza mamlaka yao ya kujitawala kwa mambo ya ndani, na Lenin akapeleka simu mahsusi ya kupongeza hatua hiyo iliyochukuliwa.

Wakitoa madai yao ya kimaongozi kuhusu suala la mataifa, Mabolsheviki walisema kwamba haki ya kujitenga isikorogwe na jambo la kufalia kwa huko kujitenga, na kwamba tatizo hili yapasa litanzuliwe kwa kutegemea hali halisi za kihistoria, ili kutosheleza maslahi ya mapambano ya kuwania usoshalisti. "Twadai uhuru wa kujiamulia wenyewe, *yaani*, kujitegemea wenyewe, *yaani*, uhuru wa kujitenga kwa mataifa yanayokandamizwa, siyo kwa sababu tulitamani kuigawanya nchi kiuchumi, au tukifuata wazo la kupendelea vijidola vidogo vidogo, bali, kinyume chake, kwa sababu twataka madola makubwa zaidi na umoja mkubwa zaidi na hata mchanganyiko wa mataifa, lakini juu ya msingi wa kidemokrasi kikweli tu, msingi wa umoja wa kimataifa kikweli, ambao *haufikiriki* pasina kuwa na uhuru wa kujitenga."

Kwa sababu ya sera ya umoja wa kimataifa iliyoendeshwa na Chama cha Kikomunisti, haki ya kila taifa kujenga maisha yake kama lipendavyo, na msaada uliotolewa na tabaka la wafanyakazi la Kirusi kwa wananchi wafanyao kazi wa mataifa yote katika kupambana na mabwanyenye wa kitaifa wapingao mapinduzi kwa ajili ya kuwania uhuru wa kweli, mataifa yote ya mamlaka ya zamani ya Urusi yaliutambua utawala wa Kisovieti mnamo miezi michache ya mwanzo baada ya Mapinduzi ya Oktoba.

Jukumu la kimatendo la Chama sasa lilikuwa

ni kutafuta njia bora zaidi za kuyaunganisha mataifa, kutafuta maumbo ya utaratibu wa kiserikali ambayo yangeweza kupatanisha vizuri zaidi maslahi ya kila taifa na yale ya dola zima, na urafiki mkubwa zaidi miongoni mwa mataifa yote ya nchini. Ilikuwa ni suala la kuunda maumbo ya kiserikali ya aina mpya kabisa. Utafiti huu ulipelekea pasina kuepukika kuzuka maoni mbalimbali kuhusu namna za kujitawala wenyewe, uhusiano baina ya jamhuri, tabia ya kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani, shirikisho, n. k. Fanikio kuu la kihistoria la Lenin lilikuwa ni hilo kwamba baada ya kwisha kujumlisha maarifa ya kimatendo ya mwanzoni ya dola la Kisovieti, aliamua tabia na aina za uhusiano baina ya jamhuri zenye kujitawala zenyewe katika dola moja la muungano.

Mkabala Halisi wa Kihistoria

Uhalisi wa kihistoria kwa ukomo wake ndilo dai kuu la mafunzo ya Marx na Lenin kuhusu suala la mataifa. Tabia mahsusi zote za kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamaduni, kisaikolojia, za maisha ya kila siku na nyinginezo lazima zizingatiwe. Kila taifa au kabila likiwa halikuendelea zaidi katika pande zote hizi, ndivyo haja ya kuwa na mkabala wa hadhari, wa kuridhia, wa uangalifu na uvumilivu inavyokuwa kubwa zaidi kwa kazi ya utaratibu maalumu ambayo ingezingatia, kama Lenin alivyoelezea, njia zote "za upugoupugo" na "za kupindapinda".

Mabolsheviki walizingatia tabia mahsusi za kila taifa na kuamua majukumu makuu kuhusiana na kila taifa moja maalumu. Haya yanaweza kuonekana kwa urahisi kutokana na maelezo ya Lenin juu ya tabia mahsusi za sera ya Chama kuhusu mataifa madogo katika sehemu za Mashariki za nchi ya Kisovieti, ambako tabaka la wafanyakazi lilikuwa dogo sana na uhusiano wa kimwinyi wa zama za kale ulikuwa ungali umehifadhika.

Kama matokeo ya sera ya kikoloni ya kikatili sana iliyoendeshwa na utawala wa mfalme katika Asia ya Kati, ilikuwa vigumu zaidi kwa mataifa ya Mashariki kuondosha tuhuma yao kwa Warusi. Mabwanyenye wa kienyeji waliokuwa wakipendelea kujibagua kitaifa, mashehe na wasomi wa kibwanyenye waliendelea kuwa na athari kubwa miongoni mwa wakazi wa huko. Kwa kuzingatia yote haya, iliwabidi viongozi wa serikali kuu kufuata siasa ya hadhari hasa kuhusu wakazi wa Kiislamu. Kila hatua ilibidi ifikiriwe kwa uangalifu, kwani kila kosa lililofanyika lilikuzwa mno na maadui wa utawala wa Kisovieti. Isitoshe, *mabasmachi* (wapinga mapinduzi huko Mashariki), ambao walibeba silaha mkononi kuupiga vita utawala wa Kisovieti, walikuwa mara nyingi wakiongozwa na wawakilishi wa mabwanyenye na wasomi wa kitaifa, ambao walikuwemo katika safu za mbele za harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa kabla ya Mapinduzi ya Oktoba. Hali ya mambo katika Asia ya Kati ilitatanishwa zaidi kwa makosa yaliyofanywa na viongozi wa kienyeji wa idara za Chama na Masovieti. Mathalan,

mwanzoni walichukua wawakilishi wachache sana wa wakazi wa kienyeji katika vyombo vya serikali za mitaa, na vyeo vya madaraka vilikuwa kwa wingi zaidi vikishikiliwa na Warusi wakaao huko. Uhusiano baina ya wawakilishi wa utawala wa Kisovieti (aghalabu Warusi) na wakazi wa Kiislamu ukawa ahasi.

Kamati Kuu ya CKU(Mab.)* na Lenin binafsi walichukua hatua za kusahihisha makosa yaliyofanywa huko Turkestan. Lenin aliwashauri ndugu wa Turkestan, kwa kutia maanani tabia mahsusi za kitaifa kurekebisha vifungu vile vya dikrii zilizotolewa na Baraza la Mawaziri wa Umma ambavyo havikuzingatia vilivyo hali za maisha ya kila siku katika Turkestan. Wakati wa Mkutano Mkuu wa Nane wa CKU(Mab.), Lenin alilipokea mara mbili kundi la wajumbe wa Turkestan, akionyesha hamu kubwa ya kutaka kujua mambo yao yote, hasa ukuaji wa fahamu ya kisiasa na shughuli za kisiasa miongoni mwa umma, uhusiano baina ya mataifa na hali ya chakula.

Mkutano wa Pili wa Chama wa Turkestan katika Machi 1919 uliunda idara mahsusi inayohusika na mambo ya Waislamu, ambayo iliendesha shughuli zake hadi Januari 1920 na kufanya mengi katika kuwaelimisha wakazi wa Kiislamu na kuwaingiza katika idara za utawala wa Kisovieti.

Ili kukomesha matokeo ya makosa yaliyofany-

---

* *CKU (Mab.)* – Chama cha Kikomunisti cha Urusi (cha Mabolsheviki), jina la Chama cha Kikomunisti cha Urusi ya Kisovieti toka 1918.– *Mhariri.*

wa mnamo siku za mwanzoni baada ya mapinduzi, tume mahsusi ilipelekwa huko Turkestan. Ilichukua barua ya Lenin kuwapelekea Wakomunisti wa Turkestan, ambayo ndani yake aliwaita "kufanya kila jitihada ili kutoa mfano barabara wa uhusiano wa kidugu na mataifa ya Turkestan, kuyaonyesha kwa vitendo vyenu kwamba sisi ni wakweli katika azma yetu ya kufuta kabisa alama zote za ubeberu wa Kirusi na kuendesha mapambano makali kabisa dhidi ya ubeberu wa dunia". Lenin alivutia nadhari yao juu ya umuhimu wa kimataifa wa tanzuo sahihi la tatizo la uhusiano wa mataifa huko Mashariki: "Yawezekana kusema bila ya kutia chumvi kwamba uwekwaji wa uhusiano barabara na mataifa ya Turkestan ni wenye umuhimu mkubwa sana wa kihistoria kwa Jamhuri ya Shirikisho ya Urusi.

"Uwekwaji wa mahusiano barabara ya Jamhuri ya Kisovieti ya Wafanyakazi na Wakulima na mataifa dhaifu na yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla ni yenye umuhimu sana wa kimatendo kwa Asia nzima na kwa makoloni yote ulimwenguni, kwa maelfu na mamilioni ya watu."

Lenin alikumbusha daima haja ya kuzingatia tabia mahsusi za kazi iendeshwayo miongoni mwa Waislamu kama ndiyo sehemu iliyozorota zaidi ya wakazi wa Turkestan. Katika maelezo yake kwenye Mkutano Mkuu wa Pili wa Urusi Nzima wa Jumuiya za Kikomunisti za Mataifa ya Mashariki (Novemba 1919), Lenin alitilia mkazo kwamba ni lazima kuzingatia matatizo halisi ya kila taifa kwa mujibu wa kiwango chake

cha maendeleo, tabia zake za kipekee, na kadhalika; kutafuta njia za kuweka mawasiliano na masikini, na wananchi wafanyao kazi wa kila taifa dhidi ya warasimu wake, makabaila na mabwanyenye wake.

Alisisitiza kwamba iliwapasa Wakomunisti wa Kirusi wafanyao kazi huko Mashariki watoe mfano wa mwenendo wa kuigizwa, na kuwa na maoni ya kirafiki ya dhati kuhusiana na wenyeji wa huko.

Lenin alidai kwamba Wakomunisti wote walioambukizwa na kiburi cha taifa kuu warejeshwe kutoka Turkestan.

Katika Februari 1920, Kamati Kuu ya CKU (Mab.), kwa kushirikiwa na Lenin, ilipeleka barua ya kusambazwa "Kuhusu Kazi Miongoni mwa Mataifa ya Mashariki", yenye kusema juu ya haja ya kuzingatia mambo mawili: la uhusiano wa mataifa na lile la dini. Lilitilia mkazo kwamba Wakomunisti hawakuwa na budi kushirikiana maoni na wananchi wafanyao kazi wanaowania kujiamulia wenyewe kitaifa, lakini wakati huo huo wawafahamishe kwamba pale utawala wa wafanyakazi na wakulima nchini Urusi yote unapokabiliwa na hatari ya ubeberu wa nchi za Magharibi, halikadhalika na ile ya sera ipingayo mapinduzi ya mabwanyenye wa Kiislamu na mamullah, njia ya wananchi wafanyao kazi wa Kiislamu ya kuweza kujiokoa nafsi zao ni kufanya muungano mkubwa kabisa kadiri iyumkinikavyo na Urusi ya Kisovieti.

Majukumu ya kiuchumi, kisiasa na kitaifa ya Wakomunisti wa Turkestan yalifafanuliwa katika

azimio la Kamati Kuu "Kuhusu Majukumu Makuu ya CKU(Mab.) katika Turkestan" (Juni 1920). Azimio hilo liliambata matatizo mengi yanayohusiana na maisha katika eneo hilo na kuonyesha njia za kuyatanzua kimatendo. Lilielezea maoni kuhusu mataifa mbalimbali ya Kiislamu, kuhusu warasimu wa zamani wa Kirusi na makulak (wakulima matajiri), uhusiano wa umilikaji na utumiaji wa ardhi, muundo wa utawala katika eneo hilo, na mengineyo.

Lenin alipendekeza kwamba azimio hilo litoe maelekezo ya kimatendo ya kuwashirikisha Wakomunisti na wananchi wafanyao kazi wa Turkestan katika shughuli za utawala wa eneo hilo. Lenin aliona pia kuwa ni lazima kuainisha tabia ya uhusiano baina ya Tume ya Turkestan ya Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima na wakuu wa mitaani ili kukuza zaidi mawasiliano baina yao, kuimarisha jukumu la Baraza la Mawaziri wa Umma na Kamati Kuu ya Utendaji ya Turkestan, na kuonyesha njia za kuwashirikisha wakulima wafanyao kazi katika wendeshaji wa serikali za mitaa, na pia mbinu za kuendesha mapambano dhidi ya masalio ya kidini, Umoja wa Waislamu na harakati za mabwanyenye za kupendelea kujibagua kitaifa. Jukumu lao sasa lilikuwa ni kuchukua hatua za taratibu na zilizofikiriwa barabara za kutayarisha ukabidhiwaji wa madaraka mikononi mwa Masovieti ya mitaani ya Wajumbe wa Wananchi Wafanyao Kazi chini ya udhibiti wa Wakomunisti wa kuaminika.

Wakati ule, wanachama wa jumuiya za kikomunisti katika sehemu za pembezoni mwa nchini

walikuwa kwa vikubwa sana ni Warusi, na wachache tu ndio waliotoka miongoni mwa wenyeji wa huko, jambo ambalo lilifanya iwe vigumu kuingiza athari yao miongoni mwa umma. Kwa hivyo basi, wakati ule jukumu kuu la Chama lilikuwa ni kuandikisha wanachama wa jumuiya za Chama za huko kutoka miongoni mwa wakazi wa kienyeji. Azimio la Kamati Kuu ya CKU (Mab.) "Kuhusu Majukumu Makuu ya CKU (Mab.) katika Turkestan" liliziwajibisha jumuiya za Chama kupambana siyo tu na mitokezo ya maoni ya kujitukuza kwa taifa kuu, bali pia makosa mabaya ya kujibagua kitaifa. Katika kukifichua kiini cha kibwanyenye cha makosa ya kujibagua kitaifa, Lenin alitilia mkazo hasa kwamba yapasa kuwaelimisha makada wa Kiislamu na kuwashirikisha katika shughuli za pande zote. Lenin aliwafunza makada vipi na wapi pa kuzingatia tabia mahsusi za kila eneo la kitaifa.

Katika maelezo yake kuhusu Ripoti iliyotolewa na A. Sultan-Zade kwenye Mkutano Mkuu wa Pili wa Jumuiya ya Kikomunisti ya Kimataifa kuhusu matazamio ya mapinduzi ya kijamii huko Mashariki katika Julai 1920, Lenin aliandika: "...yapasa *kuzirekebisha* idara za Kisovieti halikadhalika na Chama cha Kikomunisti (uanachama wake, majukumu yake mahsusi) kulingana na kiwango cha nchi *za kikulima* za Mashariki zilizoko chini ya utawala wa kikoloni.

"Hiki ndicho kiini cha jambo hilo. Lahitaji kufikiriwa na *kutafuta* jawabu *halisi*". Kwa ajili ya majukumu ya ukiukaji kwendea katika usoshalisti yatekelezwe kwa kufana, ni lazima kuelewa

"njia, mbinu na zana gani *za katikati* zinazohitajika kwa ajili ya ukiukaji kutoka uhusiano wa *kutangulia ubepari* kuingia katika usoshalisti. Hilo ndilo jambo lenyewe lote linalohusika." Hivyo ndivyo Lenin alivyofundisha.

Katika Novemba 1920, ripoti kutoka Turkestan zilimwarifu Lenin juu ya utungaji wa mswada wa sheria kuhusu ardhi ambayo madhumuni yake yalikuwa ni kudhoofisha mastakimu ya mabai (makabaila wa huko) na makulak pasina kuyaathiri maslahi ya wakulima wenye vijishamba vidogo (*dekhkan*), kadhalika juu ya ujenzi wa miradi ya mifereji ya kumwagilia maji kwa mapeo makuu, ambao ulikuwa ni muhimu sana kwa kilimo cha huko, pia juu ya sera ya chakula yenye kurekebishika upesi, na badiliko (ili kusahihisha makosa ya zamani) katika mbinu za kuwaandikisha Waislamu kwa huduma za kazi.

Lenin alitunga Azimio lililotolewa na Halmashauri ya Kisiasa ya Kamati Kuu ya CKU (Mab.) kuhusu Majukumu ya CKU(Mab.) katika mitaa yenye kukaliwa na mataifa ya Mashariki (Oktoba 1920), ambalo lilidai pafanywe uchunguzi mkali wa madhara yote yaliyofanywa na baadhi ya watu kutoka miongoni mwa wakazi wa Kirusi kuhusiana na watu wa mataifa madogo ya Mashariki, na kuwaadhibu wale wanaopatikana na hatia ya kufanya madhara hiyo; lilitaka pia patolewe ilani kwa niaba ya vyombo vikuu vya utawala wa Kisovieti ili kuthibitisha maongozi makuu ya sera ya Jamhuri ya Shirikisho ya Urusi kuhusu mataifa, pamoja na kudhibiti barabara utekelezwaji wake kikamilifu; lilidai haki ya kuji-

tawala kwa mambo ya ndani – kwa maumbo yenye kufalia vizuri zaidi hali za kienyeji – kwa mataifa yale ya Mashariki ambayo hayana bado taasisi zao wenyewe za kujitawala kwa mambo ya ndani, n. k.

Lenin aliunga mkono kwa juhudi mapendekezo ya ndugu fulani yaliyokusudiwa kueneza aina zile za kazi miongoni mwa mataifa yaliyoko pembezoni mwa nchini ambazo zingesaidia kuwafahamisha wale waliozorota mno miongoni mwa wakazi wa huko maana ya utawala wa Kisovieti. Mathalan, aliikubali fikira ya kutengeneza misafara, meli na magarimoshi ya kueneza siasa, na kusaidia utekelezwaji wa fikira hiyo. Kwa mfano, aliarifiwa kwamba msafara wa matishali yenye makundi ya waenezaji siasa, duka na chombo cha kuonyeshea sinema uliondoka kwa kupitia katika Mto Amudarya na mito ya Jamhuri ya Khorezm. Maduka ya kuhamahama pamoja na vyombo vya kuonyeshea sinema yalitumiwa na waenezaji siasa ambao walikuwa wakizuru vijiji (*kishlak*) vya huko.

Katika kujadili suala la "garimoshi la Mashariki", Halmashauri Kuu ya Jumuiya za Kikomunisti za Mataifa ya Mashariki iliamua kwamba kabla garimoshi halijaondoka, yapasa watumishi wake wafahamishwe vilivyo mpango wa utekelezaji wa sera ya Mabolsheviki ya uhusiano wa mataifa huko Turkestan. Komisaa wa kisiasa aliyeteuliwa kwa safari hiyo alikuwa ni mtumishi wa Chama mwenye jadi ya Kiislamu, ambaye si kama alikuwa akijua vilivyo sera ya Chama cha Kikomunisti tu, bali pia alielewa vyema hali mahsu-

si za huko Mashariki. Watumishi hao walikuwa ni waenezaji siasa na wafundishaji wa mambo ya Chama (watu watatu kutoka idara ya kisiasa ya mpakani na wawili walihitimu shule ya Chama mjini Moscow), na pia wahadhiri (mwandishi, profesa, mjumbe wa Wizara ya Elimu ya Umma, na wengineo). Watumishi hao walipanga kuchapisha gazeti kwa mojawapo ya lugha za Mashariki (katika 1920, kulikuwa tayari kukitolewa magazeti 60 kwa lugha za mataifa madogo mbalimbali).

Misafara ya kueneza siasa, magarimoshi na meli ziliondoka kuelekea sehemu mbalimbali, zikibaki kila mahali kwa muda wa miezi miwili au mitatu. Wakazi wa kienyeji waliwaona waenezaji siasa hawa kama ni ishara ya huko kushughulikiwa kwao sana na wajumbe wa serikali kuu na kwa hivyo walihudhuria kwa hamu sana mikutano yote iliyokuwa ikifanywa na waenezaji siasa hao.

Katika Januari 1920, Lenin nafsi yake alitunga orodha ya maelekezo kwa magarimoshi na meli za waenezaji siasa na wafundishaji wa mambo ya Chama. Alishauri kuzidisha shughuli zao katika mambo ya kiuchumi na ya kimatendo, kuwaingiza wataalamu wa kilimo na mambo ya ufundi katika makundi hayo, kuchagua vizuri zaidi orodha ya majarida na vitabu vya mambo ya ufundi vinavyohitajika, na kupatana halani na makampuni ya kigeni kwa utengenezaji wa filamu za sinema kuhusu kilimo, viwanda na sayansi.

Mkabala halisi wenye kulingana na hali ya kihistoria ulitokezwa wazi hasa katika uundaji wa

sehemu zenye kujitawala kwa mambo ya ndani na shirikisho katika daraja mbalimbali za ujenzi wa taifa na dola.

Wakijitahidi kukomesha mabaki ya uhusiano wa zama za kale na ya umwinyi katika Jamhuri za Mashariki, kuwasaidia wale waliokuwa wakiendesha maisha ya kuhamahama kufanya maskani, na kuwasahilishia wakulima masikini na vibarua wa kilimo kupiga hatua zao za mwanzo kuelekea katika ushirika, Mabolsheviki na Lenin binafsi waliwaonya watumishi wa Chama na Masovieti wasifanye pupa mno katika kuyang'oa mabaki ya miundo ya kiuchumi iliyokwisha zake, kwani pupa kama hiyo ingeweza kuushushia hadhi utawala wa Kisovieti na kuwapa wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa kisingizio cha kufanya kampeni ya kupinga utawala wa Kisovieti. Kwa hivyo basi, taasisi fulani za mila zilizokwisha zake zilibidi zihifadhiwe kwa muda hivi, na nyingine hata kurejeshwa tena. Wakati wa kuundwa kwa chombo kipya cha utawala huko Khorezm baada ya mapinduzi ya umma, ilibidi pachukuliwe hatua za kuratibisha kazi ya wanadi (*djarghi*). Zamani, wakati palipokuwa hakuna magazeti wala huduma za posta katika sehemu hizi na wakazi wa huko walikuwa hawajui kusoma na kuandika, maamuzi ya wakuu wa serikali yalikuwa yakitangazwa na wanadi. Katika Aprili 1920 kuliundwa idara kuu ya wanadi, ambayo iliwabadilisha wanadi wote wasiojua kusoma wala kuandika huko mijini na vijijini kwa wale wanaojua kusoma na kuandika. Katika 1921 na 1922, mahakama za makadhi ambazo ziliondosh-

wa kwa sababu ya kuundwa kwa mahakama za umma, zilirejeshwa tena katika sehemu fulani za Asia ya Kati. Mahakama hizi ziliharijiwa na wakazi wenyewe.

Katika baadhi ya sehemu za Mashariki, utawala wa Kisovieti uliwekwa kwa umbo la Masovieti ya Wakulima, wala siyo ya Wafanyakazi na Wakulima. Katika sehemu zile ambako mataifa madogo yalikuwa yangali bado yako kwenye daraja ya maendeleo ya makabila, Masovieti yaliwekwa siyo kwa kutegemea msingi wa kawaida wa majimbo, bali kwa mujibu wa makabila pasina kuangalia mahali pa ukazi pa daima, na kukawekwa Masovieti ya vijijini na ya mitaani ya wajumbe wa kabila moja.

Misingi ya Mgawanyo Mpya wa Maeneo ya Utawala

Katika kufafanua misingi mikuu ambayo ilikuwa iliongoze tabaka la wafanyakazi lililoshinda katika ujenzi wa taifa na dola na katika masuala yanayohusu mgawanyo kwa mujibu wa maeneo, Lenin alisema kwamba mpangiko wa mataifa wa wananchi ulikuwa ni mojawapo la mambo muhimu kabisa.

Katika kitabu chake *Po na Rhine*, Engels aliandika kwamba katika maendeleo ya historia, ambayo yalikomesha kuwepo kwa idadi kadhaa ya mataifa madogo na yasiyo na uhai wo wote, mipaka ya mataifa makubwa na yenye uhai ya Ulaya ilikuwa ikizidi kuamuliwa kwa mujibu wa

"lugha na ushirikiano wa maoni" miongoni mwa wananchi. Engels aliita mipaka hii kama ni "ya kimaumbile". Katika kulichambua wazo hilo, Lenin alifahamisha kwamba lilikusudia dahari ya ubepari wa kabla ya uhodhi, kwamba ubepari kwenye daraja yake ya ubeberu ulielekea zaidi kuivunja mipaka hii iliyofafanuliwa kwa njia ya kidemokrasi, ukiuachia usoshalisti unaokuja kuulikiza urithi wa mipaka ambayo si ya kidemokrasi kamwe, idadi kadhaa ya nchi zilizobakuliwa katika Ulaya na sehemu nyinginezo za dunia.

Kwa upande wake, Lenin alibashiri, usoshalisti ulioshinda katika kurejesha tena na kutekeleza demokrasi kamili katika pande zote, utatambua ufafanuaji wa kidemokrasi tu wa mipaka kwa mujibu wa matakwa na "ushirikiano maoni" wa wananchi. Alitilia mkazo kwamba uundwaji wa sehemu za nchi zenye kujitawala zenyewe kwa mambo ya ndani zikiwa na mpangiko wa mataifa wa utangamano, ulikuwa ni muhimu sana kwa kukomesha mkandamizo wote wa kitaifa.

Lakini ili kuanzisha muundo wa utawala wa kidemokrasi katika dola lenye mataifa mengi, haitoshi kuzingatia mpangiko wa mataifa tu wa wananchi.

Katika makala yake, *Maelezo ya Ukosoaji Kuhusu Suala la Mataifa*, Lenin alitilia mkazo kwamba mpangiko wa mataifa wa wananchi "ni *mojawapo* la mambo muhimu sana ya kiuchumi, lakini *silo la pekee wala* muhimu kabisa. Kwa mfano, miji inatenda kazi *muhimu sana* ya kiuchumi chini ya ubepari, na kila mahali nchini Poland, Lithuania, Ukraina, Urusi, na kwingineko miji inapem-

bulika kwa kuwa na wakazi wa mchanganyiko wa mataifa mbalimbali. Kuitenganisha miji na vijiji na maeneo yanayovutikia kwayo kiuchumi, kwa ajili ya sababu 'ya utaifa', kungekuwa ni upuuzi na hakuyumkiniki. Hiyo ndiyo maana kwa nini haiwapasi wafuasi wa Marx kuutegemeza msimamo wao kwa ujumla na pekee juu ya msingi wa 'mgawanyiko wa maeneo ya nchi kwa mujibu wa mataifa'."

Wakati Chama cha Mabolsheviki kilipoanza kujishughulisha na kazi ya kujenga dola baada ya ushindi wa mapinduzi ya kisoshalisti, kilitekeleza mgawanyo mpya wa maeneo kwa kuzingatia mambo haya mawili: hali za kiuchumi halikadhalika muundiko wa kitaifa wa wakazi wa maeneo yanayohusika.

Mathalan, katika kutunga azimio la Baraza la Mawaziri wa Umma la Jamhuri ya Shirikisho ya Urusi juu ya uundwaji wa Majimbo Yajitawalayo Yenyewe kwa Mambo ya Ndani ya Kalmyk, Mari na Votyak, Lenin aliyapiga mchoro maneno hayo "katika sehemu ambako mataifa hayo yako kwa wingi" kutoka katika sentensi "majimbo yenye kujitawala yenyewe kwa mambo ya ndani ya wananchi wafanyao kazi wa Kalmyk, Mari na Votyak – katika sehemu ambako mataifa hayo yako kwa wingi", na kutoka katika kifungu cha pili cha mswada huo, kisemacho "uwekwaji wa hatimaye wa mipaka", aliyafuta maneno hayo "wa hatimaye".

Kwa njia hii, Lenin alitaka kuonyesha kuwa haipasi kutegemeza hoja zake mtu juu ya huko kutamalaki kwa wingi kwa taifa moja tu, bali ya-

faa kuzingatia mkururo mzima wa mambo kadha wa kadha. Moja kati ya mambo haya laweza kutiliwa mkazo ikitegemea juu ya hali halisi zilizoko.

Katika kadhia moja moja, fungamano za kiuchumi yapasa zipewe umbele katika kuamua mipaka ya maeneo fulani. Mathalan, Jimbo Lijitawalalo Lenyewe la Ossetia ya Kusini liliundwa kwa kutengana mbali na Jimbo la Ossetia ya Kaskazini kwa sababu majimbo haya yalikuwa yametengana mbalimbali kwa kiasi hivi, ambapo hilo la kwanza lilikuwa na fungamano kubwa zaidi za kiuchumi na Georgia. Kwa hivyo basi, upinzani wa Mamensheviki wa Georgia kwa uingizwaji wa mji wa Tskhinvali (mji mkuu wa Jimbo hilo) katika Ossetia ya Kusini kwa dai hilo kwamba taifa la Waossetia halikuwa ndilo lenye kutamalaki kwa wingi katika mji huo, ulikuwa ni wa upuuzi kabisa. Ilibidi kuzingatia vilivyo fungamano za kiuchumi za mji huo na wakazi wa jirani. Miji ya Kazan na Ufa, ambayo wakazi wake wakati ule walikuwa kwa wingi zaidi ni Warusi, iliingizwa katika Jamhuri Zijitawalazo Zenyewe za Tataria na Bashkiria kwa kutegemea sababu hizo hizo.

Katika kadhia nyingine, kulikuwa na hali za mambo ambazo zilipelekea kupewa umbele kwa mazingatio ya kitaifa. Mathalan, kulipokuwa kuamuliwa suala la kuyapa mataifa madogo ya Bashkir na Tatar uhuru wa kujitawala wenyewe kwa mambo yao ya ndani, Kamati ya Utendaji ya Jimbo la Ural ilipinga kutolewa kwa uhuru kama huo, ikitoa hoja kwamba mgawanyo wa

maeneo kwa mujibu wa mataifa ungeleta "uharibifu" na hata "uangamiaji" wa uchumi wote, pamoja na tabaka la wafanyakazi lenyewe. Hakuna shaka yo yote kwamba msimamo huo ulionyesha mwelekeo wa kiburi cha taifa kuu.

Chama kiliongozwa na misingi mikuu ya mgawanyo wa maeneo iliyofafanuliwa na Lenin na kutegemezewa hoja za haja ya kupatanisha fungamano za kiuchumi na mpangiko wa kitaifa wa wananchi.

Utaratibu wa Kujiendesha Wenyewe kwa Mambo ya Ndani Juu ya Msingi wa Utawala wa Wafanyakazi na Wakulima

Lenin aliuona utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kama mpango wa kuunda dola la kidemokrasi, kama mwongozo mkuu, wa pande zote wa dola la kidemokrasi lenye mataifa mengi mbalimbali, na aina chungu nzima mbalimbali za hali za kijiografia, na nyinginezo. Dai la kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kwa mujibu wa maeneo ya kitaifa lilikuwa ni sehemu ya mpango mkuu wa kidemokrasi wa Mabolsheviki. Kwa mujibu wa maoni ya Lenin, mpango huo ulitoa fursa ya kujiendesha wenyewe, kwa upeo mpana kabisa kadiri iyumkinikavyo, katika maeneo ya dola yenye aina mahsusi ya maisha ya kila siku na mpangiko wao wenyewe wa makabila.

Bila ya shaka, kujitawala wenyewe kitaifa kwa

mambo ya ndani katika dola la kibwanyenye hakudhaminii bado usawa kamili kwa mataifa. Lenin aliandika kwamba taifa "lenye kujitawala lenyewe kwa mambo ya ndani" huwa halina haki sawa na zile za taifa "linalotawala". Dai la kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani ni sehemu mojawapo ya mageuzi ya kidemokrasi na, kwa maana hiyo, ni chombo cha kuendeshea mapambano ya kimapinduzi ya kuwania usawa kamili zaidi, dhidi ya sera ya utumiaji mabavu iendeshwayo na taifa linalotawala.

Baada ya Mapinduzi ya Kisoshalisti ya Oktoba 1917, mabwanyenye wa kitaifa waliendesha mapambano ya kutapia roho dhidi ya utawala wa Kisovieti kwa msaada wa makundi na vyama vya kibwanyenye na vya kibwanyenye uchwara vishikiliavyo msimamo wa kujibagua kitaifa, wakilitafsiri dai la haki ya kujiamulia wenyewe kwa mataifa na kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kama ni lenye kukusudia haki ya kuunda dola "huru" la kibwanyenye.

Papo tu baada ya ushindi wa Mapinduzi ya Oktoba 1917 ubeberu wa kimataifa uliziunga mkono serikali za kibwanyenye za kitaifa kwa madhumuni ya kuweka utawala wake katika sehemu zikaliwazo na mataifa madogo madogo zilizoko pembezoni mwa Urusi. Mipango hii ya mabwanyenye wa kimataifa ilikwenda kapa.

Lakini wakati huo huo katika baadhi ya sehemu zikaliwazo na mataifa madogo madogo, kipindi cha kwanza cha utawala wa Kisovieti hakikumalizikia kwa ushindi wa utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi kwa sababu fulani

mahsusi kadha wa kadha. Kwa mfano, katika Transcaucasia ilikuwa ni kwa sababu tabaka la wafanyakazi lilikuwa dogo na halikujumuishwa barabara vya kutosha. Kwa msaada wa mabeberu wa Kimarekani, Kiingereza, Kifaransa na baadaye wa Kijerumani, mabwanyenye wapendeleao kujibagua kitaifa wa Georgia na wa Azerbaijan walifaulu kwa muda fulani hivi kung'ang'ania utawala upingao mapinduzi uliotetea kujibagua kitaifa. Lenin alisema katika Julai 1918: "...Uhuru huu wa Georgia umekuwa ni uhadaifu mtupu. Kwa hakika hasa, unajumlikia kukaliwa na kunyakuliwa kabisa kwa Georgia kulikofanywa na mabeberu wa Kijerumani, muungano wa masinge ya Kijerumani na serikali ya Mamensheviki dhidi ya wafanyakazi na wakulima wa Kibolsheviki...".

Mfano mwingine ambapo mabwanyenye waliutumia kwa maslahi yao wenyewe mwongozo wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani na haki ya mataifa kujiamulia mambo yao yenyewe ulikuwa ni huo "utawala wa mambo ya ndani wa Kokand" (jumuiya ipingayo mapinduzi ya mabwanyenye wenye kujibagua kitaifa huko Kokand, ambayo katika Novemba 1917 ilijitangaza kama ndiyo "serikali" ya huko kwa kuhitilafiana na Baraza la Mawaziri wa Umma katika Tashkent ili kuitenganisha Turkestan na Urusi ya Kisovieti). Uliungwa mkono kwa juhudi na mabeberu wa Kiingereza ambao walitaka kuigeuza Turkestan kuwa koloni lao.

Tangu siku za mwanzo kabisa za dola la Kisovieti, Lenin aliyakashifu pasina huruma maja-

ribio yo yote ya maadui wa tabaka la wafanyakazi kutaka kuunyakua uhuru wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kama ni njia ambayo ingesaidia kuhifadhi utawala wa mabwanyenye wa kitaifa. Alifahamisha kwamba chini ya utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani umekuja kuwa na maudhui mapya. Uliundwa juu ya msingi wa Masovieti – mabaraza ya utawala wa tabaka la wafanyakazi na wakulima watumiao jasho lao. Ilikuwa ni kwa kupitia katika utaratibu wa Kisovieti tu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani (yaani, kwa kupitia katika vyombo vya utawala wa tabaka la wafanyakazi) ndiyo ikawezekana kutanzua tatizo la uhusiano baina ya mataifa: kupata uhuru wa kweli, usawa na urafiki baina ya mataifa, na kuyashirikisha mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla na kuzorota katika shughuli za ujenzi wa usoshalisti.

Lenin aliuona utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani juu ya msingi wa Masovieti sio tu kama ni umbo la kujiendesha wenyewe kwa majimbo, bali pia kama ni umbo la mamlaka ya kiserikali ya kitaifa ndani ya Jamhuri ya Urusi kwa watu wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla.

Wakati ule, utaratibu wa Kisovieti wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani ulikuwa ni chombo kikuu katika mapambano ya kuutenga umma kutokana na mabwanyenye wa kitaifa wapingao mapinduzi, chombo cha kusambazia utawala wa Kisovieti pembezoni mwa Urusi. Kama-

ti Kuu ya Chama cha Mabolsheviki, Serikali ya Kisovieti na Lenin nafsi yake walifanya ukomo wa uwezo wao kudhaminia kwamba taratibu za kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kwa mataifa zinaundwa juu ya msingi wa Masovieti.

Mwongozo huu ulitekelezwa katika upande wote mzima wa ujenzi wa taifa nchini. Risala ya simu iliyopelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa Tashkent wa Masovieti ya Turkestan tarehe 22 Aprili, 1918, ilisema kwamba Baraza la Mawaziri wa Umma litaunga mkono kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kwa jimbo hilo juu ya msingi wa Masovieti.

Tume ya Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima kuhusu mambo ya Turkestan ilitaja katika azimio mahsusi kwamba "wafuasi wa mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa wanajaribu kuzatiti mastakimu ya mabwanyenye wa kienyeji kwa kisingizio cha kutetea uhuru wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani". Tume hiyo ilifumua kampeni kubwa ili kuyakinza majaribio kama hayo.

Uundwaji wa jamhuri zenye kujitawala zenyewe kwa mambo ya ndani ulitekelezwa rasmi kwa vifungu mahsusi vya kisheria vilivyotungwa na Wizara ya Umma Kuhusu Mataifa. Tarehe 23 Machi, 1918, kulitolewa tangazo juu ya kuundwa kwa Jamhuri ya Kisovieti ya Watatar-Wabashkiria. Kulitungwa pia vifungu kuhusu uundwaji wa jamhuri zijitawalazo zenyewe kwa mambo ya ndani za Turkestan na nyinginezo, na kukaanza matayarisho ya kuunda Jimbo la Chuvash lenye

kujitawala kwa mambo ya ndani. Lakini kwa sababu ya kuanza kwa Vita vya Nchini na uvamizi wa kigeni, urajisiwaji wa sehemu mpya zenye kujitawala zenyewe kwa mambo ya ndani ulibidi usimamishwe.

Kama Lenin alivyobashiri, utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani juu ya msingi wa Masovieti ulikuwa ndiyo aina bora kabisa ya demokrasi, yenye uwezo wa kuuvutia umma wa mamilioni ya watu wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla kuja kushiriki kwa bidii katika ujenzi wa usoshalisti. Fursa kama hizo sasa ziliyafungukia mataifa ambayo kabla ya Mapinduzi ya Kisoshalisti ya Oktoba hayajakuwa na hata chembe ya mamlaka ya kiserikali yao yenyewe. Madhumuni ya utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani juu ya msingi wa Masovieti yalikuwa ni kuyawezesha mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla na kuzorota kijamii-kiuchumi kukuza mamlaka yao yenyewe ya kiserikali kwa lugha zao zenyewe, kuupeleka mbele utamaduni wao wenyewe, na kuzishirikisha sehemu kubwa sana za wakazi wa kienyeji katika shughuli za kujitawala wenyewe.

Mnamo robo ya pili ya 1918, Chama kilifafanua suala la kuimarisha mamlaka ya kiserikali juu ya msingi wa Masovieti miongoni mwa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo awali kwa maumbo yaliyofalia hali zao za kitaifa na za maisha ya kila siku. Liliendelezwa zaidi katika maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.) mnamo 1921. Katika azimio lake,

mkutano mkuu huo ulifafanua majukumu ya Chama katika kukomesha uzorotaji wa kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla, ukihimiza juu ya haja ya kuyasaidia kuimarisha mamlaka yao ya kiserikali juu ya msingi wa Masovieti na kukuza utaratibu wao wenyewe wa kisheria na wendeshaji, kuendeleza vyombo vya utawala vyenye wakazi wa kienyeji wa kike na wa kiume ambao wanajua vyema hulka ya wakazi wa huko na maisha ya kila siku, na pia magazeti yao, shule, majumba ya tamasha na vituo na taasisi nyingine za utamaduni na elimu zikitumia lugha za kienyeji; na kuunda mtando wa kutandaa sana wa mafunzo ya elimu ya kawaida na ya kazi ya ufundi na skuli maalumu za kufunza wafanyakazi wenye ujuzi na makada wa kiserikali na wa Chama kutoka miongoni mwa wakazi wa kienyeji.

Ulikuwa ni mpango wa kuyashirikisha mataifa yaliyokombolewa katika shughuli za shime za ujenzi wa usoshalisti kwa kuunda mamlaka za kujitawala wenyewe kitaifa.

Uhuru wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani juu ya msingi wa Masovieti ulitolewa kupewa mataifa na makabila yote ya Urusi yenye kupembulika kwa utamaduni, lugha na maisha ya kila siku ya aina yao ya kipekee, pasina kujali ukubwa wa idadi ya wakazi, eneo lao na mahali yalipo. Kwa maana hii, mataifa yote sasa yalikuwa na haki sawa. Lakini maumbo ya utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani yalitofautiana, ikitegemea juu ya kiwango chao cha maendeleo ya kijamii-kiuchumi na kiutamaduni,

juu ya kama yaliwahi hapo kabla kuwa na aina yo yote ile ya mamlaka ya kiserikali, juu ya makada wa kitaifa na masharti mengine: kulikuwa na jamhuri za kitaifa, majimbo, mikoa, wilaya, na baadhi ya wakati hata mitaa ya kitaifa. Hali za maisha za taifa zilivyokuwa zikibadilika, baadhi ya sehemu zenye kujitawala zenyewe ziligeuzwa, huku aina moja ikiipisha njia nyingine. Ubadilikaji huu wa utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani juu ya msingi wa Masovieti ulikuwa ni mojawapo ya sifa zake njema za mwanzoni kabisa, kwani ulifanya iwezekane kuzingatia aina chungu nzima mbalimbali za sehemu zilizoko pembezoni mwa Urusi, ambazo wakati ule zilikuwa na viwango mbalimbali vya maendeleo ya utamaduni na uchumi.

Utekelezwaji wa utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani juu ya msingi wa Masovieti kwa maumbo mbalimbali uliuwezesha utawala wa Kisovieti kupenya katika vitongoji vya ndani na vya mbali sana vya Urusi. Kwa hakika hasa, kiini cha utaratibu huo wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kilikuwa ni kuusaidia umma wa sehemu hizi za pembezoni mwa Urusi kuuelewa na kuukubali utawala wa Kisovieti kama ni wao wenyewe.

Lakini utekelezaji wa utaratibu huo wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani haukuwa ndilo jukumu pekee tu katika kutengeneza dola la Kisovieti lenye mataifa mengi na kuweka uhusiano wa usawa baina ya mataifa mbalimbali. Utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani watokeza upande mmoja tu wa suala hili,

nao ni umbo lenyewe na ukubwa wa huko kujiendesha wenyewe kitaifa, kujitegemea na kujitawala, ukubwa wa huko kujitegemea wenyewe kutokana na serikali kuu. Upande mwingine unahusika na umbo na tabia ya uhusiano baina ya mataifa, baina ya sehemu za kitaifa zijiendeshazo zenyewe za utawala wa kiserikali mnamo mipaka ya dola kuu moja.

Kama ijulikanavyo, umbo kama hilo ni uhusiano wa shirikisho (wa muungano). Lakini Chama hakikuutambua papo hapo uhusiano wa shirikisho kama ndilo umbo bora zaidi la mfumo wa kiserikali wa mataifa mbalimbali chini ya utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi.

Mabadiliko ya kimaendeleo ya maoni kuhusu suala la shirikisho yanaonyesha tabia ya kusanii, yenye kuendelea daima ya maongozi ya Marx kama mafunzo ambayo yanategemezwa juu ya majaribio na matendo ya kimapinduzi.

Kabla na wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza, wakati suala la uhusiano wa mataifa lilipokuwa kali mno, Lenin alijitokeza mbele mara kadhaa kupinga shirikisho. Wakati ule, aliuona mpango wa Chama juu ya uhusiano wa mataifa katika hali za mapinduzi ya kibwanyenye ya kidemokrasi na kushikilia kwamba katika jamhuri ya kibwanyenye shirikisho haliwezi kusaidia kutanzua tatizo la uhusiano wa mataifa au kuukomesha mkandamizo wa kitaifa.

Katika hali za Urusi, ambako tabaka la wafanyakazi la maeneo ya pembezoni mwa Urusi yakaliwayo na mataifa madogo lilikuwa na idadi ndogo ya watu, mwito wa shirikisho usingeweza

kupelekea ko kote isipokuwa katika kuundwa kwa madola ya kibwanyenye yenye kujibagua kitaifa. Hiyo ndiyo maana kwa nini Lenin akaona njia ya kuelekea katika ukombozi wa kitaifa iko katika mapambano ya kimapinduzi ya pamoja ya wananchi wafanyao kazi wa mataifa yote mnamo mipaka ya dola kubwa moja, lenye uongozi mkuu mmoja wa kidemokrasi, ambalo lingetosheleza siyo mahitaji ya ustawi wa kimaendeleo wa jamii tu, bali pia lingesaidia kuliimarisha tabaka la wafanyakazi juu ya msingi wa kimataifa.

Wakati ule, Lenin alitetea kwa ung'ang'anivu kanuni ya uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi, ambayo ingeweza kuwakilishwa kikamilifu zaidi katika jamhuri ya kidemokrasi iliyotangamana ikiwa na utaratibu wa kutandaa wa kujiendesha kwenye mitaa na kujitawala wenyewe kwa majimbo katika mambo yao ya ndani. Wafuasi wa maongozi ya Marx wamekuwa mara nyingi wakiiona maana ya shirikisho kama ni mwelekeo wa kutaka kujitenga.

Ingawa wakati ule maoni ya Lenin kuhusu shirikisho yalikuwa ni ya kupinga kabisa, hata hivyo alitambua kwamba katika hali fulani za kihistoria shirikisho lilihalalika kabisa kwa baadhi ya nchi. Mathalan, katika tasnifu yake, *Mapinduzi ya Kisoshalisti na Haki ya Mataifa Kujiamulia Mambo Yao Yenyewe*, aliainisha kwamba mtu anaweza kuwa mpinzani shupavu wa shirikisho kutokana na imani zake, lakini hata hivyo kulikubali baada ya unyonge wa kitaifa. Alisema kwamba Marx, kwa mfano, alipendelea shirikisho la Ireland na Uingereza wakati Waingereza walipokuwa wakiiti-

shia Ireland kuitawalia kwa nguvu.

Katika Oktoba 1912, Lenin alichapisha makala katika *Pravda* (gazeti la Chama) yenye kichwa cha maneno: *Sura Mpya ya Historia ya Dunia*, ambayo ndani yake aliuelezea mwito wa shirikisho uliotolewa na wafanyakazi wa safu ya mbele wa nchi za Balkan kama ni mwito wenye kutetea utanzuliwaji wa kidemokrasi vilivyo wa tatizo la uhusiano wa mataifa katika nchi za Balkan. Alitambua kwamba shirikisho la jamhuri za Balkan lingekuwa wakati ule ndiyo njia bora pekee ya kuokoka kwa mataifa ya Balkan, ambayo yalikuwa yako chini ya utawala wa Austria na Uturuki na kukabiliwa na hatari ya kuvamiwa na madola makuu ya kibwanyenye.

Lenin alionyesha kwamba suala la kujitenga au shirikisho laweza kuwa na usuluhisho wake tofauti kabisa ikitegemea juu ya mabadiliko ya hali zenyewe halisi zilizoko. Mathalan, mnamo miaka ya 1840-1860, wakati harakati za umma za kuwania uhuru zilipofumuka nchini Poland, Marx aliunga mkono kwa juhudi kuu dai la kujitenga kwa Poland kutokana na Urusi iliyokuwa chini ya utawala wa mfalme. Na mnamo mwanzoni mwa karne ya 20, wakati makao makuu ya harakati za kimapinduzi yalipohamia Urusi, Lenin aliliona dai la kujitenga kwa Poland kama "jaribio la kutaka kukitumia kile *kilichoandikwa* na Marx ili kukipinga kile *kilichokusudiwa* na mafunzo ya Marx".

Kwa hivyo basi, huku akipinga shirikisho kama mwongozo unaofalia kote wa utaratibu wa mamlaka ya kiserikali, Lenin mapema sana hata

kabla ya Mapinduzi ya Oktoba alikubali kuwa linaruhusika kwa baadhi ya nchi katika hali fulani, yaani huko ambako lilimaanisha hatua moja mbele ikilinganishwa na uzuiliwaji kwa nguvu wa taifa ndani ya dola moja na kusaidia kukomesha mkandamizo wa kitaifa.

Lenin alibainisha kwa mara ya mwanzo kabisa uwezekano wa kuwa na shirikisho nchini Urusi katika *Agizo Kwa Wajumbe Waliochaguliwa Viwandani na Mataponi wa Sovieti la Wajumbe wa Wafanyakazi na Maaskari.*

Akiuhutubia Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Urusi Nzima wa Masovieti katika Juni 1917, Lenin aliwabisha Mamensheviki, ambao walichapisha katika gazeti *Izvestia* dai la kutaka pahifadhiwe utaratibu wa wendeshaji serikali uliokuwako nchini Urusi kabla ya Mapinduzi ya Kibwanyenye ya Kidemokrasi ya Februari, 1917. Alisema kwamba hata mkutano mkuu wa wakulima ulikuwa karibu zaidi na ukweli, kwa sababu katika kudai jamhuri ya shirikisho ulitokeza fikira hiyo kwamba Jamhuri ya Urusi haitaki kulikandamiza taifa lo lote wala kutumia mabavu kuhusiana na taifa lo lote lile.

Katika kitabu chake *Serikali na Mapinduzi,* Lenin alitoa maoni yake kwa uthabiti zaidi kupendelea shirikisho kama mwongozo wa kijumla katika kutanzua tatizo la uhusiano wa mataifa katika dola lenye mataifa mengi, huku akiendelea kukosoa dosari za jamhuri ya shirikisho.

Kwa sababu ya mabadiliko makuu yaliyotokia nchini baada ya tabaka la wafanyakazi kutwaa madaraka, suala la shirikisho lilitokeza kwa njia

mpya, na papo tu baada ya Mapinduzi ya Oktoba Lenin aliita paweko uhusiano wa kishirikisho baina ya mataifa ya nchini.

Tayari katika "Ilani kwa Watu wa Ukraina..." iliyotolewa tarehe 3 Desemba, 1917, Lenin aliandika kwamba Jamhuri ya Ukraina ilikuwa na haki ama kujitenga kabisa na Urusi au kutia saini mkataba juu ya uhusiano wa kishirikisho na Jamhuri ya Urusi.

Sheria kuhusu Kamati za Ardhi, iliyopitishwa tarehe 4 Desemba na kusainiwa na Lenin, ilikuwa ndiyo sheria ya kwanza ambayo iliielezea Urusi ya Kisovieti kama jamhuri ya shirikisho na ambayo kwa mara ya kwanza kabisa iliifungamanisha pamoja maana ya kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani na shirikisho.

Azimio la Baraza la Mawaziri wa Umma kuhusu Jawabu ya *Rada* (Baraza la Utawala la Ukraina) kwa Baraza la Mawaziri wa Umma, lililotungwa na Lenin na kupitishwa na Baraza la Mawaziri wa Umma tarehe 30 Desemba, 1917, lilisema kwamba madai ya kitaifa ya Waukraina, uhuru wa jamhuri yao ya umma, na haki yake ya kudai uhusiano wa kishirikisho yanatambuliwa na Baraza la Mawaziri wa Umma. Katika nyaraka hizi, suala la uhusiano wa kishirikisho limeshakuwa tayari likiwasilishwa kimatendo.

Hatimaye, katika muswada wa *Tangazo la Haki za Watu Wafanyao Kazi na Wanyonywao* mnamo Januari 1918 Lenin aliandika kwamba Jamhuri ya Kisovieti ya Urusi inaasisiwa juu ya msingi wa muungano huru wa mataifa huru, kama shirikisho la jamhuri za kitaifa za Kisovieti. Katika hotuba

yake ya kufunga Mkutano Mkuu wa Tatu wa Urusi Nzima wa Masovieti, Lenin alisema: "Mfumo mpya wa kiserikali wa Jamhuri ya Kisovieti ya kisoshalisti, kama shirikisho la jamhuri huru za mataifa mbalimbali yakaayo Urusi, umeshakubaliwa hatimaye nchini humu katika upande wa siasa za ndani".

Mkutano Mkuu wa Tatu wa Urusi Nzima wa Masovieti, ambao ulipitisha *Tangazo la Haki za Watu Wafanyao Kazi na Wanyonywao* na azimio mahsusi "Kuhusu Taasisi za Shirikisho za Jamhuri ya Urusi", uliimarisha, kama Lenin alivyosema, utawala mpya wa kiserikali ulioasisiwa na Mapinduzi ya Oktoba.

Katiba ya Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti ya Shirikisho la Urusi iliyotungwa chini ya uongozi wa Lenin na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Tano wa Urusi Nzima wa Masovieti katika Julai 1918, ilithibitisha kisheria kwamba miungano ya majimbo yenye kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani iliingizwa katika Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti ya Shirikisho la Urusi juu ya msingi wa shirikisho.

Mpango uliopitishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Nane wa CKU(Mab.) katika 1919 ulisema kwamba ili kuiondosha tuhuma iliyokuwako miongoni mwa umma wa watu wafanyao kazi wa nchi zinazokandamizwa kwa tabaka la wafanyakazi la madola yaliyokuwa zamani yakizikandamiza nchi hizi, Chama kilipendekeza muungano wa kishirikisho wa madola hayo wenye kutegemezwa juu ya Masovieti kama umbo la kupita kwendea katika umoja kamili.

Basi, Lenin na Mabolsheviki wenzake walikuja kulitambua kikamilifu shirikisho kama umbo la mamlaka ya kiserikali kwa jamhuri za Kisovieti katika hali za ujenzi wa usoshalisti.

Kipi kilichomwezesha Lenin kufanya uamuzi kama huo?

Mnamo wakati wa Mapinduzi ya Kisoshalisti ya Oktoba, mataifa mengi yalikuwa kwa hakika hasa yametenganishwa mbalimbali. Nguvu zenye kupendelea mgawanyiko zilikuwa na athari kubwa sana. Msaada uliokuwa ukitolewa na wapinga mapinduzi wa ndani na ubeberu wa kimataifa katika kuziunga mkono serikali zipendeleazo kujibagua kitaifa ungeweza kupelekea kurejeshwa kwa mfumo wa kibepari nchini Urusi.

Katika hali hizi, wakati uhusiano baina ya sehemu ya katikati ikaliwayo na wafanyakazi na zile za pembezoni ulipovunjika, na wakati hizo za pili zingeweza kwa urahisi kuwa nyara ya ubeberu wa kimataifa na kuwa chombo chake katika kuchochelea uhasama wa kitaifa nchini kote, shirikisho la jamhuri za Kisovieti lilitokezea kuwa ndiyo njia madhubuti ya kuuunganisha umma wa wananchi wafanyao kazi wa mataifa yaliyotenganishwa, na hatua kuu ya kusonga mbele. Uundaji wa shirikisho ulifanywa uwe rahisi zaidi kwa hilo jambo kwamba katika kuitika mwito uliotokana na sera sahihi na yenye kugeuzika upesi ya Chama cha Mabolsheviki juu ya uhusiano wa mataifa, wananchi wafanyao kazi wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla walionyesha kupendelea kuungana kutoka kwa chini. Hata hivyo, njia ya kuelekea katika muun-

gano kama huo ilitokezea kuwa ngumu zaidi kuliko ilivyodhaminiwa kabla ya Mapinduzi ya Oktoba. Katika kadhia fulani, harakati za kitaifa zilipelekea takriban katika kujitenga hasa kwa mataifa, na hii ilionyesha kwamba mpango wa zamani, uliotungwa wakati harakati zipendeleazo kujibagua kitaifa zilipokuwa dhaifu kwa kiasi – mpango wa kujitawala kwa mambo ya ndani mnamo mipaka ya dola yenye utawala mmoja mkuu – ulikuwa haufai tena.

Mwishowe, kama tukizingatia ubishi wa kupinga shirikisho, uliotolewa kabla ya Mapinduzi ya Oktoba, yaani, huko kuchelea kwamba muundo wa kishirikisho utakwenda kinyume na shabaha za kuwa na uongozi mmoja mkuu, basi matendo yenyewe yameonyesha kwamba maumbo ya shirikisho yaliyokuwa yakianza kuchomoza wakati wa ujenzi wa usoshalisti hayakukinza, bali yalisaidia kuyajongeza karibu zaidi mataifa mbalimbali ya Urusi kwa upande wa uchumi, hayakuhitilafiana na kanuni za uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi. Umbo jipya la mamlaka ya kiserikali, juu ya msingi wa Masovieti, lililogunduliwa na Lenin lilifanya iyumkinike kuchanganyisha juhudi za kienyeji za upeo mpana na umoja madhubuti kabisa.

Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.) ulibainisha katika maazimio yake kwamba shirikisho la jamhuri za Kisovieti lilikuwa ni umbo la kijumla la muungano wa kiserikali ambalo lilifanya iwezekane: a) kudhaminia utangamano na maendeleo ya kiuchumi ya jamhuri mbalimbali na shirikisho lote kwa jumla; b) kuzingatia vi-

livyo hali zote tofauti za maisha ya kila siku, za utamaduni na uchumi za mataifa na makabila mbalimbali yaliyoko kwenye daraja tofauti za maendeleo yao, na kutumia umbo la shirikisho linalofalia barabara; c) kutengeneza hali za kuishi pamoja kwa amani na ushirikiano wa kidugu baina ya mataifa na makabila ambayo yameshaifungamanisha sudi yao kwa njia hii au ile na sudi ya shirikisho.

Lenin alisisitiza mara kadha wa kadha kwamba shirikisho, likiwa kama umbo la uhusiano baina ya mataifa, halidhaminii wenyewe kwa wenyewe tu mchanganyiko barabara wa majukumu ya mitaa na yale ya serikali kuu. Linatoa fursa zote kwa hayo, ilhali utumiwaji wa fursa hizi wategemea juu ya vipi shirikisho linavyowiana na kanuni za uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi. Katika muswada wake mwanzoni wa makala *Majukumu ya Papo ya Utawala wa Kisovieti*, Lenin alitilia mkazo kwamba endapo shirikisho likitekelezwa mnamo mipaka ambayo ni ya busara, kutokana na maoni ya upande wa uchumi, endapo likitegemezwa juu ya mipembuo muhimu ya kitaifa ambayo inapelekea kuzuka haja halisi ya kuwa na kiasi fulani cha uhuru wa kiserikali, basi linakuwa halihitilafiani kwa vyo vyote vile na uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi.

Lenin aliweka nadhari kubwa katika kudhamini kwamba kila sehemu ijitawalayo yenyewe kwa mambo ya ndani katika dola la Kisovieti la shirikisho iwe na kila inachokihitajia kwa maendeleo yake ya kisiasa na ya kiuchumi, lakini wakati huo huo, maslahi ya kijumla ya dola lenye

uongozi mmoja mkuu yasisahauliwe au kudhuriwa. Hiyo ndiyo maana kwa nini kila utaratibu wa kujitawala kwa mambo ya ndani unapoanzishwa hapa au pale, kila mara huamuliwa haki zake maalumu halikadhalika na zile za dola zima. Chama kiliendesha mapambano dhidi ya wale wanaopepelea kiburi cha utaifa halikadhalika na wale wanaopendelea kujibagua kitaifa, ambao waliyapambanisha malengo yao ya kitaifa yaliyopakika mno na yale ya nchi nzima ya Kisovieti.

Mathalan, wakati wa kuundwa kwa Jamhuri ya Bashkiria madaraka ya vyombo vyake vya kuendeshea serikali yalikuwa hayakufafanuliwa barabara, kwa hivyo wafuasi wa mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa waliomo katika kamati ya kimapinduzi ya Bashkiria hawakukawia kuichukulia fursa hali hiyo ya mambo. Walijaribu kutafsiri mamlaka ya Bashkiria ya kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kama ni uhuru kamili kutokana na Urusi ya Kisovieti, hata serikali mkuu ikabidi kutoa dikrii mahsusi "Kuhusu Mfumo wa Kiserikali wa Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti Ijitawalayo Wenyewe kwa Mambo ya Ndani ya Bashkiria", ambayo ilifafanua mipaka ya usambazaji madaraka. Mambo yote ya nje na biashara ya nje yalibakia chini ya mamlaka ya serikali kuu, na wizara za kienyeji zilikuwa chini ya amri ya wizara zinazohusika za Shirikisho la Urusi.

Akikusudia utaratibu wa kishirikisho wa dola, Lenin alishikilia kwamba uongozi mmoja mkuu, kama uelewekavyo kwa maana ya kidemokrasi

kikweli, wakusudia fursa, iliyopatikana kwa mara ya kwanza katika historia, ya kukuza kikamilifu na pasina kukinzwa siyo tabia fulani mahsusi tu za kienyeji, bali pia uwezo wa kienyeji wa kutoa mapendekezo, wa kutoa juhudi, pia kuendeleza njia, mbinu na nyenzo za usongaji mbele kuelekea kwenye lengo la pamoja.

Chini ya utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi, jamhuri za shirikisho zaweza kuwa na kiasi kikubwa cha uhuru, ambao haugongani na majukumu ya uongozi mmoja mkuu siyo tu kwa sababu ya tabia ya kimataifa ya utawala huo wenyewe, bali pia kwa sababu Chama cha Kikomunisti kinachotawala kimejengwa juu ya msingi wa uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi. Chaweza siku zote, kwa kupitia katika jumuiya zake, kuhakikisha kwamba kunakuwako mizani barabara baina ya maslahi ya kienyeji na yale ya serikali kuu.

Akitetea uundwaji wa vyama vya kikomunisti vyenye kujitegemea wenyewe katika jamhuri za Kisovieti zijitawalazo zenyewe, Lenin alidai kwamba yapasa vyama hivi vichukuliwe kama ni sehemu zisizotenganishika za Chama kizima cha Kikomunisti cha Urusi (cha Mabolsheviki). Mathalan, azimio "Kuhusu Kazi ya Kikomunisti huko Armenia", lililopitishwa na Halmashauri ya Kisiasa ya KK ya CKU(Mab.) tarehe 3 Januari, 1920, kwa kushirikiwa na Lenin, lilisema kwamba mapambano ya kupinga kiburi cha utaifa cha kienyeji na haja ya kuleta hali za kufalia uenezaji wa mawazo ya mapinduzi ya kisoshalisti miongoni mwa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa

na utawala wa mfalme wa Kirusi, yalifanya iwe lazima kwa jumuiya za kikomunisti katika madola "yenye kujitegemea yenyewe" ambayo kwa hakika hasa yalichomoza mnamo mipaka ya mamlaka ya zamani ya Urusi, kuendesha shughuli zao kama vyama vya kikomunisti vijitegemeavyo vyenyewe. Jumuiya za kikomunisti zilizokuwa zikiundwa katika maeneo yanayokaliwa na mataifa madogo kwa mujibu wa mwongozo huu wa Lenin, zilijiona kama ni sehemu isiyotenganishika ya CKU(Mab.).

Kwa mataifa ya nchi hii, Chama cha Kikomunisti kilikuwa ni kifani cha ushikamano wa kimataifa, nguvu iliyowaunganisha wananchi wafanyao kazi wa mataifa yote na kuongoza shughuli za jumuiya zote.

Hivi ndivyo Lenin alivyoyaelezea haya katika ripoti yake kwenye Mkutano Mkuu wa Tisa wa CKU(Mab.): "...Hadhi ya Chama iliziunganisha idara na taasisi zote za kiserikali, kwa sababu miito iliyotolewa na Kamati Kuu iliitikiwa kwa pamoja na makumi, mamia, maelfu na hatimaye mamilioni ya watu...". Ilikuwa ni kwa sababu hiyo tu ndiyo sisi tukaweza kupata ushindi. Katika hotuba yake kwenye Mkutano wa Urusi Nzima wa Waenezaji wa Elimu ya Siasa wa Idara za Elimu za Mikoa na Mitaa, alitilia mkazo kwamba "Katiba yote ya Jamhuri ya Kisovieti imetegemezwa, kisheria na kimatendo, juu ya msingi huo kwamba Chama kunasahihisha, kinapanga na kujenga yote kwa mujibu wa mwongozo mmoja".

Chini ya utawala wa kipekee wa tabaka la wa-

fanyakazi, ambapo Chama cha Kikomunisti huwa kinatwaa jukumu la uongozi, na maslahi makuu ya wananchi wafanyao kazi wa mataifa yote huwa yanalingana, uhusiano wa kishirikisho wa usawa baina ya jamhuri unapelekea katika umoja mkubwa zaidi na ujongeleanaji karibu zaidi wa mataifa, ukisaidia kung'oa kabisa mabaki ya mtindo wa kujibagua kitaifa na kueneza itikadi ya urafiki baina ya mataifa.

Maumbo halisi ya utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani na shirikisho yalitegemea juu ya kiwango cha maendeleo ya kiuchumi na kiutamaduni ya mataifa yaliyojiunga na shirikisho hilo na kukamilishwa, kufafanuliwa na kuainishwa kisayansi zaidi kwa kadiri dola la Kisovieti na kila taifa lililokuwamo ndani yake lilivyokuwa likiendelea. Lenin alitilia mkazo kwamba taifa laweza kujaribu aina mbalimbali za mahusiano ya kishirikisho mpaka lijiamulie aina ile inayolifalia vizuri zaidi. Chaguo la aina hii au ile ya shirikisho lategemea juu ya maendeleo ya ndani ya mataifa yanayohusika, juu ya kama tabaka la wafanyakazi limeweza kuishinda hali hiyo ya kuyumbayumba kwa wakulima, juu ya nguvu ya mielekeo ya kujibagua kitaifa, n. k.

Utawala wa Kisovieti ulitumia kwa mafanikio aina mbalimbali za shirikisho: zile zenye kutegemezwa juu ya kujitawala kwa mambo ya ndani (Bashkiria, Tataria, Daghestan na jamhuri nyinginezo); juu ya uhusiano wa ki-mkataba na jamhuri huru za Kisovieti (Ukraina na Azerbaijan katika 1920); na zile zilizomo ndani ya daraja za katikati baina ya hizi (kama Turkestan na Byelo-

russia). Baadaye kulikuwa na mashirikisho ya jamhuri za Transcaucasia na Asia ya Kati, na hatimaye, Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti. Maisha yenyewe yalisaidia kuchagua umbo bora kabisa na wakati wa kufalia vizuri kabisa.

Mabadiliko haya kwa vikubwa sana yalisababishwa na kuimarisha mastakimu ya usoshalisti. Matukio ya mambo katika Asia ya Kati yanaonyesha vizuri sana jinsi gani maumbo ya fungamano za shirikisho yalivyokamilishwa kwa kadiri mataifa ya huko yenyewe yalivyokuwa yakiendelea, kadhalika mahusiano ya kisoshalisti ya uzalishaji mali yalivyokuwa yakiimarika.

Mnamo miaka ya mwanzoni ya utawala wa Kisovieti, Vita vya Nchini vilifanya iwe ni muhali kutekeleza mpango wa kuyapambanua mataifa huko Asia ya Kati, na wakazi wote wa huko waliunganishwa katika jamhuri moja ya Turkestan, ambayo ilikuwa ni sehemu ya Shirikisho la Urusi.

Matukio ya baadaye zaidi ya mambo huko Asia ya Kati yalipelekea kuchomoza kwa jamhuri za Bukhara na Khiva. Wakati wa kuundwa kwa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti, jamhuri hizi ziliendelea kuwa na uhusiano wa ki-mkataba na Shirikisho la Urusi. Ilikuwa ni mnamo 1924 tu ndipo jamhuri za Asia ya Kati zilipopembuliwa kwa mujibu wa mataifa yao. Kwa kadiri zilivyokuwa zikiendelea, jamhuri za Asia ya Kati zilikuja kuwa Jamhuri za Muungano za Soviet Union (yaani Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti).

Bila ya shaka, umbo hili au lile la shirikisho ha-

likubadilisha madhumuni yake makuu, ambayo yalikuwa ni kudhaminia, kama Lenin alivyosema, "ukiukaji kwendea katika umoja *wa fahamu* na mkubwa zaidi wa wananchi wafanyao kazi, wakati watakapokuwa wameshajifunza kukwea *kwa hiari yao* juu zaidi kupindukia uhasama wao wa kitaifa", kwendea katika urafiki mkubwa zaidi baina ya mataifa.

Kwa hivyo basi, shirikisho la Kisovieti lilitokezea kuwa ndilo umbo la kufalia zaidi la ushirikiano baina ya mataifa mnamo mipaka ya dola la mataifa mengi katika kipindi cha ukiukaji kutoka ubepari kuingia katika usoshalisti. Kama uzoefu wa nchi hii uonyeshavyo, shirikisho laweza kutumiwa kama umbo la kukuza maendeleo ya dola la kisoshalisti la mataifa mengi katika awamu ya ujenzi wa ukomunisti vile vile.

Lakini wakati tulichukuliapo shirikisho kama umbo la ushirikiano baina ya mataifa katika dola la kisoshalisti lenye mataifa mengi kwa jumla, je, si tunakuwa, pengine, tunalipuuza dai muhimu sana la Lenin kuhusu mkabala halisi wa kihistoria katika kuamua maumbo ya mamlaka ya kiserikali ya kitaifa?

Bila ya shaka, Lenin alifikilia uamuzi huo juu ya uwezekano na uhitajiko wa kuanzisha uhusiano wa kishirikisho baina ya jamhuri za Kisovieti kutokana na hali halisi za kihistoria za Urusi. Lakini uzoefu wa Urusi waonyesha kwamba baada ya mapinduzi ya kisoshalisti uhusiano wa kishirikisho baina ya mataifa mnamo mipaka ya dola la mataifa mengi ni wenye kufalia zaidi. Suala la kama dai la kutaka shirikisho litolewe au lisitole-

we kama mwito wa kuujumuisha umma kwa mapinduzi ya kisoshalisti lategemea hali halisi za kihistoria. Aina au umbo la uhusiano wa kishirikisho baada ya mapinduzi lategemea pia juu ya hali hizi halisi, lakini siyo tabia yenyewe hasa ya uhusiano huu, ambayo kwa vikubwa sana ni ya kishirikisho. Katika *Mtungo wa Mwanzoni wa Tasnifu Kuhusu Suala la Mataifa na la Ukoloni kwa Mkutano Mkuu wa Pili wa Jumuiya ya Kikomunisti ya Kimataifa* (waraka uliokusudiwa kwa ajili ya harakati za kikomunisti za kimataifa), Lenin alitoa fikira ya shirikisho kama umbo kamili baina ya watu wafanyao kazi wa mataifa mbalimbali, akiutaja mfano wa uzoefu wa uhusiano na Hungary na Finland, na kuita pafanywe majaribio ya kimatendo ya "uzoefu wa mashirikisho haya mapya, ambayo yanazuka juu ya msingi wa mfumo wa Kisovieti na harakati za Kisovieti". Haya yaonyesha kwamba aliliona shirikisho kama ni umbo la uhusiano baina ya mataifa linalofalia siyo kwa Urusi tu.

Baada ya mapinduzi ya kisoshalisti, mataifa yaliyokombolewa ya Urusi yalivutikia katika muungano na tabaka la wafanyakazi la Urusi, yakiuthamini vilivyo msimamo wake wa kuheshimu usawa na mamlaka yao. Taifa la Warusi lilikuwa la mwanzo kushika njia ya mageuzi ya kisoshalisti na kutoa kila msaada uyumkinikao kuyapa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo zamani katika maendeleo yao ya kiuchumi na ya kisiasa.

Uundwaji wa Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti ya Shirikisho la Urusi (JKKSU) ulikuwa ni tukio lenye umuhimu wa kihistoria kwa dunia

nzima. Shirikisho la Urusi, lililotegemezwa juu ya msingi wa utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani, lilitumika kama kifani cha muundo wa kiserikali kwa jamhuri nyingine za Kisovieti. Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU (Mab.) ulitaja katika maazimio yake kwamba JKKSU ilikuwa ni nchi pekee ulimwenguni ambako majaribio ya kuishi pamoja kwa amani na ushirikiano wa kidugu baina ya mkururo mzima wa mataifa na makabila juu ya msingi wa kuaminiana na kuwania muungano kwa hiari kwa upande wa wananchi wafanyao kazi wa mataifa mbalimbali yametokezea kuwa ni ya kufana.

Utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani mnamo mipaka ya Shirikisho la Urusi ulisaidia kuondosha tuhuma iliyokuwako kwa Warusi miongoni mwa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla. Bila ya kuundwa kwa JKKSU, ambayo ndani yake Warusi waliyasaidia mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa zamani kuutupilia mbali mkatale wa kijamii na wa kitaifa na walikuwa ndio mwitifaki wao wa kweli katika kuinua kiwango chao cha uchumi na utamaduni na kuyashirikisha katika shughuli za wendeshaji wa serikali, ingekuwa ni muhali kuweza kukomesha uhasama baina ya mataifa mnamo kipindi kifupi sana kama hicho.

Shirikisho la Urusi lilitenda kazi muhimu sana katika uundwaji wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti. Mathalan, bila ya msaada wake isingewezekana kuunda jamhuri za Kisovieti, ambazo uhuru wao ulitambuliwa nalo. Ilikuwa ni kwa kuitegemea JKKSU tu ndiyo

jamhuri hizo huru ziliweza kuyathibitisha rasmi na kuyaimarisha mamlaka yao ya kiserikali, kuuhami uhuru wao na kustawisha uchumi na utamaduni wao. Serikali ya Urusi ya Kisovieti ilitoa msaada mkubwa sana kuyapa mataifa yote yaliyoanza kujenga mamlaka yao yenyewe ya kiserikali, ikiyapatia mikopo, vifaa mbalimbali na vyakula, na kuyapelekea wataalamu wenye ujuzi mwingi, n. k.

Katiba ya kwanza ya Kisovieti ya JKKSU ilikuwa imetegemezwa juu ya maongozi ya Lenin kuhusu ujenzi wa dola la Kisovieti lenye mataifa mengi. Lenin nafsi yake alishiriki katika utungaji wa Katiba hiyo. Watu wafanyao kazi wa nchi zote, aliandika, wataona kwamba Katiba ya Kisovieti yawakilisha malengo ya tabaka la wafanyakazi la dunia nzima.

Sura ya Tatu

AWAMU KUU KATIKA UUNDIKAJI WA DOLA LA KISOVIETI LILILOTANGAMANA LA MATAIFA MENGI

Katika "Barua kwa Wafanyakazi na Wakulima wa Ukraina Kuhusu Ushindi Uliopatikana Dhidi ya Denikin *", Lenin alitilia mkazo kwamba muungano wa mataifa yapasa uwe kwa hiari tu na utegemezwe juu ya utambuzi wazi wa umoja wa kidugu, na kwamba ni lazima kuitekeleza kazi ya kuleta muungano huo kwa uvumilivu na hadhari kubwa sana, ili kutozusha tuhuma, ili kuondosha tuhuma iliyokuwako kwa makarne kadhaa kwa sababu ya ukandamizi wa makabaila na mabepari.

Dola la Kisovieti la mataifa mengi lilipitia awamu kadhaa katika maendeleo yake: uundwaji wa muungano wa kijeshi-kisiasa wa jamhuri huru za Kisovieti, ukijaliziwa kwa uhusiano wa ki-mkataba baina ya jamhuri hizo na, baadaye,

* *Denikin* – jemadari wa jeshi la mfalme, aliongoza mapambano ya kupinga mapinduzi huko Kusini mwa Urusi mnamo miaka ya Vita vya Nchini. – *Mhariri.*

kwa umoja wao wa kidiplomasia; na uunganishwaji wa jamhuri huru katika dola moja la Muungano.

Muungano wa Kijeshi-Kisiasa wa Mataifa

Katika hali za dola la mataifa mengi, ambapo wapinga mapinduzi walifanya juu chini kuyafarakisha mataifa ili kuupindua utawala wa Kisovieti, matokeo ya vita yalitegemea ushikamano na umoja wa vitendo wa wananchi wafanyao kazi wa mataifa yote.

Shukrani kwa sera sahihi ya Chama cha Mabolsheviki kuhusu suala la mataifa na shughuli zake za kujisabilia kabisa katika upande huo, umma wa wananchi wafanyao kazi wa sehemu za pembezoni mwa nchi zikaliwazo na mataifa madogo haukuziunga mkono harakati za mabwanyenye za kujibagua kitaifa zilizokuwa na madhumuni ya kujitenga na Urusi ya Kisovieti. Tangu hata katika Desemba 1917, Lenin alisema: "Matukio ya karibuni katika Ukraina (kwa sehemu pia katika Finland na Byelorussia, halikadhalika na huko Kaukasi) yanaonyesha kwa hali moja huko kujipanga upya kwa nguvu za kitabaka ambako kunatukia katika mwendo wa mapambano baina ya mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa wa *Rada** ya Ukraina,

* Baraza la utawala.– *Mfasiri.*

*Diet** ya Finland, n. k., kwa upande mmoja, na utawala wa Kisovieti, mapinduzi ya wafanyakazi na wakulima katika kila moja ya jamhuri hizi, kwa upande mwingine".

Jamhuri huru za Kisovieti zilizokuwa zikiundwa pembezoni mwa Urusi wakati wa Mapinduzi ya Oktoba na Vita vya Nchini zilielezea utayari wao kuweka mawasiliano makubwa zaidi na Urusi na jamhuri nyinginezo za Kisovieti. (Ukraina ilianzisha fungamano kama hizo na JKKSU tarehe 5 Februari, 1918, na Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti zilizojipatia uhuru wao karibuni za Lithuania, Latvia, Byelorussia na Estonia, mnamo mwishoni mwa 1918.)

Uhusiano wa kirafiki ulioanzishwa baina ya jamhuri za Kisovieti tangu siku za mwanzo kabisa za kuchomoza kwao kwa hakika hasa ulijumlikia kuwa muungano wa kijeshi-kisiasa uliosababishwa na haja ya kupambana na wapinga mapinduzi wa kimataifa na wa ndani. Lakini kulihitajika juhudi nyingi na shughuli za pande zote kwa upande wa Chama cha Lenin kwa ajili ya kuudumisha na kuuendeleza muungano huu ili kuzishinda nguvu zote zipingazo mapinduzi na kuunda dola huru la Kisovieti lililotangamana na lenye mataifa mengi.

Chama cha Mabolsheviki kilifanya kazi kwa bidii ili kuyakashifu masengenyo ya Mamensheviki na Wasoshalisti-Wanamapinduzi, ambao walijaribu kuushawishi umma uamini kwamba

---

* Baraza la utawala.–*Mfasiri.*

Mabolsheviki wameyahadaa mataifa, wakiyaletea vita badala ya hiyo amani waliyoahidi. Katika nyaraka za Chama na hotuba chungu nzima zilizotolewa na Lenin, mlitiliwa mkazo kwamba mataifa ya Kisovieti yalishurutishiwa vita kwa nguvu na matabaka ya kinyonyaji ya Urusi na mabeberu wa Uitifaki wa Madola (uitwao *Entente*) na Marekani. Serikali ya Kisovieti ilitoa tena na tena mapendekezo ya amani kwa nchi za Uitifaki wa Madola, lakini mapendekezo haya yalikataliwa. Zikienda kinyume na maslahi ya kitaifa ya jamhuri zao, serikali za kibwanyenye zenye kujibagua kitaifa zilitekeleza matakwa ya mabeberu wa kigeni na kuyakataa mapendekezo yote ya utawala wa Kisovieti ya kuendesha mapambano ya pamoja dhidi ya wavamizi wa kigeni. Umma uliona kutokana na uzoefu wao wenyewe kwamba ni utawala wa Kisovieti tu ndio uwezao kuyapatia mataifa uhuru wao.

Mpango mpya, ambao ulipitishwa na Mkutano Mkuu wa Nane wa CKU(Mab.) wakati wa kutukia kwa Vita vya Nchini na uvamizi wa kigeni (1919) na ambao uliainisha, kati ya mambo mengine, majukumu ya Chama katika upande wa sera ya uhusiano wa mataifa, ulikuwa ni wenye umuhimu mkuu wa kimatendo, halikadhalika na wa kinadharia kwa kuimarisha muungano wa mataifa ya nchini.

Akikanusha hoja zilizotolewa na wapinzani wake, ambao walidai kwamba mwito wa kujiamulia wenyewe kwa mataifa yapasa uondoshwe, Lenin alisema kwamba njia ya kuongozea katika kujiamulia wenyewe kwa wananchi wafanyao ka-

zi iko katika huko kujiamulia wenyewe kwa kila taifa kwa jumla, kwa sababu kabla wawakilishi wa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo zamani hawajajihisi wenyewe kama wananchi wafanyao kazi, wanajiona nafsi zao kama ni watu wa taifa fulani. Mabwanyenye wa kitaifa wanalitumia jambo hilo kwa manufaa yao, wakijaribu kuzidhibiti harakati za kitaifa.

Ili kuwafanya wananchi watumiao jasho lao watengane na mabwanyenye "wao wenyewe", inabidi wafahamu kwamba Warusi hawawakandamizi kwa vyo vyote vile, na kwamba adui yao wa kitabaka ni mabwanyenye wa kitaifa. Mwendo wa kujiamulia wenyewe ulikuwa ndiyo kwanza unaanza nchini Urusi, na unyimaji wa haki ya mataifa kujitenga ungepelekea kuzidisha tuhuma tu kwa Urusi ya Kisovieti miongoni mwa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo zamani. Lenin alithibitisha kwamba wapinzani wake walipuuza ukweli wa mambo uliokuwako, kadhalika njia za kupindapinda za kufanya mipembuo ndani ya mataifa.

Kwenye Mkutano Mkuu wa Nane wa CKU (Mab.), Lenin alifafanua maoni ya kihistoria na kitabaka juu ya suala kuhusu nani anayewakilisha matakwa ya taifa, akilitanzua tatizo hili kwa mujibu wa awamu ya maendeleo ya kihistoria ya taifa linalohusika. Katika awamu ile ya maendeleo ya kijamii ambapo mabwanyenye wameshamaliza kabisa kutekeleza jukumu lao la kimaendeleo, ambapo wanaendesha mapambano dhidi ya nguvu za kimapinduzi na wako tayari kuyatoa mhanga maslahi ya kitaifa ili kuhifadhi mastaki-

mu yao ya kitabaka, tabaka la wafanyakazi linakuwa ndiye mtetezi halisi wa maslahi haya ya kitaifa. Likiongozwa na jeshi lake la mbele la kimapinduzi, ambalo limeandaliwa kwa maarifa ya kawaida za maendeleo ya kijamii, tabaka la wafanyakazi linatetea maslahi ya kitaifa na kuamua mahitaji na matazamio ya maendeleo ya taifa, jambo ambalo linaliwezesha kujumuisha chini ya uongozi wake nguvu zote za kimaendeleo za taifa.

Akidai paendeshwe mapambano makali dhidi ya kiburi cha utaifa cha dola kuu kwa mitokezo yake yote, Lenin aliamini kwamba maoni ya mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo zamani kwa Warusi, wakiwa kama ni wawakilishi wa taifa lililokuwa likitawala hapo awali – maoni yaliyorithiwa kutokana na utawala wa mfalme wa Kirusi – hayawezi kukomeshwa kwa kutoa dikrii tu. Alitilia mkazo kwamba taifa la Warusi lapaswa liwe na hadhari sana katika kudhaminia usawa halisi wa mataifa na uhuru wa kujitenga ili kuondosha sababu zo zote za kutoaminiana na kupata muungano wa hiari wa mataifa yote.

Mathalan, wakati Lenin alipopata habari ya ugomvi uliozuka baina ya uongozi wa kijeshi wa mpakani na serikali ya Ukraina, alimpelekea simu V. A. Antonov-Ovseyenko * tarehe 21 Januari, 1918, akielezea masikitiko yake makubwa kuhusu jambo hilo na kumsihi: "Kwa hisani yako, fanya *kila* uwezalo ili *kukomesha* ugomvi

---

* *Antonov-Ovseyenko* – mmojawapo wa waanzilishi wa Jeshi Jekundu. – *Mhariri.*

w o t e.... Jambo hili ni muhimu sana kwa *d o l a*... yatambue mamlaka yao ya kujitawala kwa *u m b o l o l o t e l i l e*.... Hapa panahitajia hadhari kubwa kwa hisia *z a k i t a i f a*".

Azimio la Mkutano Mkuu wa Nane wa CKU (Mab.) juu ya maoni kuhusiana na wakulima wa hali ya wastani lilikuwa ni lenye umuhimu mkuu na wa kimsingi kwa kuimarisha muungano wa kijeshi-kisiasa wa mataifa ya nchini. Mkutano huo ulitangaza ukiukaji kutoka sera ya kuwafanya wakulima wa hali ya wastani wasiwe na madhara kwendea katika kuungana nao barabara chini ya uongozi wa kudumu wa tabaka la wafanyakazi.

Wakati ule, wakulima wa hali ya wastani walikuwa ndio wingi wa wakazi wa nchini, na mustakbali wa utawala wa Kisovieti hatimaye ulitegemea juu ya kiasi kile ambacho wakulima wa hali ya wastani wataliunga mkono tabaka la wafanyakazi katika mapambano dhidi ya wapinga mapinduzi wa ndani na uingilizi wa kigeni, na katika kujenga jamii ya kisoshalisti.

Mnamo kipindi cha mwanzoni cha Vita vya Nchini, wakulima wa hali ya wastani waliendelea bado kujiachilia nafsi zao kuchochelewa na Kolchak * na Denikin, ambao waliitumia hulka ya kibwanyenye uchwara ya wakulima kwa manufaa yao, kadhalika uhadaifu wa Mamensheviki na Wasoshalisti-Wanamapinduzi ambao waliupaka matope utawala wa kipekee wa tabaka la

---

* *Kolchak* – admeri wa jeshi la wanamaji la mfalme, aliongoza uasi wa kupinga mapinduzi huko Siberia wakati wa Vita vya Nchini.– *Mhariri.*

wafanyakazi kwa kila njia na kuwaahidi wakulima matunda ya "demokrasi safi" na "usawa wa wote". Vibwanyenye uchwara vipendeleavyo kujibagua kitaifa viliyatumia makosa katika utanzuaji wa suala la ardhi yaliyofanywa na Wakomunisti katika mitaa fulani. Lenin aliona hatari kuu ya makosa haya, hasa katika sehemu zile zikaliwazo na mataifa madogo, na kusaidia katika kuyasahihisha.

Akiainisha majukumu yanayowakabili Wakomunisti katika sehemu zikaliwazo na mataifa madogo, Lenin aliwahimiza kabla ya yote kutafuta njia barabara ya kutanzua suala la ardhi na kuzingatia vilivyo tabia mahsusi za sehemu hizo.

Umuhimu wa kihistoria wa maazimio yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa Nane wa CKU (Mab.) ulikuwa ni kwamba yaliainisha sera ya kuwavutia wakulima watumiao jasho lao kujia upande wa utawala wa Kisovieti, jambo ambalo hatimaye liliamua matokeo ya mapambano dhidi ya majeshi ya wapinga mapinduzi. Muungano wa kudumu na wakulima wa hali ya wastani ulimaanisha pia kuwashirikisha katika shughuli za kujenga usoshalisti watu wafanyao kazi wa sehemu za pembezoni mwa nchi zikaliwazo na mataifa madogo, ambao kwa wingi sana ni wakulima. Lenin alishikilia paweko mkabala tofauti kwa matabaka tofauti ya wakulima wa sehemu za pembezoni mwa nchi zikaliwazo na mataifa madogo kwa kuzingatia tabia za kipekee za kila taifa. Alisema kwenye Mkutano Mkuu wa Nane wa CKU(Mab.): "...Sisi kwa vyo vyote vile hatutajifungia nafsi zetu kwa kufuata njia fulani zile kwa

zile; hatutaamua papo hapo na milele kwamba uzoefu wetu, uzoefu wa Urusi ya Kati, lazima utumiwe kila mahali kama hivyo ulivyo". Kwenye Mkutano wa Nane wa Urusi Nzima wa CKU(Mab.), Lenin aliwapinga vikali ndugu wale wa Ukraina ambao walipuuza maelekezo ya Kamati Kuu ya CKU(Mab.) kuhusu suala la wakulima. Aliwakosoa wale ambao walitaka kuanzisha mashamba ya serikali huko Ukraina kwa upeo mkuu, alifahamisha kwamba sehemu ndogo tu ya miliki ya ardhi ya makabaila ya zamani ndiyo inayoweza kutumiwa kwa kuanzisha mashamba ya serikali, kwa sababu "ama sivyo hatutaweza kupata muungano na wakulima wa hali ya chini, ilhali sisi twauhitajia sana muungano huo".

Lenin aliona kuwa ni muhimu sana kutanzua suala la ardhi katika Kaukasi, ambako suala hili lilikuwa ni la hima sana.

Lenin aliwataka Wakomunisti wawe na mkabala mahsusi kuhusu wakulima wa Mashariki. Aliwafunza Wakomunisti wale waliokuwa wakitumika huko Mashariki kutumia nadharia na matendo ya kikomunisti ya kijumla katika sehemu hizi kwa kulingana barabara na hilo jambo kwamba jukumu la awali na la mbele kabisa huko lilikuwa hasa ni kung'oa mabaki ya Zama za Kati, wala siyo kupambana na rasilmali. Ili kukomesha uhusiano usio wa kawaida baina ya walowezi wa Kirusi na wenyeji wa kiasilia wa mataifa ya huko, Lenin alibainisha katika kumbukumbu zake juu ya Muswada wa Azimio la Kamati Kuu Kuhusu Majukumu ya CKU(Mab.) katika

Turkestan katika Juni 1920, ardhi zilizotwaliwa hapo awali kutoka kwa wenyeji wa huko na kupewa walowezi wa Kirusi lazima zirejeshwe kwa wenyewe, na miliki ya ardhi ya Warusi isawazishwe na ile ya wenyeji wa huko. Wakati huo huo, alisema, yapasa wakulima washirikishwe kwa bidii katika shughuli za wendeshaji na katika mambo yote ya huko.

Kama matokeo ya sera sahihi iliyoendeshwa na Chama kuhusu suala la wakulima, wakati wa Vita vya Nchini wakulima waliendea upande wa utawala wa Kisovieti, ijapokuwa iliwabidi wawapatie nafaka wafanyakazi pasina kupata hata kile kilicho cha lazima kabisa kutoka kwao. Karibu na mwishoni mwa 1919, wakimbizi wakaanza kurejea katika Jeshi Jekundu (Jeshi la Kimapinduzi). Wakulima wa Ukraina na sehemu nyinginezo wakaanza kushiriki kwa shime zaidi katika mapambano kwanza dhidi ya Denikin, na baadaye dhidi ya Vrangel *. Katika Desemba 1919, Lenin aliweza kusema kwa uhakika kabisa: "Tumeshafaulu kuwavutia wakulima upande wetu, tumethibitisha kimatendo kwa uzoefu wa mitihani mikali sana, kwa kupitia shida zisizo na kifani kwamba sisi, tukiwa kama wawakilishi wa tabaka la wafanyakazi, twaweza kuwapa wakulima uongozi bora na wa kufana zaidi kuliko chama cho chote kile kingine kiwezavyo kufanya".

Wakulima wa sehemu za pembezoni zikaliwa-

---

* *Vrangel*–jemadari wa jeshi la mfalme, mmojawapo wa wapigaji njama ya kupinga mapinduzi Kusini mwa Urusi katika 1918–1920.–*Mhariri.*

zo na mataifa madogo walijumuika kwa wingi zaidi kufuata uongozi wa tabaka la wafanyakazi la Urusi. Katika kipindi hicho, Lenin alitilia mkazo hasa umuhimu mkubwa sana wa kuelimisha kwa umma wa wakulima, kwa ujumuikaji wake chini ya uongozi wa utawala wa Kisovieti na mfano mwema ajabu uliotolewa na tabaka la wafanyakazi la Urusi katika mapambano yake ya kujisabilia kabisa dhidi ya wapinga mapinduzi na kuwania maslahi ya umma wa wananchi wafanyao kazi.

Alibainisha kwamba "...nguvu ya *ushirikiano maoni* wa wafanyakazi na wakulima kwa jeshi lao la mbele imethibitisha *nafsi yake* kuwa na uwezo wa *kufanya miujiza*". Lenin alisema, ushurutishaji hauwezi kufanya cho chote katika upande huu; kinachohitajika hasa ni matengenezo na hadhi ya moyoni.

Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Tisa wa Chama yaliliita tabaka la wafanyakazi lifanye matengenezo ya hali ya juu kabisa, nidhamu na kujitolea mhanga, jambo ambalo halina budi kusaidia kuwajumuisha hata zaidi wakulima watumiao jasho lao kufuata uongozi wa tabaka la wafanyakazi kama nguvu ya taathira ya moyoni.

Kazi iliyoendeshwa na Chama katika kutengeneza utaratibu wa kusaidiana kwa mataifa wakati wa Vita vya Nchini ilifanya mengi sana ili kukuza imani kwa Warusi miongoni mwa mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo zamani. Ukraina, iliyokombolewa karibuni kutokana na majeshi ya uvamizi, ilikuwa ikihitajia fedha na wataalamu wenye ujuzi mwingi kwa ajili ya kuu-

fufua uchumi ulioteketezwa na vita na kuunda chombo cha utawala wa Kisovieti. Urusi ya Kati ilikuwa na uhitaji mkubwa sana wa chakula.

Mnamo mwanzoni mwa 1919 JKKSU iliipa Jamhuri ya Ukraina mikopo ya kufufua viwanda na uchukuzi.

Tarehe 17 Aprili, 1919, Lenin aliwahutubia wafanyakazi wa Petrograd kwa niaba ya ndugu wa Ukraina, akiwaita kupeleka watu wengi zaidi huko Ukraina kwenda kusaidia kukijenga chombo cha utawala wa Kisovieti. Kwa upande mwingine, aliwaomba wafanyakazi na wakulima wa Ukraina kuisaidia mikoa ya kati ya Urusi kwa ngano. Wakati huo huo Lenin alifahamisha kwamba Ukraina haitoweza kuendelea endapo sehemu za Kaskazini zilizopigwa na njaa zikishindwa, na kwamba itaweza kuendelea kwa hakika kabisa endapo ikizisaidia sehemu za Kaskazini. Vikosi vinavyoshughulikia mambo ya chakula vyenye kuambata wafanyakazi kutoka mikoa ya kati ya Urusi viliendesha kampeni ya kutandaa sana ya kuwaelimisha wakulima wa Ukraina. Kwenye mkutano wa wafanyakazi wa huduma za reli katika Aprili 1919 Lenin alisema kwamba si chini ya wafanyakazi 3,000 wa reli yapasa wapelekwe katika sehemu hizi. Mnamo miezi ya mwanzoni na katikati ya 1918, pasina kujali hali mbaya sana ya chakula katika mikoa ya kati, serikali ilipeleka chakula huko Turkestan, ambako kulikuwa kukifanywa kazi ya kukifufua na kukistawisha kilimo cha pamba katika eneo la Turkestan. Serikali ilitoa dikrii ya kutenga kando fedha za kugharimia miradi ya mifereji ya kum-

wagilia maji mashambani, za kugharimia ustawishaji wa hekta laki tano za ardhi katika Mbuga za Njaa, za kugharimia ujenzi wa mifereji na mabwawa mapya ya kuhifadhia maji.

Kazi ya pande nyingi ya Chama cha Mabolsheviki iliufungulia njia muungano wa kijeshi wa jamhuri huru za Kisovieti. Uundwaji wake ulichapuliwa kwa shambulio la majeshi yaliyoungana ya wapinga mapinduzi.

Mabeberu walifanya muungano na wapinga mapinduzi wa kibwanyenye-kikabaila wa Kirusi na wengineo wanaopendelea kujibagua kitaifa. Na ingawa shambulio la kwanza la majeshi ya Uitifaki wa Madola (*Entente*) lilitokomezwa, hata hivyo wapinga mapinduzi walikuwa bado sana kumalizwa. Mnamo katikati ya mwaka 1919, Uitifaki wa Madola ulikuwa ukijitayarisha kwa kampeni mpya ya kuivamia nchi ya Kisovieti. Mabeberu waliyapatia majeshi ya wapinga mapinduzi kila kitu yalichokihitaji. Nchi ya Kisovieti ilijikuta imo katika hali ya hatari mno. Haja ya hima na ya lazima kabisa sasa ilikuwa ni kuyaunganisha majeshi yote na kuasisi muungano wa kijeshi wa jamhuri huru za Kisovieti.

Tarehe 18 Mei, 1919, Kamati Kuu ya Utendaji ya Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti ya Ukraina ilipitisha azimio juu ya haja ya lazima ya kuyaunganisha majeshi ya jamhuri za Kisovieti.

Tarehe 31 Mei, 1919, Baraza la Ulinzi la Lithuania na Byelorussia pia lilipendekeza muungano mkubwa zaidi wa kijeshi kati ya jamhuri za Kisovieti, kukiwa na uongozi wa pamoja kwa

majeshi yaliyoungana na kugawanywa kwao katika majeshi ya kutekeleza shabaha zinazohusika na matendo ya kivita, wala siyo kwa mujibu wa mgawanyiko wa kitaifa-kiserikali. Siku hiyo hiyo serikali ya Latvia ilitangaza msimamo wake wa kuunga mkono kikamilifu muungano wa kijeshi wa jamhuri hizo.

Tarehe 1 Juni, 1919, mapendekezo ya jamhuri hizo huru yalijadiliwa na Halmashauri ya Kisiasa ya Kamati Kuu ya CKU(Mab.), na kuamuliwa umbo la muungano huo.

Siku hiyo hiyo, kikao cha pamoja cha Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima na wawakilishi wa jamhuri hizo huru kilipitisha Dikrii ya Uunganishwaji wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti – Urusi, Ukraina, Latvia, Lithuania na Byelorussia – kwa ajili ya kupambana na ubeberu wa dunia. Dikrii hiyo ilikusudia paweko wendeshaji wa pamoja wa pande kuu za maisha katika jamhuri hizo, jambo ambalo lilimaanisha muungano huo ni zaidi kuliko kuwa wa kijeshi tu.

Muungano wa kijeshi-kisiasa si kama ulitosheleza maslahi ya jamhuri za Kisovieti zilizokuwako wakati ule tu, bali pia ulikuwa na taathira kubwa sana kwa mapambano ya wananchi wafanyao kazi dhidi ya serikali za kibwanyenye zipendeleazo kujibagua kitaifa ambazo zilinyakua madaraka katika sehemu fulani za nchini kwa msaada wa majeshi ya uvamizi ya kigeni. Ingawa Lenin alikuwa ameshughulika sana katika kutengeneza ulinzi wa nchi, hata hivyo alichungua hali ya mambo ilivyo katika kila jamhuri ya Kisovieti, na kujitahidi kuhakikisha kwamba uhusiano ba-

ina ya JKKSU na jamhuri nyingine unatosheleza siyo maslahi ya ulinzi ya pamoja tu, bali pia maslahi mahsusi na tabia za kipekee za kila taifa. *Muswada wa Azimio la KK ya CKU(Mab.) Kuhusu Utawala wa Kisovieti Katika Ukraina,* ambao uliandikwa na Lenin katika Novemba 1919, ukapitishwa na kikao kikamilifu cha Kamati Kuu ya CKU(Mab.), na kuthibitishwa na Mkutano wa Nane wa Urusi Nzima wa Chama, ulitilia mkazo kwamba Chama kitaendelea kujaribu kuanzisha fungamano za kishirikisho baina ya JKKSU na JKK ya Ukraina kwa kutegemea maazimio ya mwanzoni yaliyopitishwa na utawala wa Kisovieti, na kusisitiza haja ya kuondoa mapingamizi yote kwa ukuzwaji huru wa lugha na utamaduni wa Kiukraina, na kuzingatia jambo hilo kwamba nchi kandamizi ziliacha urithi wa mitindo ya kujibagua kitaifa miongoni mwa sehemu iliyozorota zaidi ya wakazi wa Ukraina. Wanachama wa CKU(Mab.) wanapaswa kuwa na hadhari sana wakati wa kukabiliana na mitokezo kama hiyo, na wajitahidi kupambana nayo kwa msaada wa maelezo ya kirafiki juu ya mlingano wa maslahi ya umma wa wananchi wafanyao kazi wa Ukraina na Urusi.

Ilivyokuwa wakazi wa kikulima walikuwa hata wengi zaidi katika Ukraina kuliko katika Urusi, azimio hilo lilisema kwamba yapasa Chama kifuate sera barabara kuhusiana na wakulima wa hali ya wastani, kihifadhi vilivyo maslahi yao katika sera yake ya chakula na ardhi kwa kuzingatia hali mahsusi za sehemu za vijijini za Ukraina, na kuwashirikisha wakulima masikini na wale wa

hali ya wastani kwa upeo mkubwa katika shughuli za wendeshaji na ujenzi wa usoshalisti.

Lenin aliona kwamba katika mapambano ya kuikomboa Ukraina kutokana na utawala wa mabwanyenye wapendeleao kujibagua kitaifa na waingilizi wa kigeni, ilikuwa ni lazima kupata kuungwa mkono na *Maborotba* *, ambao wakati ule walikuwa na taathira kubwa miongoni mwa wakulima. Ingawa msimamo wa Maborotba wa kupendelea kujibagua kitaifa ulikinza shughuli za Mabolsheviki, hata hivyo Lenin aliwashauri Wakomunisti wa Ukraina kuwashirikisha katika mapambano ya pamoja dhidi ya wapinga mapinduzi. Mbinu zenye kurekebishika upesi zilizotegemezwa juu ya maongozi ya Lenin zilifanya iwezekane kuzitumia kwa maslahi ya utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi chipukizi zote za kimapinduzi kikweli za chama hicho na sehemu ya wakulima wa Kiukraina walioko chini ya taathira yake.

Katika hali za shida sana za Vita vya Nchini na uingilizi wa kigeni, Chama cha Kikomunisti

---

* Wafuasi wa chama cha kibwanyenye uchwara kiteteacho kujibagua kitaifa cha Wasoshalisti-Wanamapinduzi wa mrengo wa Kushoto katika Ukraina, ambacho kiliitwa kwa jina la gazeti kuu la chama hicho *Borotba* (*Mapambano*). Chini ya athari ya mizani inayobadilika ya nguvu za kijamii, jukwaa la kisiasa la Maborotba liligeuka kutoka udemokrasi wa kibwanyenye mpaka kuja kulikubali jukwaa la Kisovieti. Katika Machi 1920, wafuasi wa mrengo wa Kushoto wa chama hicho walishikilia kujivunja wenyewe kwa chama hicho. Wawakilishi wake bora kabisa walikubaliwa (kwa kila mtu mmoja mbali) kujiunga na Chama cha Kikomunisti cha Mabolsheviki cha Ukraina.–*Mhariri.*

kiliendelea na kazi yake ya kutengeneza muundo wa kitaifa-kiserikali ambayo ilianza papo tu baada ya Mapinduzi ya Oktoba 1917.

Lenin aliielezea dikrii ya Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima kuhusu Muungano wa kijeshi-kisiasa baina ya jamhuri za Kisovieti kama ni mkataba ambao ulikusudia "shirikisho lenye kushikamana zaidi", kwani imethibitisha kwa hakika hasa uhusiano wa kushikamana uliokuwa tayari umeshaanzishwa baina ya jamhuri hizo. Katika Muswada wa Azimio la Halmashauri ya Kisiasa ya KK ya CKU(Mab.) *Kuhusu Majukumu ya CKU(Mab.) Katika Mitaa Inayokaliwa na Mataifa ya Mashariki* (Oktoba 1920), Lenin aliainisha haja ya kuendelea kutekeleza utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani – kwa maumbo yenye kufalia vizuri zaidi hali halisi za huko – kwa mataifa yale ya Mashariki ambayo hayana bado taasisi zao zenyewe za kujitawala kwa mambo ya ndani.

Kadiri sehemu yą nchi ilivyokuwa ikikombolewa kutokana na wavamizi wa kigeni na majeshi ya wapinga mapinduzi, ndivyo jamhuri hizo zilivyofufua na kukuza uhusiano wa muungano.

Katika Aprili 1919, tume mahsusi iliundwa kwa kuandalia ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Kirghizia Nzima ili kutangaza Jamhuri Ijitawalayo Yenyewe Kwa Mambo ya Ndani ya Kirghizia (Kazakhstan), na tarehe 26 Agosti, 1920 kulipitishwa dikrii ya kuundwa kwa jamhuri hiyo *.

---

* Kwa hakika hasa, Jamhuri Ijitawalayo Yenyewe kwa Mambo ya Ndani ya Kirghizia (Kazakhstan) iliundwa kati-

Mnamo katikati ya 1919, kulianza kazi ya kuunda majimbo yajitawalayo yenyewe kwa mambo ya ndani ya Mari na Votyak (sasa Udmurtia).

Katika Januari 1920 kulianzishwa kazi ya maandalio ya kuunda serikali yenye kujitawala yenyewe kwa mambo ya ndani ya Turkestan.

Katika Februari 1920, kwa sababu ya ukombozi wa maeneo yaliyoko pembezoni mwa Mto Volga, Ural, Siberia, Asia ya Kati na Turkestan, na ukombozi unaokaribia wa Crimea na Kaukasi ya Kaskazini, Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima ilipitisha azimio la kuunda tume ya kufafanua masuala yanayohusiana na utaratibu wa shirikisho wa JKKSU. Katika Juni 1920, Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima ilipitisha sheria ya Kuundwa kwa Jimbo la Chuvash Lijitawalalo Lenyewe kwa Mambo ya Ndani na Komyuni ya Kazi ya Karelia (ambayo mnamo 1923 ilikuwa ni Jamhuri Ijitawalayo Yenyewe kwa Mambo ya Ndani ya Karelia). Kuliundwa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti Zijitawalazo Zenyewe kwa Mambo ya Ndani za Daghestan na Milimani. Tarehe 1 Januari, 1920 kulitolewa Ilani yenye kutangaza kuundwa kwa Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti ya Byelorussia.

Kwa hivyo basi, karibu na mwishoni mwa Vita vya Nchini, Chama kilikuwa kimeshafanya mengi katika upande wa kutengeneza muundo wa kitaifa-kiserikali. Uundwaji wa jamhuri huru za

---

ka Oktoba 1920. Mnamo Aprili 1925 iliitwa kama Jamhuri Ijitawalayo Yenyewe kwa Mambo ya Ndani ya Kazakhstan. Katika 1936 iligeuzwa kuwa jamhuri ya Muungano – Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti ya Kazakhstan.– *Mhariri.*

Kisovieti za kitaifa iliyanyima majeshi ya wapinga mapinduzi na wavamizi wa kigeni fursa ya kujitokeza kama "wakombozi" wa mataifa ya Urusi yaliyokuwa yakikandamizwa hapo zamani, ukiwakosesha uwanja wa kusimamia katika sehemu za pembezoni mwa Urusi zikaliwazo na mataifa madogo. Sera ya Chama cha Kikomunisti, iliyokusudiwa kuleta muungano wa kimataifa wa tabaka la wafanyakazi, ilidhaminia umadhubuti wa sehemu ya nyuma ya mpakani kwa Jeshi Jekundu, ilisaidia kuyafisha moyo majeshi ya kibeberu na ya wapinga mapinduzi, na kuwajumuisha pamoja wazalendo wote kwa ulinzi wa nchi yao ya jadi ya kisoshalisti. Baada ya kwisha kuonja sera ya kiserikali ya wavamizi na ya mabwanyenye wapendeleao kujibagua kitaifa, mataifa yote yalilipokea Jeshi Jekundu, lililoadilishwa kwa ari ya umoja wa kimataifa, kama mkombozi wao.

Uhusiano wa Ki-mkataba

Karibu na mwishoni mwa Vita vya Nchini, uhusiano wa ki-mkataba ulikuwa tayari umeshaanzishwa baina ya jamhuri huru za Kisovieti. Katika 1920, JKKSU ilitiliana saini mikataba na jamhuri za Khorezm, Azerbaijan na Ukraina, na katika 1921, na jamhuri za Byelorussia, Bukhara, Georgia na Armenia. Kwa mujibu wa mikataba hiyo, muungano wa kijeshi na wa kiuchumi ulianzishwa baina ya JKKSU na jamhuri huru za Kisovieti. Mikataba iliyotiwa saini baina ya JKKSU na jamhuri za Watu wa Bukhara na

Khorezm, ambako mpaka wakati huo kulikuwa kumetukia mapinduzi ya kupinga umwinyi na ya kidemokrasi tu, ilipembulika kwa tabia fulani mahsusi. Kama mikataba hiyo ilivyotilia mkazo, jamhuri hizo zisingeweza kwendea katika njia ya mageuzi ya kisoshalisti isipokuwa kwa msaada wa JKKSU tu na jamhuri nyingine za Kisovieti.

Ilikuwa ni wakati wa kutukia kwa Vita vya Nchini ndipo jamhuri hizo zilipotambua haja ya kuwa na uhusiano kama huo, na papo tu sehemu zao zilipokombolewa kutokana na wapinga mapinduzi wa ndani na wa nje, zilianza kufanya mazungumzo kwa madhumuni ya kutia saini mikataba hiyo.

Chama cha Kikomunisti cha Ukraina kilikuwa miongoni mwa vile vya mwanzo kupendekeza fungamano kubwa zaidi baina ya JKKSU na JKK ya Ukraina. Takriban mnamo wakati ule ule, Mkutano Mkuu wa Pili wa Byelorussia Nzima wa Masovieti ulipendelea muungano imara zaidi baina ya mataifa ya Urusi na mengineyo.

Maudhui ya mikataba hiyo yaonyesha kwamba iliwakilisha usongaji mbele zaidi katika kuzijongeza karibu jamhuri hizo huru kwa kuunganisha siyo nguvu zao za kijeshi tu, bali pia pande kuu za mambo ya kiuchumi.

Katika mwenendo huu, mamlaka ya jamhuri mbalimbali hayakuathirika. Kinyume chake, mikataba hii ilielezea kwamba pasina kujali hilo jambo kwamba maeneo ya jamhuri hizo huru yalikuwa hapo awali chini ya mamlaka ya Urusi, jamhuri hizi hazina mawajibiko kwa ye yote. Jambo hili lilitilia mkazo tabia ya kujitolea ya

muungano huo. Mawajibiko ya jamhuri hizo yalichukuliwa kwa hiari na kutokana na maslahi ya pamoja. Mikataba hiyo ilitia maanani kama inavyostahiki maslahi ya kidiplomasia na ya kibiashara ya kila moja kati ya jamhuri hizo. Ilitokeza tabia mahsusi za kila jamhuri, na hiyo ndiyo sababu kwa nini maudhui yao yakatofautiana kidogo.

Lenin alidai kuheshimu kama ipasavyo mamlaka ya jamhuri zinazoanzisha uhusiano wa ki-mkataba. Mathalan, wakati nchi ilipokuwa ikigawanywa katika majimbo ya kiuchumi mnamo 1922, Tume ya Taifa ya Upangaji ilipendekeza kwamba Ukraina igawanywe katika majimbo mawili ya kiuchumi, na kwamba Kaukasi ya Kaskazini iunganishwe na Transcaucasia. Jamhuri hizo, hasa Ukraina, ziliupinga mpango huo. Lenin aliuchungua ubishani uliotolewa kuhusu mamlaka ya jamhuri hizo na, kwa pendekezo lake, Kamati Kuu ya CKU(Mab.) ilitoa elekezo la kuusahihisha mpango huo wa ugawanyaji wa majimbo kwa mujibu wa vyombo vya Chama na vya Kisovieti (vya kiserikali) vya Ukraina. Vivyo hivyo iliamuliwa kutoiunganisha Transcaucasia na Kaukasi ya Kaskazini.

Wakati wa Vita vya Nchini, Chama kiliendesha sera ya ukomunisti wa kivita, kikikusanyisha pamoja kikamilifu uongozi wa uzalishaji mali na ugawaji na kutumia akiba na nguvu zote kwa ajili ya ulinzi wa nchi. Tabaka la wafanyakazi lililazimika kutwaa kutoka kwa wakulima ziada zao za chakula (na baadhi ya wakati hata zaidi kuliko ziada tu) ili kuuokoa utawala wa Kisovieti.

Wakulima walitambua kwamba mihanga hii haiepukiki, kwani ama sivyo wangeweza kupoteza matunda yote ya mapinduzi.

Kama matokeo ya miaka saba ya vita – vya kibeberu na vya nchini – uchumi wa taifa ulikuwa umeanguka vibaya sana. Shughuli za viwanda na uchukuzi zilikuwa zimeharibiwa kabisa, na uzalishaji wa kilimo ulikuwa umepungua sana kufika hadi ya kuhatarisha kuleta maafa makuu. Mchafuko wa uchumi wa kikulima, ambao ulizidi kuwa ahasi kwa ukosefu wa mavuno wa mwaka 1920, uliwahilikisha wakulima kwa hali ya shida kubwa mno, kadhalika ulikuwa ni pingamizi kubwa katika ufufuaji wa viwanda na uchukuzi, na kupelekea kuzuka mgogoro baina ya tabaka la wafanyakazi na wakulima.

Shida za kiuchumi zilileta pamoja nazo mitataniko mikubwa ya kisiasa. Mabwanyenye ambao walishindwa wakati wa Vita vya Nchini, na mabaki ya vyama vipingavyo mapinduzi walilitumia dukuduku la wakulima, na kujaribu kuwachochelea wawapinge wafanyakazi, kuuvunja muungano wao ambao ndio msingi wa utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi. Katika sehemu fulani fulani, wapinga mapinduzi walifaulu kuwachochelea wakulima kufanya uasi.

Lenin alithibitisha uhitajiko wa kufanya ukiukaji kutoka sera ya ukomunisti wa vita – ambayo imekuwa ni pingamizi kwa maendeleo ya nguvu za uzalishaji mali – kwendea katika sera mpya ya uchumi (SMU). Madhumuni yake yalikuwa ni kumpatia mtu anayezalisha mali kwa upeo mdogo hali kama zile ambazo zingesaidia kwa kiasi

kikubwa zaidi maendeleo ya nguvu za uzalishaji mali katika kilimo na ufufuliwaji wa viwanda, na jambo hili lisingeweza kufanywa isipokuwa kwa ukiukaji tu kutoka utaratibu wa kutwaa ziada ya chakula kwendea katika ule wa kodi ya mazao, ambapo mkulima mwenye kijishamba kidogo ataweza kupanga uzalishaji mali wake mapema na kuamua ukubwa wake kwa mujibu wa kodi atakayotozwa.

Kuruhusiwa kwa biashara isiyo na vikwazo, bila ya shaka, kulihuisha chipukizi za kibepari. Lakini madhali hatamu za kuongoza uchumi zilibakia mikononi mwa tabaka la wafanyakazi, serikali ilikuwa siku zote ina uwezo wa kutekeleza jukumu lake la kuratibisha. Sera mpya ya uchumi ilikusudiwa kusaidia kuushinda uharibifu wa uchumi na njaa, kustawisha viwanda vikubwa, kuweka fungamano za kiuchumi baina ya miji na vijiji, kuimarisha muungano wa wafanyakazi na wakulima, kuzipunguza na kuzing'oa chipukizi za kibepari, na kuleta ushindi wa usoshalisti.

Sera mpya ya uchumi iliyotungwa na Lenin na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.) katika 1921, ilisaidia kuimarisha urafiki baina ya mataifa ya nchi ya Kisovieti. Azimio *Juu ya Majukumu ya Papo ya Chama katika Suala la Mataifa* lililopitishwa na Mkutano Mkuu wa Kumi lilisema kwamba kiburi cha utaifa na uhasama baina ya mataifa hauepukiki madhali wakulima wenye fikira fupi za kitaifa (na vibwanyenye uchwara kwa jumla, kwanza kabisa wale wa mataifa yanayotawala) wakiendelea ku-

wafuata mabwanyenye, na kwamba, kinyume chake, amani ya taifa na uhuru wa taifa waweza kuhesabiwa kuwa umeshadhaminiwa hasa endapo wakulima wakilifuata tabaka la wafanyakazi, yaani, chini ya utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi.

Sera mpya ya uchumi ilisaidia kuunda msingi madhubuti wa kiuchumi kwa muungano wa tabaka la wafanyakazi siyo na wakulima wa Urusi tu, bali pia na wale wa sehemu za pembezoni mwake zikaliwazo na mataifa madogo. Ingawa wakulima wa Ukraina, Kaukasi, na sehemu nyinginezo za pembezoni mwa nchi hii hawakukutwa na shida na njaa kubwa kama ile iliyowabana wakulima wa Urusi ya Kati, hata hivyo serikali ililazimika kutwaa chakula kutoka kwao vile vile pasina kuwapatia bidhaa zo zote za viwandani kama malipo yao.

Lenin aliwashauri wakuu wa serikali za mitaa kuzingatia vilivyo hali mahsusi za kila sehemu ya pembezoni mwa nchi ikaliwayo na taifa dogo katika kutekeleza sera mpya ya uchumi. Kwenye Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.), alionya kutoigiza kipofu huko Ukraina na sehemu nyinginezo za mataifa madogo sera iliyokuwa ikifuatwa na serikali katika Urusi ya Kati.

Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.) kuhusu madaraka na majukumu ya vyama vya wafanyakazi na umoja wa Chama yalikuwa na umuhimu mkuu katika kuimarisha muungano wa wafanyakazi na wakulima, kuyajumuisha mataifa yaliyoko pembezoni mwa nchi yalifuate tabaka la wafanyakazi la Urusi, na kuzi-

disha jukumu la uongozi la tabaka la wafanyakazi katika mwendo huo. Wakati wa ukiukaji kwendea katika utaratibu wa sera mpya ya uchumi, Chama kilitoa juhudi kubwa kulielimisha tabaka la wafanyakazi na ushikamano wake, kadhalika juhudi za kuwania umoja wa chama chenyewe kilichounganisha wawakilishi wa mataifa mbalimbali pia zilisaidia kuleta umoja katika kufuata sera barabara ya uhusiano wa mataifa.

Ushindi uliopatikana katika Vita vya Nchini haukuondosha uwezekano, bali kinyume chake, ulikusudia kufanywa majaribio mengine zaidi kwa upande wa mabeberu kutaka kuuangamiza mfumo wa Kisovieti. Hiyo ndiyo maana kwa nini papo tu Vita vya Nchini vilipomalizika, ilikuwa ni muhimu kabisa kuendelea kuimarisha fungamano za kishirikisho baina ya jamhuri hizo na kuunda dola lililotangamana la mataifa mengi. Ilikuwa ni lazima kuimarisha na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kuyaunganisha mataifa yote ya nchi ya Kisovieti kwa ajili ya kuustawisha zaidi mfumo wa Kisovieti.

Katika kipindi hicho, Lenin alifichua sababu zilizozipelekea jamhuri za Kisovieti kujongeleana karibu, na kuthibitisha haja ya kuwa na dola la Kisovieti lililotangamana la mataifa mengi.

Muungano wa jamhuri hizo ulihitajika kwanza kabisa kwa madhumuni ya ulinzi. Ilibidi dola la Kisovieti kuwa tayari kuyajibiza mashambulio yo yote mengine ya ubeberu. Kwa hivyo basi, Lenin aliita kuwa macho daima wakati wa ujenzi wa amani, pia kufanya jitihada zisizochoka za kudhaminia uwezo wa kujihami wa nchi hii. Alian-

dika katika 1920: "...Chini ya hali za sasa za kimataifa hakuna uokozi wo wote kwa mataifa mategemezi na dhaifu isipokuwa kwa muungano wa jamhuri za Kisovieti".

Kwenye Mkutano Mkuu wa Tisa wa Urusi Nzima wa Masovieti katika Desemba 1921, jamhuri huru za Ukraina, Georgia, Armenia, Azerbaijan na Byelorussia zilitoa taarifa ya pamoja yenye kuelezea maoni yao ya kauli moja kuhusu haja ya kuchukua hatua halani za kuzidisha uwezo wa kupigana wa Jeshi Jekundu.

Jamhuri huru za Kisovieti zilihitaji kujongeleana karibu zaidi kwa sababu ilibidi zitende kwa pamoja kwenye uwanja wa kimataifa.

Ubeberu wa kimataifa ulijitahidi kutaka kulikaba dola la Kisovieti kwa mzingio wa kiuchumi na kuitenga kidiplomasia. Huku nyuma, sera ya Lenin ya urafiki na usawa baina ya mataifa yote iliweza kuzivutia upande wa dola la Kisovieti baadhi ya nchi za kibepari zenye kukandamizwa na madola makuu ya kibeberu, na hasa nchi za jirani. Isitoshe, maslahi ya uchumi wa dunia na uhusiano mpya wa kimataifa ulioanzishwa na Mkataba wa Amani wa Versailles yalizilazimisha nchi nyingi kubwa za kibepari kuwa na fungamano za kiuchumi na nchi ya Kisovieti.

Mipango ya kufufua na kustawisha uchumi wa taifa na mpango wa serikali uliotungwa na Lenin wa kusambaza umeme nchini kote Urusi (GOELRO) ilihitajia fedha nyingi sana.

Wakati walipokuwa wakianzisha uhusiano wa kiuchumi na nchi ya Kisovieti, mabeberu walijaribu kuzitumia jamhuri huru za Kisovieti kwa

matilaba yao wenyewe. Mathalan, walijaribu kuanzisha uhusiano mbali na Georgia, Ukraina, n. k. Jambo hilo lilifanya ihitajike kuweko umoja wa jamhuri za Kisovieti katika upande wa diplomasia.

Haja ya kuwa na umoja katika mambo ya kidiplomasia ilidhihirika wazo papo tu baada ya Vita vya Nchini, wakati wawakilishi wa Uturuki, katika mazungumzo yao na wawakilishi wa jamhuri za Transcaucasia katika Aprili 1921, walijaribu kuwafarakisha na kwa hivyo kupata faida zaidi.

Sababu muhimu kabisa iliyozifanya jamhuri hizo za Kisovieti kuwania muungano mkubwa zaidi ilikuwa ni mahitaji ya kiuchumi ya nchini. Baada ya miaka saba ya vita, uchumi ulikuwa umeharibika kabisa, na njia ya kuufufua ilikuwa ni kuchanganyisha akiba na nguvu za mataifa yote, kuutumia kwa busara mgawanyo wao wa kazi wa kimaumbile, uliozuka kihistoria baina ya majimbo mbalimbali, na kuendesha njia zote za mawasiliano kwa mpango wa pamoja.

Katika ripoti yake kwa Mkutano Mkuu wa Nane wa Urusi Nzima wa Masovieti, Lenin alitilia mkazo kwa nguvu haja ya kuunda akiba ya chakula kama msingi wa uchumi, kama akiba ya kufufua viwanda na kuwasaidia wakulima. Na akiba kama hiyo haiwezi kuanzishwa isipokuwa kwa kushirikiana pamoja tu na Ukraina, Kaukasi na jamhuri nyingine za kitaifa.

Ilikuwa ni muhali vile vile kuanza kufufua viwanda bila ya hatabu, ambayo yapatikana kwa wingi zaidi huko Ukraina na Transcaucasia. Lenin alisema kwamba makaa ya Donbass na mafu-

ta ya Baku yalikuwa ndicho chanzo cha pili kikuu cha kiuchumi katika kufufua viwanda na kuanzisha uhusiano barabara baina ya wafanyakazi na wakulima.

Lakini ilikuwa si jambo la shida za kiuchumi za muda tu zinazotokana na vita vya kibeberu na vile vya nchini. Shida hizi zilifanya ihisike kwa nguvu zaidi tu haja ya jamhuri zote kuunganisha jitihada zao. Ujenzi wa usoshalisti kwa jumla ulihitajia kukusanyisha pamoja akiba na nguvu zote za nchini, ambazo zingefanya iyumkinike kuzitumia vilivyo fursa za upangaji wa kiuchumi. Kulikuwa na akiba nyingi ya mawe ya madini huko Ural, makaa huko Siberia ya Magharibi, mafuta huko Kaukasi, kadhalika kulikuwa na miti mingi, akiba za maji, malighafi kwa viwanda vya kemikali, na maliasili nyinginezo chungu nzima huko Siberia na majimbo mengineyo. Lenin alitilia mkazo kwamba utengenezaji wa maliasili hizi kwa msaada wa mbinu za kisasa utafagilia njia kwa usongaji mbele usio na kifani wa nguvu za uzalishaji mali.

Haja ya kuwa na muungano mkubwa zaidi wa kiuchumi kati ya jamhuri za Kisovieti ilitokana na fungamano za kiuchumi zilizopatikana kihistoria, ushughulikiaji wa upande maalumu wa uzalishaji mali katika majimbo mbalimbali, na madai ya kufanywa mgawanyo mpya wa kazi kati ya jamhuri za kitaifa ambao ungeondosha dosari za maendeleo yanayohusika na upande mmoja tu wa uchumi na ya utegemezi ya sehemu za pembezoni mwa nchi zikaliwazo na mataifa madogo.

Katika "Utungo wa Mwanzoni wa Tasnifu Kuhusu Masuala ya Mataifa na Ukoloni", Lenin aliandika kwamba haja ya kuwa na uchumi wenye kupangwa uliotangamana ilikuwa ni mojawapo ya sababu kuu zinazohimiza kufanywa shirikisho la ushikamano mkubwa zaidi. Aliainisha kwamba mwelekeo wa kuchomoza kwa uchumi uliotangamana wenye kuratibishwa kwa mpango wa pamoja, ambao tayari waonekana chini ya ubepari, hauna budi kuendelezwa na kukamilishwa chini ya usoshalisti.

Lenin aliainisha pia kwamba bila ya muungano wa kiuchumi wa kushikamana zaidi wa jamhuri za Kisovieti itakuwa ni muhali kuinua hali za maisha ya watu wafanyao kazi nchini kote.

Kwa hivyo basi hali ya mambo ya ndani na ya nje ilifanya ihitajike kuwako uhusiano wa kushikamana zaidi kati ya jamhuri huru za Kisovieti. Haja hii yatokana na tabia yenyewe hasa ya uchumi wa kisoshalisti, wenye kutegemezwa juu ya miliki ya kijamii ya nyenzo za uzalishaji mali, na pia tabia ya umoja wa kimataifa ya utawala wa Kisovieti.

Hoja zilizotolewa na Lenin kupendelea muungano wa kushikamana zaidi wa Jamhuri za Kisovieti zilikuwa ndio msingi wa kifungu kinachohusika cha azimio lililopitishwa na Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.). Katika waraka huo, suala kuhusu umbo la muungano wa jamhuri huru za Kisovieti lilikuwa tayari limeshatolewa kimatendo.

Uwekwaji wa uhusiano wa ki-mkataba baina ya jamhuri za Kisovieti ulisaidia kupanua na ku-

kuza fungamano zao za kiuchumi na kuendeleza nguvu zao za uzalishaji mali. Ukusanywaji pamoja wa biashara ya nje, utaratibu wa sarafu za kigeni na mfumo wa aina moja wa kufunza makada iliziwezesha jamhuri hizo kuweka mkazo wa jitihada zao juu ya sekta muhimu kabisa za uchumi wa taifa.

Uendelezwaji wa uhusiano wa ki-mkataba baina ya jamhuri hizo ulikuwa ni awamu muhimu sana ya usongaji mbele kuelekea katika muungano wao. Lakini maisha yenyewe punde yalionyesha kwamba uhusiano wa ki-mkataba ulikuwa hautoshi kwa ufufuaji chapuchapu na uendelezwaji wa uchumi kwa upeo wa nchi nzima. Ilianza kudhihirika wazi kwamba mambo ya kisiasa na ya kiuchumi ya jamhuri zote za Kisovieti hayakuwa na budi kuendeshwa chini ya uongozi mmoja kamili zaidi, na hayo yasingeweza kufanywa vingine isipokuwa kwa uundwaji wa vyombo vya kudumu tu vya shirikisho vyenye kupewa madaraka kamili ya kiserikali kwenye maeneo ya jamhuri zote. Uhusiano wa ki-mkataba, kwa mfano, haukufafanua uhusiano wa kifedha baina ya jamhuri zote za Kisovieti, wala haukuzingatia uunganishwaji wa idara zote za upangaji za nchi ni; wendeshaji wa uchumi wa ufanisi ulikuwa mara nyingi ukikinzwa na shida zilizokuwako katika uratibishaji na utanzuaji wa matatizo mbalimbali ya kimatendo.

Wale waliopendelea kujibagua kitaifa miongoni mwa wakazi wa kienyeji waliuchukulia fursa ukosekano wa utaratibu wa pamoja wa sheria ili kudhoofisha fungamano za kishirikisho kati ya

jamhuri za Kisovieti na kuuharibu uhusiano wa ki-mkataba.

Wakati huo huo, utaratibu uliokuwako ambapo vyombo vya ngazi za juu kabisa vya JKKSU mara nyingi vilitekeleza shughuli za shirikisho zima ulisababisha mzozano na kuwapa kisingizio wale wanaopendelea kujibagua kitaifa ili kuusengenya utaratibu huo.

Muungano wa Kidiplomasia

Uhusiano wa ki-mkataba ulikuja kudhihirika kuwa hautoshi kwa kutekeleza majukumu ya pamoja yenye kuyakabili mataifa yote ya nchini, hasa wakati wa mikutano ya Genoa na Hague katika 1922, kwa sababu mikataba hiyo haikuzingatia uunganishwaji wa shughuli zinazohusika na siasa za nje za jamhuri huru za Kisovieti. Kwenye mkutano wa kiuchumi wa Ulaya, madola ya kibeberu yaliazimia kulishinikiza kwa pamoja dola la Kisovieti ili kulifanya lirudi nyuma. Mabeberu walizichukulia fursa shida za kiuchumi za nchi ya Kisovieti na huko kuwako kwa jamhuri huru kadhaa kwenye eneo la nchi hiyo. Jamhuri huru zote za Kisovieti zilialikwa kwenye Mkutano huo uliokusudiwa kuitishwa mjini Genoa kama madola yenye mamlaka yao yenyewe ya kiserikali.

Katika ripoti yake kwenye Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja wa CKU(Mab.), Lenin aliwaambia wajumbe juu ya maelekezo ya kinaganaga yaliyofafanuliwa na Kamati Kuu kwa wanabalozi

wa Kisovieti mjini Genoa, ambao shabaha yao huko ilikuwa ni kupata upanuliwaji wa fungamano za kibiashara za Kisovieti na nchi za kibepari.

Lenin aliona kwamba endapo kila moja kati ya jamhuri huru za Kisovieti ikipeleka ujumbe wake kwenye mkutano huo, basi hiyo ingekuwa ni kwa manufaa ya mabeberu, ambao walitaka kuzifarakisha jamhuri za Kisovieti.

Mnamo wakati huo, JKKSU ilikuwa tayari imeshawahi mara kadha wa kadha kuziwakilisha jamhuri nyingine. Mathalan, katika kutia saini mkataba wa amani na Poland huko Riga mnamo Machi 1921, serikali za JKKSU na JKK ya Ukraina ziliteua ujumbe wa pamoja, na Serikali ya JKK ya Byelorussia iliupa idhini ujumbe huo kuwakilisha maslahi ya Byelorussia vile vile. Kwa mujibu wa mapatano yaliyofikiliwa baina ya JKKSU na Ujerumani (19 Aprili, 1921) juu ya kurejesheana mahabusi wa kivita na raia waliowekwa kizuizini, ilikuwa si raia wa JKKSU tu, bali pia wale wa jamhuri zote nyingine za Kisovieti ndio waliokusudiwa kurejeshwa. Kwa mujibu wa Mkataba wa Moscow uliotiwa saini pamoja na Uturuki tarehe 16 Machi, 1921, Uturuki pia iliahidi kuweka sawa uhusiano wake na jamhuri za Transcaucasia. Kwa msaada wa JKKSU, mikataba ilitiwa saini baina ya JKK ya Ukraina na serikali za kibwanyenye za Lithuania na Latvia, mapatano ya kibiashara ya muda baina ya JKK ya Ukraina na Chekoslovakia, na baina ya JKKSU na JKK ya Ukraina, kwa upande mmoja, na Austria, kwa upande mwingine. Genoa ilikuwa iwe ndio mtihani mkali kabisa.

Tarehe 20 Januari, 1922 Halmashauri ya Kisiasa ya KK ya CKU(Mab.) ilithibitisha uhitajiko wa kupeleka ujumbe wa pamoja wa kidiplomasia wa jamhuri zote za Kisovieti katika Mkutano wa Genoa. Tarehe 27 Januari, kikao mahsusi cha Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima iliamua orodha ya wajumbe watakaokwenda Genoa. Lenin, ambaye aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wake, alisimamia matayarisho ya mkutano huo, na pia alitoa maelekezo kwa kazi yote ya ujumbe wa Kisovieti huko Genoa.

Tarehe 22 Februari, 1922, palitiwa saini mapatano ambayo kwa mujibu wake Azerbaijan, Armenia, Byelorussia, Bukhara, Georgia, Jamhuri ya Mashariki ya Mbali, Ukraina na Khorezm ziliipa idhini JKKSU kuziwakilisha jamhuri zao kwenye Mkutano wa Genoa na kutia saini kwa niaba yao mikataba na mapatano na nchi zo zote.

Akiipokea hati hiyo, Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima (Rais) M. I. Kalinin, ambaye aliiwakilisha JKKSU, alisema kwamba serikali ya Jamhuri ya Urusi itafanya ukomo wa uwezo wake kwenye mkutano huo ili kutetea kama ipasavyo maslahi ya madola yote ambayo imehusiana nayo kwa fungamano zisizokatika, za kidugu na za muungano. Itaangalia kwa makini kwamba ujumbe uliotolewa na Jamhuri ya Urusi kuiwakilisha Urusi na waitifaki wake kwenye Mkutano wa Ulaya unatetea barabara maslahi yao na kuziarifu kinagaubaga serikali za muungano na za kidugu juu ya matukio yote ya mkutanoni. Jambo muhimu la kuzingatia hapa

ni kwamba ujumbe wa JKKSU ulikuwa na wawakilishi wa jamhuri za kitaifa.

Mbinu zilizotumiwa na Lenin wakati wa mikutano ya Genoa na Hague zilijihalalisha kikamilifu. Ujumbe wa Kisovieti huko Genoa ulitetea vilivyo maslahi ya jamhuri za Kisovieti. Ulizitumia tofauti za uhasama baina ya nchi za kibepari na kwa kutia saini mapatano ya kibiashara na Ujerumani, ulileta mfarakano katika msimamo wa pamoja wa madola ya kibepari.

Kwa hivyo basi, uzoefu wa kutenda kwa pamoja kwa upande wa jamhuri zote za Kisovieti kwenye uwanja wa kimataifa uliihizi mipango ya kibeberu na kufungua njia kwa fungamano za kiuchumi za kutandaa zaidi na nchi nyingine.

Akizingatia uzoefu wa Genoa, Lenin alisema kwenye kikao cha Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima wakati alipokuwa akifafanua majukumu yanayoukabili ujumbe ambao ulikuwa punde uondoke kwenda kwenye Mkutano wa Lausanne: "Nina hakika kwamba huko, pia, wanabalozi wetu hawatatuaibisha, na kwamba tutaweza kuyatetea maslahi ya jamhuri zetu zote za shirikisho pamoja na yale ya JKKSU."

Bila ya shaka, hilo jambo kwamba jamhuri moja iliziwakilisha zote nyingine lilikuwa rasmi ni utengano na utaratibu wa shirikisho "safi", uvunjaji kwa kiasi fulani wa usawa kamili, lakini wakati ule lilishurutishwa na hali ya kimataifa.

Mpango wa Lenin wa umoja wa kidiplomasia wa kushikamana ulikuwa uonyeshe papo tu baada ya vita kumalizika haja ya kuziunganisha zaidi jamhuri hizo. Kwa maana hii, msimamo wa

pamoja uliochukuliwa na jamhuri hizo kwenye Mkutano wa Genoa ulikuwa ni mtokezo mwingine zaidi wa imani ya dhati ya mataifa yaliyokuwa yakikandamizwa hapo kabla kwa Warusi, ambayo ilipelekea kuchapua mwendo wa matayarisho ya muungano wa jamhuri huru katika dola la Kisovieti lililotangamana.

Uundwaji wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti

Miaka miwili ya uhusiano wa ki-mkataba ilithibitisha uhitajiko wa kwendea katika daraja ya juu zaidi ya uhusiano wa kiserikali kwa upeo wa nchi nzima. Jamhuri ya Ukraina ilipendekeza kwamba jamhuri huru za Kisovieti zianze kushughulikia kimatendo suala la uunganishwaji wao kwa madhumuni ya kuunda dola moja la muungano.

Kikao kikamilifu cha Kamati ya Eneo la Transcaucasia ya CKU(Mab.) katika Julai 1922 kiliwaagiza wajumbe wake waliokuwa wakienda Moscow kuwasilisha suala la uhusiano baina ya Shirikisho la Transcaucasia na JKKSU mbele ya Kamati Kuu ya CKU(Mab.) kwa mapendekezo halisi. Suala la uunganishaji liliwasilishwa pia na Byelorussia mnamo wakati ule kama katika Ukraina na Transcaucasia.

Tarehe 10 Agosti, 1922, Kamati Kuu ya CKU(Mab.) ilipitisha azimio kuhusu hatua za kimatendo za kuelekea katika uundwaji wa muungano wa jamhuri huru za Kisovieti, ikiunda

tume ya matayarisho kwa ajili ya shabaha hiyo.

Katika kuamua uhusiano baina ya jamhuri mbalimbali ndani ya dola moja la Muungano, yapasa pazingatiwe mwongozo wa kimatengenezo uliosaidia kuunda Shirikisho la Transcaucasia, ambalo uanzishwaji wake ulikuwa ni sharti la lazima (kwani mabaki ya uhasama baina ya mataifa yalikuwa na nguvu sana huko) na kusadifiana na kazi ya maandalio kwa uunganishwaji wa jamhuri huru zote za Kisovieti.

Kwa kutofautiana na JKKSU, Shirikisho la Transcaucasia halikutegemezwa juu ya msingi wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani, lakini ulikuwa ni muungano wa jamhuri tatu zilizo sawa na zenye mamlaka zao zenyewe za kiserikali. Juu yao kulikuwa na Baraza la Muungano, ambalo jamhuri zote hizo za shirikisho zimeliridhia kwa hiari na ambalo lilihusika na mambo ya pamoja kwa jamhuri zote (mambo ya kijeshi, ya uchumi, ya fedha na ya nchi za nje). Jamhuri zote tatu ziliwakilishwa sawasawa katika Baraza la Muungano.

Shirikisho la Urusi lilitoa mfano wa ujenzi wa amani na ushirikiano wa kidugu kati ya mataifa juu ya msingi wa kuaminiana na matakwa ya hiari ya kuunganishwa kwa wananchi wafanyao kazi wa mataifa mbalimbali. Kuhusiana na haya, Lenin aliiona JKKSU kama kifani cha utaratibu wa kiserikali wa mataifa.

Hata hivyo, uzoefu uliopatikana katika Shirikisho la Transcaucasia ulikuwa muhimu kama aina mpya ya uhusiano kati ya jamhuri za Kisovieti, kwani kwa mara ya mwanzo kabisa kati-

ka historia lilitokeza kwa umbo halisi wazo la Shirikisho la muungano lenye kuambata jamhuri huru kadhaa.

Muswada wa azimio kwa kikao kikamilifu cha Kamati Kuu ya CKU(Mab.), "Juu ya Uhusiano Baina ya JKKSU na Jamhuri Huru", ambao ulipitishwa na tume ya matayarisho, ulitambua kujiunga na JKKSU kwa jamhuri huru za Kisovieti za Ukraina, Byelorussia, Azerbaijan, Georgia na Armenia. Ulipendekeza kuliacha wazi suala la kujiunga kwa Bukhara, Khorezm na Jamhuri ya Mashariki ya Mbali, huku kukiendelea kudumishwa uhusiano wa ki-mkataba na jamhuri hizo. Mamlaka ya Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima, Baraza la Mawaziri la Umma, na Baraza la Kazi na Ulinzi la JKKSU yalikuwa yaambate idara kuu za Kisovieti zinazohusika za jamhuri hizo huru zilizojiunga karibuni na shirikisho hilo.

Muswada huo wa azimio ulikusudia kuweko uhusiano wa kishirikisho juu ya msingi wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani, na kwa hivyo ulikuja kujulikana kama mpango wa "kuanzisha utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani".

Vyama vya kikomunisti vya jamhuri huru za Kisovieti vililijadili suala la uhusiano baina yao kwa madhumuni ya kuungana kwao katika dola moja, na mjadala huo ulionyesha kwamba hakujakuwa na pendekezo hata moja kati ya hayo lililopindukia aina zile za shirikisho zilizokuwa tayari zikitumiwa kimatendo. Ilikuwa ama ni shirikisho lililotegemezwa juu ya utaratibu wa kujita-

wala wenyewe kwa mambo ya ndani /muswada uliowasilishwa na tume ya Kamati Kuu ya CKU(Mab.) na maazimio ya KK za vyama vya kikomunisti vya Azerbaijan na Armenia, na pia ya Kamati ya Eneo la Transcaucasia ya CKU (Mab.), ingawa, kama ilivyokwisha tajwa kabla, Shirikisho la Transcaucasia halikutegemezwa juu ya msingi wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani, bali lilikuwa ni muungano wa jamhuri sawa na zenye mamlaka zao zenyewe za kiserikali/ au shirikisho lililotegemezwa juu ya msingi wa kimkataba /azimio la Halmashauri Kuu ya Chama cha Kikomunisti (Mab.) cha Byelorussia/. Ama kwa wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa wa kila aina, basi wao walifanya juu chini ili kukinza muungano wa aina yo yote ile.

Hati za tume hiyo na maazimio yaliyopitishwa na Kamati Kuu za vyama vya kikomunisti vya jamhuri za Transcaucasia zilipelekwa kwa Lenin, na muswada wa azimio "Juu ya Uhusiano Baina ya JKKSU na Jamhuri Huru" uliopitishwa na tume hiyo ulisambazwa miongoni mwa wanachama na wagombea uanachama wa Kamati Kuu ya CKU(Mab.) wakati wa kikao kikamilifu ambacho kilipangwa kufunguliwa mnamo mwanzoni mwa Oktoba 1922. Muswada huo ulikuwa ungali bado umetegemezwa juu ya fikira ya "kuanzisha utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani". Ulitokeza mawazo na maoni ya watumishi wengi wa Chama na wa kiserikali, ambao sehemu kubwa yao walikuwa ni wanamapinduzi watiifu, wenye ari ya umoja wa kimataifa, ambao walitaka kutanzua tatizo la uhusiano

wa mataifa kwa njia bora kabisa kadiri iyumkinikavyo. Waliamini kwamba kufaulu kulitanzua tatizo hilo, kadhalika maendeleo ya mataifa na uimarishwaji wa urafiki baina yao mnamo mipaka ya Shirikisho la Urusi, hilo jambo kwamba mataifa yote yalikuwa yakijumuika kulifuata tabaka la wafanyakazi la Urusi – yote hayo yalipelekea kufanywa uamuzi huo kwamba umbo la uhusiano baina ya mataifa ndani ya JKKSU halina budi kukuzwa katika aina mpya ya muungano wa kiserikali. Isitoshe, wafuasi wa mwelekeo huo wa "kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani", hasa kutoka miongoni mwa watumishi wale wa ngazi za juu ambao walikuwa wakifanya kazi katika jamhuri za kitaifa, ambako sera mpya ya uchumi ilifufua mapambano makali ya kitabaka, waliamini kwamba kushindwa kufuata mwongozo wa kuanzisha utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani kwaweza kuudhoofisha umoja wa jamhuri za Kisovieti. Waliathirika pia kwa msimamo wa wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa wa Georgia, Bashkiria na Tataria wa kutaka kukomesha uhusiano ulioko wa kishirikisho, ili kwamba muungano huo unaoundwa upate kuziingiza kwa masharti sawa jamhuri zote za kitaifa, pamoja na zile zinazojitawala kwa mambo ya ndani. Walipuuza tofauti za kimsingi baina ya jamhuri zijitawalazo kwa mambo ya ndani na zile za Muungano, kwa hivyo kuufagilia njia ufufukaji wa mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa. Kundi la wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa wa Kiukraina lilikuwa likitaka kushurutisha kwa nguvu huo

uliojumlikia kuwa ni umoja wa kishirikisho wa kibwanyenye. Yote haya yaliwatia wasiwasi watumishi wengi wa Chama, ambao walichelea kwamba kutilia mkazo uhuru na mamlaka ya kiserikali ya jamhuri kutadhoofisha misingi ya umoja wa wafanyakazi wa kimataifa na kutawapa wale wanaopendelea kujibagua kitaifa kisingizio cha kufanya mashambulio mengine dhidi ya Chama.

Wafuasi wengi wa kweli wa umoja wa kimataifa waliliunga mkono wazo la "kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani" pia kwa sababu walio na uundwaji wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti kwa vikubwa sana kama ni njia ya kuyakabili majukumu ya kimataifa, ya ulinzi na ya kiuchumi, hasa yale ya kuufufua uchumi uliotekezwa, jambo ambalo lilihitaji ukusanywaji pamoja wa akiba na nguvu zote, na kuwakushughulika na utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa, wala matazamio ya ujenzi wa usoshalisti katika uundaji wa muungano mpya wa kiserikali.

Wafuasi wa ukusanyaji pamoja wa utawala hawakuzingatia mtataniko wote wa uhusiano baina ya mataifa wakati ule, hali hiyo ya kuhitilafiana, ambapo kushamiri kwa mielekeo ya kujitenga, halikadhalika na ule ya kupendelea umoja wa kimataifa, kulikuwa si kwa kusadifia tu; waliikadiria haba hamu ya kimaumbile ya kuwania usambazaji madaraka ambayo inakutikana miongoni mwa umma wa vibwanyenye uchwara katika jamhuri za kitaifa. Vikosi vidogo vya tabaka la wafanyakazi katika jamhuri hizo vilikuwa vimedhoofishwa. Mapambano ya umma wa wananchi

wafanyao kazi dhidi ya uvamizi na ukaliwaji wa maeneo ya jamhuri zao za kitaifa, kadhalika dhidi ya tawala za kimabavu za kibwanyenye na za kujibagua kitaifa katika sehemu hizo yalizidisha jitihada zao za kuwania umoja na tabaka la wafanyakazi la Kirusi. Wakati huo huo baadhi ya wakazi wa huko waliendelea kushikilia maoni yao ya kujibagua kitaifa na ya kupendelea kujitenga, kutoiamini kwao Urusi ya Kati, na jambo hili lilikuwa ni chanzo chema cha kuchipuka kwa wafuasi wa mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa.

Wakipambana na mitindo hii na kuwania kuimarisha fungamano za kidugu baina ya jamhuri zote juu ya msingi wa umoja wa wafanyakazi wa kimataifa, wafuasi wa mwelekeo huo wa "kuanzisha kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani" walishindwa kuzingatia vilivyo haja ya kuzitilia nguvu haki za jamhuri za kidugu za kuwa na mamlaka zao zenyewe za kiserikali, na jambo hili mara nyingi lilitumiwa na wapepeleaji kiburi cha dola kuu na wafuasi wa kienyeji wa mtindo wa kujibagua kitaifa.

Ilikuja kuwa dhahiri kwamba mpango wa "kuanzisha utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani" ulikuwa haukubalika baada ya Vita vya Nchini na uvamizi wa kigeni, wakati jamhuri zilizo huru zilipojitokeza kama madola yanayojitegemea yenyewe. Katika hali hizi, hakujakuwa na aina yo yote ya uhusiano wa kishirikisho kati ya zile zilizokuwako wakati ule ambazo zingetosheleza kikamilifu mahitaji ya majukumu yaliyotokana na uundwaji wa Muun-

gano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti kama umbo jipya la muungano wa kiserikali. Uhusiano wa ki-mkataba haukudhaminia kiasi kinachohitajika cha umoja na ulikuwa ni pingamizi kwa maendeleo zaidi ya dola, na shirikisho lenye kutegemezwa juu ya utaratibu wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani usingedhaminia mamlaka kamili kwa jamhuri zinazoungana na ungetoa fursa ya kuzuka kwa mitindo ya kiburi cha utaifa na kujibagua kitaifa miongoni mwa wakazi wa kienyeji. Hiyo ndiyo maana kwa nini utafiti wa kielekevu wa umbo la kufalia zaidi la muungano ukatokezea kuwa mgumu na wa mtataniko mno.

Ilikuwa ni Lenin ndiye aliyependekeza umbo linalohitajika la uhusiano baina ya mataifa, ambalo lilitosheleza mahitaji yote ya kuheshimu vilivyo mamlaka ya kitaifa, usawa wa jamhuri hizo na kujiunga kwao kwa hiari.

Alipendekeza njia mpya kabisa kimsingi ya kutanzua tatizo hilo: badala ya kuingia katika JKKSU (kama mpango wa "kuanzisha kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani" ulivyokusudia), jamhuri huru za Kisovieti, pamoja na JKKSU, zilikuwa ziungane kwa hiari katika umbo jipya la kiserikali – Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti – juu ya msingi wa usawa wao kamili. Aliandika katika barua kuwapelekea wanachama wa Halmashauri ya Kisiasa ya Kamati Kuu ya CKU(Mab.) tarehe 26 Septemba, 1922: "Twajiona nafsi zetu, JKK ya Ukraina na nyinginezo, kuwa ni sawa, na kuingia pamoja nazo, kwa usawa katika muungano mpya, shirikisho

jipya...". Badala ya kuzigeuza pasina kuwaza vilivyo shughuli za vyombo vikuu vya JKKSU kwendea katika vile vya jamhuri huru, alipendekeza uundwaji wa Kamati Kuu ya Utendaji ya Shirikisho Nzima ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti.

Akishughulikia sana suala la kuwako usawa kamili kwa jamhuri zote zinazoungana, Lenin alitilia mkazo katika barua hiyo: "Jambo muhimu si kuwapigia ngoma wale 'wanaopendelea uhuru', si kuubomoa *uhuru* wao, bali kujenga *ghorofa* nyingine *mpya*, shirikisho la jamhuri *sawa*".

Mpango wa Lenin ulikuwa ni uendelezwaji wa kimantiki wa mawazo yake juu ya muungano wa hiari wa mataifa, kwa usawa wao kamili ndani ya muungano huo, na juu ya kuheshimu mamlaka yao ya kiserikali. Alijua kwamba tatizo la uhusiano wa mataifa lilikuwa ni gumu sana kulitanzua, kadhalika aliyapa nadhari kubwa maoni mbalimbali, wala hakufanya pupa kuyaelezea makosa yaliyofanywa na viongozi fulani katika jamhuri za kitaifa kama ni uachano na ukomunisti mpaka pale suala hilo lilipokwisha fafanuliwa kikamilifu. Wakati huo huo, mjadala wa kusambaa sana wa suala hilo kwa kutegemea maelekezo ya Lenin uliwasaidia wafuasi wa utaratibu wa "kuanzisha kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani" kushikilia msimamo barabara.

Tarehe 6 Oktoba, 1922, kikao kikamilifu cha Kamati Kuu ya CKU(Mab.) kilijadili uunganishwaji wa jamhuri hizo na kupitisha muswada wa mpango wa Lenin.

Maazimio ya kikao hicho kikamilifu na nyara-

ka zilizowasilishwa na tume yake (Tangazo na Mkataba wa Muungano juu ya Uundwaji wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti) zilitolewa kwa ajili ya mjadala wenye kuambata watu wengi kama iyumkinikavyo. Kamati Kuu za vyama vya kikomunisti na mikutano mikuu ya Masovieti ya jamhuri huru zote ilipitisha maazimio ya kupendelea Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti.

Tarehe 29 Desemba, 1922, mkutano wa wajumbe wenye madaraka kamili wa jamhuri huru za Kisovieti ulilichungua Tangazo na Mkataba wa Muungano, na Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Muungano Mzima wa Masovieti, ambao ulifunguliwa tarehe 30 Desemba, 1922, ulizithibitisha nyaraka hizi mbili kama msingi wa majadiliano zaidi na kuazimu kuzipeleka katika Kamati Kuu za Utendaji za jamhuri za Muungano kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Lenin alikuwa na azma ya kuuhutubia Mkutano Mkuu wa Kumi wa Urusi Nzima wa Masovieti, lakini hakuweza kufanya hivyo kwa sababu ya kubanwa na maradhi.

Wakati wa Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Muungano Mzima wa Masovieti (tarehe 30 na 31 Desemba, 1922), Lenin alitoa imla ya barua kuhusu "Suala la Mataifa au 'Kuanzisha Utaratibu wa Kujitawala Wenyewe kwa Mambo ya Ndani'", ambayo umuhimu wake waweza kulinganishwa na maandishi yake ya mwisho ya kimaongozi juu ya masuala ya ujenzi wa baadaye zaidi wa usoshalisti.

Alifahamisha kwamba katika nchi kubwa

yenye mataifa mengi kama hii utanzuaji wa moja kwa moja wa tatizo la uhusiano wa mataifa, jitihada za kudhaminia urafiki baina ya mataifa ni sehemu isiyotenganishika ya mpango wa kujenga usoshalisti.

Katika barua yake, alionyesha kushughulikia sana siyo tu umbo la muungano, bali pia utekelezwaji kimatendo wa Tangazo la Mkataba uliopitishwa na Mkutano Mkuu wa Masovieti. Lenin aliweka nadhari mahsusi juu ya majukumu ya mapambano dhidi ya mitokezo ya mtindo wa kujibagua kitaifa kwa jumla na hasa kiburi cha taifa kuu, akiyafungamanisha majukumu haya na suala la mamlaka ya kiserikali ya kitaifa.

Alibainisha kwamba suala la mataifa lilipembulika kutoka miongoni mwa masuala mengine mbalimbali yenye kukikabili Chama na sera yake: "...wanataifa 'walioudhiwa' hawavutiki moyo kwa cho chote zaidi kama kwa hisia ya usawa na uvunjwaji wa usawa huu, japokuwa kwa mapuuza tu, au kwa mzaha tu – kwa uvunjwaji wa usawa huo kwa upande wa ndugu zao wa kifanyakazi". Suala la mataifa, zaidi kuliko lo lote jingine, lahitajia uhusiano wa kinyoofu, wa kujisabilia na usio na makuu. Lenin alionya: "...Hakuna cho chote kinachozuia maendeleo na uimarishaji wa umoja wa kitabaka wa wafanyakazi kama uenevu wa kitaifa". Aliendelea mbele zaidi kutilia mkazo kwamba "maslahi ya kimsingi ya ushikamano wa wafanyakazi, na kwa hivyo, ya mapambano ya kitabaka ya wafanyakazi yanahitaji kwamba tusilikabili suala la mataifa kwa maoni rasmi tu".

USOSHALISTI PEKEE NDIO UWEZAO KUTANZUA TATIZO LA UHUSIANO WA MATAIFA

Msingi Unaotokana na Hali Halisi wa Ustawi na Ukaribianaji wa Mataifa Yote

Hata kabla ya Mapinduzi ya Oktoba 1917, Lenin alitilia mkazo kwamba aina ya kisoshalisti ya uzalishaji mali itakuwa ndio msingi wa vifaa ambao utaleta aina mpya ya mataifa – mataifa ya kisoshalisti – na itadhaminia ustawi wao wa pande zote na ukaribianaji wao karibu zaidi.

Chini ya utaratibu wa miliki ya kijamii ya nyenzo za uzalishaji mali, ambapo tabaka la wafanyakazi linakuja kuwa ni nguvu yenye kuongoza jamii, kunakuwa hakuna tena msingi wo wote wa kihalihalisi kwa tamaa za kichokozi, kwa hamu ya baadhi ya mataifa kutaka kuyaweka mengine chini ya amri yao, kwa sababu kunakuwa hakuna tena matabaka au makundi yo yote ya kijamii ambayo yangenufaika kwa hayo. Msingi huu wa kitabaka wa ukandamizi wa kitaifa, mtindo wa kujibagua kitaifa na kiburi cha utaifa unabomolewa kabisa. Tabia yenye kuambata umma mzima, ya kimataifa ya miliki ya maliasili ya ardhi na nyenzo nyingine kuu za uzalishaji mali inaa-

mua maendeleo ya kushikamana, ya kudhamiria na yaliyopangwa vilivyo ya mataifa na makabila yote.

Miliki ya kisoshalisti yafanya iyumkinike kuushinda mfarakano wa tangu zamani sana wa mataifa na kuzidisha ushirikiano wao wa pande zote. Mapingamizi baina ya mataifa yanatokomezwa, taratibu mpya za mgawanyo wa kazi zinakuzwa kwa upeo wa dola zima, na kuna maendeleo ya pande nyingi ya uzalishaji mali katika kila eneo moja na nchi nzima kwa jumla chini ya mpango wa aina moja kwa jitihada za pamoja za mataifa yote yanayoishi nchini. Chini ya usoshalisti, mienendo ya kitaifa haihitilafiani na mwelekeo unaotokana na hali halisi wa kuyafanya maisha ya kijamii kuwa ya kimataifa, kama itukiavyo katika jamii yenye matabaka yanayohasimiana. Uanzishaji wa uhusiano wa kimataifa chini ya usoshalisti wamaanisha ukuzaji wa aina zote za mawasiliano na maingiliano baina ya mataifa, pamoja na upeanaji kwa wingi sana wa vitu vyenye thamani ya hali na mali, makada, n. k.

Mfumo wa kiuchumi wa usoshalisti ulioendelea hauwezi kutenda kazi kwa kufana ikiwa nchi ingali bado imegawanyika katika majimbo ya viwanda na ya kilimo, ya malighafi na ya utengenezaji bidhaa, yaliyosonga mbele na yale yaliyozorota, na katika jambo hili unatofautiana na ubepari, ambapo mahali penyewe pa uzalishaji mali mara nyingi huamuliwa kwa mujibu wa utashi wa muda mfupi tu na shabaha za kujipatia faida nyingi zaidi kwa upande wa makampuni ya kuhodhi, ilhali maslahi ya baadhi ya majimbo

huwa yanadhuriwa daima (kama sehemu ya Kusini ya Italia, Uskochi katika Uingereza, au Quebec nchini Canada).

Licha ya mambo yanayotokana na hali halisi, kuna pia jambo muhimu la kinafsini kama lile la jukumu la uongozi la chama cha kimapinduzi katika kudhaminia maendeleo barabara katika hali halisi zilizopo. Lenin alitilia mkazo hasa jambo hili, akisema kwamba katika hali hizo mpya Chama cha Kikomunisti "kinaimarisha na kuyaunganisha mataifa yote ya Urusi katika ukoo mmoja mkuu na wenye nguvu", ambao unakuwa ni kama kitu kimoja kizima.

Tayari hata mnamo wakati wa kufafanua mpango wa usambazaji umeme (1921) na mpango wa kwanza wa miaka mitano (1927), Chama cha Kikomunisti cha Urusi kilikuwa kimeshautegemeza upandaji wake wa kisoshalisti juu ya msingi wa maendeleo ya pande nyingi ya uchumi wa nchini kwa jumla na hasa wa kila jimbo, pia juu ya majukumu ya kukomesha uzorotaji wa majimbo. Kulianzishwa miradi ya kutumia maliasili za Asia ya Kati, kupanua utaratibu wa mifereji ya kumwagilia maji mashambani katika Transcaucasia na utumiaji wa maji yake kwa madhumuni ya kusambaza umeme, n. k.

Wakati misingi ya usoshalisti ilipokwisha wekwa katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, Urusi iliyokuwa hapo awali nchi ya kilimo iligeuka kuwa dola kuu na hatua kubwa sana za kusonga mbele zimeshapigwa katika kukomesha uzorotaji wa miaka mingi sana wa jamhuri za kitaifa, jambo ambalo lilileta chanzo madhubuti cha

urafiki baina ya mataifa ya nchi nzima.

Umoja wa wananchi wa Kisovieti ulipitia mitihani mikali mingi sana. Mnamo siku za mwanzoni za utawala wa Kisovieti, ilikuwa ni umoja huu ndio ulioyadhaminia mataifa ushindi katika Vita vya Nchini na dhidi ya uvamizi wa majeshi ya nchi za kigeni kumi na nne katika 1918-1922. Majukumu magumu ya kustawisha uchumi wa kisoshalisti katika nchi iliyoteketezwa na vita katika hali za kutengwa kabisa kimataifa na mashambulio yasiyokwisha ya ubeberu yalitekelezwa kwa jitihada za pamoja za mataifa yote ya Kisovieti.

Lakini mtihani mkali kabisa kupita yote kwa usoshalisti na sera yake ya uhusiano wa mataifa ulikuwa ni vita vilivyofumuliwa na mafashisti wa Kijerumani dhidi ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti katika 1941. Mafashisti walitumai kushinda vita hivyo kwa kuyafarakisha mataifa ya Kisovieti, lakini tamaa zao zilikwenda arijojo. Urafiki uliopatikana miongoni mwa mataifa yalivyokuwa yakifikilia kiwango kipya cha fahamu ya uzalendo na umoja wa kimataifa ulistahamili mtihani wa vita ahasi kabisa visivyopata kuonekana kabla ya jamii ya binadamu, vita ambavyo vilihatarisha mustakbali wa ustaarabu wa dunia nzima. Uzito mkuu wa vita hivyo uliwaelemea wananchi wa Kisovieti na wakasonga mbele hadi kupata ushindi.

Wakiongozwa na Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, wao si kama walipata ushindi na kuwafurusha mafashisti kutoka katika eneo la nchi yao tu, bali pia walitwaa

jukumu muhimu katika kuyakomboa mataifa mengi ya Ulaya kutokana na utumwa wa kifashisti na kujipatia uhuru wao wa kitaifa. Katika Mashariki ya Mbali Jeshi Jekundu la Kisovieti, baada ya kwisha kuyatokomeza majeshi makuu ya ubeberu wa Kijapani katika bara la Asia, liliikomboa sehemu ya Kusini-Mashariki ya China na Korea ya Kaskazini na kupelekea kupatikana msingi madhubuti kwa ukombozi kamili wa China na Korea kutokana na wavamizi wa Kijapani. Isitoshe, utokomezwaji wa muungano wa mafashisti, ambao nchi ya Kisovieti ilitenda kazi kuu katika upande huo, ulisababisha kuzuka ukweaji mpya wa harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa katika nchi zilizoko chini ya utawala wa kikoloni na utegemezi wa aina hii au ile ambazo zilipelekea kuporomoka kwa mfumo wa kikoloni wa dunia.

Ilivyokuwa ufashisti ulihatarisha siyo nchi ya kisoshalisti tu, bali pia jamii nzima ya binadamu, Muungano wa Jamhuri za Kisovieti uliungwa mkono na Marekani, Uingereza na madola mengine. Baada ya ufashisti kwisha kushindwa, mabeberu wa Marekani na nchi nyingine waligeukia katika siasa ya "vita baridi" kwa kutumai kwamba Muungano wa Jamhuri za Kisovieti hautaweza mnamo kipindi kifupi kabisa cha kihistoria kuufufua uchumi wake ulioharibiwa vibaya na kwamba wao wataweza kuishurutishia masharti yao yo yote yale wayatakayo. Huo ulikuwa ni mtihani mpya na mkali zaidi vile vile kwa mataifa ya Kisovieti, ambayo yakionyesha tena ushujaa mkubwa na ushikamano wao, yalifanya miu-

jiza, kwani mnamo muda wa miaka minne Muungano wa Jamhuri za Kisovieti ulifikilia kiwango kile cha kabla ya vita cha maendeleo ya uzalishaji mali wa viwandani.

Ushindi uliopatikana vitani na ufufuaji uchumi baada ya vita ulikuwa ni ushindi wa mfumo wa kisoshalisti, ambao umeyaunganisha pamoja mataifa na makabila yote.

Yote haya yanakanusha tasnifu ya kupinga ukomunisti kwamba ilivyokuwa Wakomunisti wanaliweka suala la mataifa chini ya malengo ya mapambano ya kitabaka, wao ati wanaelekea zaidi kuzipunguzia umuhimu harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa. Kinyume chake, Wakomunisti wamekuwa siku zote wakiyaona mafanikio ya harakati za kuwania ukombozi wa kitaifa kwa kuambatana vilivyo na mabadiliko ya kijamii. Mathalan, haikuwa ni jambo la bahati tu kwamba mapambano ya wananchi wa Vietnam ya kuwania uhuru wa kitaifa yalichanganyika pamoja na mapambano ya kupinga ubeberu. Haiwezekani kamwe kukanya ukweli huo wa kihistoria kwamba ushindi wa usoshalisti katika kundi kubwa la nchi waonyesha njia halisi ya ukombozi kutokana na ukandamizi wa kitaifa.

Ama kwa nchi za kibepari, mkiwemo zile ambako haki za binadamu zinapigiwa upatu kwa makelele mno, suala la mataifa linaendelea kubaki pasina kutanzuliwa.

Haya yanaonekana wazi, kwanza kabisa, kutokana na hali ya Wanegro na watu wa makabila yote yale yasiyo ya Kizungu huko Marekani, kadhalika kutokana na ukandamizi wa harakati

za kuwania ukombozi katika Ireland ya Kaskazini kwa upande wa mabeberu wa Kiingereza na uchokozi usiokwisha dhidi ya wakazi wasio wa Kizungu huko Uingereza; kutokana na hali ya kutokuwa sawa baina ya wakazi wasemao Kiingereza na wale wasemao Kifaransa nchini Canada; kutokana na tatizo la Walloon na Wafleming huko Ubelgiji, n.k.

Usawa wa Kimatendo wa Mataifa

Utangazaji wa usawa wa kitaifa na uthibitishwaji wake kisheria ni sharti kuu kwa utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa. Lakini usawa wa kisiasa na wa kisheria wa mataifa haitoshi kwa utanzuaji wa tatizo hilo. Ni jambo lijulikanalo na wote, kwa mfano, kwamba usawa kama huo unatangazwa katika nchi za kibepari, lakini hatua hiyo haitanzui kamwe tatizo la uhusiano wa mataifa. Licha ya usawa wa kisiasa, usuluhishwaji wake wahitajia matangulizi ya kiuchumi na kiutamaduni ambayo yangeliwezesha kila taifa kuzitumia kikamilifu haki zilizokwisha tangazwa. Ni suala la kukomesha hali zilizorithiwa na mfumo mpya wa kijamii za kutokuwa sawa kiuchumi na kutokana nako pia kutokuwa sawa kiutamaduni. Kilicho muhimu katika utanzuaji wa tatizo la uhusiano baina ya mataifa ni kupata usawa wa kimatendo hasa.

Kutoka mwanzo kabisa, utawala wa Kisovieti si kama ulitangaza tu usawa wa kisiasa na wa kiserikali wa mataifa yote, lakini, kama ilivyokwi-

sha tajwa hapo awali, ulizipa msaada halisi sehemu zile za pembezoni mwa nchi zinazokaliwa na mataifa madogo ambazo zilikuwa zimezorota, katika kuendeleza nguvu zao za uzalishaji mali na kuinua viwango vyao vya utamaduni.

Katika kufafanua hatua ambazo zingesaidia kukomesha hali ya kutokuwa sawa kimatendo hasa baina ya mataifa, Chama kiliongozwa na mawazo ya Lenin juu ya vipi mataifa yaliyozorota yangeweza kwendea katika usoshalisti. Katika ripoti ya Tume inayohusika na Masuala ya Mataifa na Ukoloni kwenye Mkutano wa Pili wa Jumuiya ya Kikomunisti ya Dunia, Lenin alielezea juu ya mjadala motomoto uliozuka katika tume hiyo kuhusu tasnifu inayotungwa kwa ajili ya mkutano huo. Jambo lenyewe lilikuwa ni kama mataifa yaliyozorota ambayo yalikuwa yanautupilia mbali mkatale wa ukoloni yangeweza kuepukana na daraja ya maendeleo ya ubepari? Lenin alisema ndiyo yangeweza. Alishikilia kwamba "kwa msaada wa tabaka la wafanyakazi la nchi zilizosonga mbele, nchi zilizozorota zaweza kwendea katika mfumo wa Kisovieti na, kwa kupitia daraja fulani za maendeleo, kwendea katika ukomunisti, pasina kubidi kupitia daraja ya ubepari".

Katika hali za Urusi, msaada kama huo ilibidi utolewe na umeshatolewa kwa hakika hasa na tabaka la wafanyakazi la taifa la Warusi kama ndilo taifa lililosonga mbele zaidi nchini. Lenin aliuona msaada utolewao na tabaka la wafanyakazi la Kirusi kuyapa mataifa yaliyozorota ya Urusi kama ni mtokezo wa maoni ya kifanyakazi

kuhusu suala la mataifa.

Katika azimio lake *Majukumu ya Papo ya Chama katika Suala la Mataifa*, Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.) (1921) ulibainisha kwamba chini ya utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi jukumu la Chama ni kukomesha uzorotaji halisi wa mataifa, kuyasaidia yaifikilie Urusi ya Kati katika pande za uchumi, siasa na utamaduni. Azimio hilo lilitaja kwamba hali ya kutokuwa sawa kimatendo kwa mataifa ilikuwa ni matokeo ya kutokuwa sawa kiuchumi kulikotokezea kihistoria. Hiyo ndiyo sababu kwa nini kukahitajika kuendesha mapambano ya muda mrefu na ya kishupavu dhidi ya mabaki ya mkandamizo wa kitaifa ili kuikomesha hali hiyo ya kutokuwa sawa. Kati ya hatua za kimatendo zinazopasa kuchukuliwa, mkutano mkuu huo ulitaja kwanza kabisa ustawishaji wa mfululizo wa viwanda katika sehemu za pembezoni mwa nchi kwa kujenga viwanda na makarakhana karibu zaidi na vyanzo vya malighafi. (Mathalan, katika Turkestan, Bashkiria, Kirghizia na Kaukasi kulipangwa kujenga viwanda vya ufumaji, vya sufi, vya ngozi na vinginevyo.)

Katika maamuzi yake, mkutano mkuu huo ulikadimisha lengo muhimu sana la kukomesha hali ya kutokuwa sawa baina ya mataifa yanayoishi katika sehemu za Mashariki za nchini, ambako uhusiano wa zama za kale na wa kimwinyi ulikuwa ungali bado umehifadhika huko. Mkutano mkuu huo ulisema kwamba yapasa pachukuliwe uangalifu mkuu huko Mashariki wakati wa kuvivutia katika safu za Chama cha Kikomunisti

na shughuli za kiserikali (za Kisovieti) vikosi vya tabaka la wafanyakazi vya kienyeji vilivyo vidogo kwa kiasi hivi. Uliainisha njia za ujumuishwaji wa masikini wa pande za huko kwa kuwasaidia kusonga mbele kutoka aina za kiuchumi zilizozorota kwendea katika zile za juu zaidi, kutoka mtindo wa maisha ya kuhamahama, usanii na shirika za aina ya mwanzoni kwendea katika kilimo halisi, uzalishaji mali wa ushirika na wa viwandani, ulimaji ardhi uliopangwa juu ya msingi wa kijamii, mkiingizwa usanii na kazi nyingine za kienyeji za kutengeneza bidhaa katika utaratibu wa upangaji wa uchumi. Katika maamuzi yake hayo, mkutano mkuu huo ulionya juu ya mtindo wo wote wa kuigiza kipofu huko sehemu za Mashariki hatua za kiuchumi zichukuliwazo katika Urusi ya Kati, hasa kuhusu mambo yale kama uhodhi wa nafaka na sera ya chakula.

Mkutano mkuu huo ulionyesha ushughulikio mahsusi kwa mataifa yale ambayo ardhi yao ilikaliwa na walowezi wa Kirusi chini ya utawala wa mfalme. Ama kuhusu mataifa haya, mkutano mkuu huo uliyajalizia majukumu ya kijumla kwa lengo mahsusi la kuunganisha jitihada za umma wa wananchi wafanyao kazi wa mataifa haya pamoja na zile za watu wafanyao kazi walio Warusi walioko huko katika kupambana na makulak (wakulima matajiri) wanaobakua ardhi, kwa ajili ya kuwapatia wenyeji wa huko ardhi ya kufaa kwa kilimo.

Maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU(Mab.) yalikuwa na kifungu mahsusi kuhusu mataifa madogo yanayoishi miongoni mwa

wingi ulioshikamana wa taifa jingine. Umma wa wananchi wafanyao kazi wa mataifa hayo madogo ilibidi usaidiwe ili kuweza kuitumia kikamilifu haki ya maendeleo huru kwa mujibu wa tabia yenyewe ya mfumo wa Kisovieti na sera ya Chama cha Kikomunisti. Suala hilo huwa ni la mtataniko mno, kwa sababu taifa dogo kwa kawaida huwa halina eneo lake lenyewe, na inabidi lilindwe dhidi ya mitokezo inayowezekana kutokea ya sera ya kiburi cha utaifa kwa upande wa mataifa ambayo linakaa kwenye eneo lao la nchi.

Kikitekeleza maamuzi ya mkutano mkuu huo, Chama kiliyakinga majaribio ya baadhi ya watumishi wake ya kuharakisha ufyekaji wa mabaki ya zama za kale na ya mgawanyiko wa makabila, kikiyaona majaribio hayo kama ni ya kubahatisha mno, kama yenye kuushushia hadhi utawala wa Kisovieti na kupelekea kuwako hali za kufalia kwa kufanya vitimbi vya kuchochelea mtindo wa kujibagua kitaifa na vya wapinga mapinduzi wa kienyeji (*mabasmatchi*).

Msaada uliokuwa ukitolewa na serikali kuu, na tabaka la wafanyakazi la Kirusi na lile la Kiukraina kuzipelekea sehemu za pembezoni mwa nchi zikaliwazo na mataifa madogo ulifuata mikondo gani?

Kwanza kabisa, fedha zilitengwa kando kutokana na bajeti ya JKKSU, iliyokuwa ingali haba bado wakati ule, kwa ajili ya kujenga miradi, vituo vya umeme na mifereji ya kumwagilia maji mashambani; miradi ya viwanda pamoja nà wafanyakazi wenye ujuzi na wataalamu walihamishwa kutoka majimbo ya kati kwenda katika

sehemu hizi (uundwaji wa vituo kama hivyo vya viwanda ulisaidia kuwajumuisha wakulima chini ya uongozi wa tabaka la wafanyakazi); kulifanywa kazi ya upelelezi ili kutafuta na kutengeneza matawi mapya ya shughuli za viwanda, miradi ya kutumia malighafi za kienyeji kwa kutengeneza bidhaa, na kadhalika.

Mathalan, katika 1921, Transcaucasia ilisaidiwa kwa fedha kwa ajili ya kuendeleza kazi za uchimbuzi wa mafuta huko Azerbaijan, na kwa ujenzi wa kituo cha umeme huko Georgia; wafanyakazi wa Moscow walipeleka zana na wataalamu kwa ajili ya kukipanua kiwanda cha ufumaji vitambaa kilichoko katika mji wa Kutaisi huko Georgia. Wafanyakazi wa Moscow, Petrograd na Ivanovo waliwapelekea Waarmenia mashine, mitambo na zana nyinginezo; Shirikisho la Urusi liliwapa msaada katika ujenzi wa mifereji na miradi mikuu ya kwanza ya vituo vya umeme: vituo vya umeme vya Yerevan na Dzori. Mtando wa kutandaa sana wa mafunzo kwa kazi za viwanda na makarakhana ulikuwa ukianzishwa katika jamhuri za kitaifa.

Msaada katika kuandikisha na kuwaelimisha wasomi kwa sehemu zilizozorota ulikuwa ni wenye umuhimu mkubwa. Kwa vile kulikuwa na makada wachache wa kitaifa mnamo miaka ya mwanzoni ya utawala wa Kisovieti, wapinga mapinduzi walifaulu kujipenyeza katika vyeo vya ngazi za juu wakiwa na shabaha za kuleta uharibifu. Kikiwaandikisha makada wa kienyeji kwa upeo mkuu, Chama kilijitahidi kuhakikisha kwamba sera yake ilikuwa ikitekelezwa barabara

mitaani, kikiwachuja mfululizo wapinga maendeleo waliojipenyeza safuni mwake.

Jukumu gumu zaidi – na muhimu sana – lilikuwa ni lile la kuwatumia watu walioelimika wa mataifa ya kienyeji katika sehemu za Mashariki za nchini, ambako kulikuwa na wachache sana waliojua kusoma na kuandika. Jambo hili liliwahusu pia wale waliokuwa hapo zamani kambini mwa wapinga mapinduzi wa kibwanyenye wenye kujibagua kitaifa, lakini baadaye wakaendea upande wa utawala wa Kisovieti. Kilicho muhimu hapa kilikuwa ni kuwafunza makada wapya wa kitaifa, na kwa hayo ilihitajika kwanza kabisa kumpiga vita adui ujinga aliyebaki kutokana na enzi za zamani. Kwa mujibu wa tarakimu za sensa ya mwaka 1920 huko Turkestan, Wakazakh na Wakirghiz 21 kati ya elfu ndio waliokuwa wakijua kusoma na kuandika, Wauzbek na Watajik 18 tu, na Waturkmen 6 tu kati ya elfu. Katika Azerbaijan, watu 99 kati ya kila mia walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Lenin alitilia mkazo kwamba jamii ya kikomunisti haiwezi kujengwa katika nchi yenye watu wasiojua kusoma na kuandika. Mtu asiyejua kusoma na kuandika anakuwa nje ya siasa, inambidi kwanza ajifunze abjadi. Aliona kuwa ni lazima kutenga kando fedha zote zinazoyumkinika, pasina kujali shida zote, kwa ajili ya kukuza elimu. Kamati Kuu ya CKU(Mab.) na Lenin binafsi walitoa msaada halisi katika kustawisha utamaduni wa kitaifa katika sehemu za pembezoni mwa nchini. Wanasayansi, walimu, wahandisi, na watumishi walioelimika wa Chama na serikali walipelekwa

katika sehemu hizi, na shule za kienyeji na viwanda vya upigaji chapa vilipatiwa zana, vitabu vya masomo na karatasi. Serikali ya JKKSU hata ilitenga kando kiasi maalumu cha fedha za kigeni (ambazo zilikuwa haba sana) kwa ajili ya ununuzi na upigishaji chapa huko ng'ambo vitabu vya masomo kwa lugha za kienyeji.

Mnamo wakati wa shida sana kwa nchi hii, vyuo vikuu vya kwanza na taasisi mahsusi zilifunguliwa katika jamhuri za kitaifa (Turkestan, Armenia, Byelorussia na nyinginezo).

Mwelekeo mwingine wa msaada katika kuwafunza makada wa kitaifa ulikuwa ni kuwavutia watu kwa wingi kutoka katika jamhuri za kitaifa kwa ajili ya kushiriki katika kazi kwenye miradi mikuu ya ujenzi yenye umuhimu kwa dola zima, ili kwamba baada ya kwisha kupata ujuzi wa kazi warejee makwao. Wawakilishi wengi wa mataifa yote pia walipata mafunzo kwenye vyuo vya elimu ya juu katika miji mikubwa ya nchini. Mathalan, katika 1931 zaidi kuliko watu 35,000 kutoka Tataria walifanya kazi katika migodi ya huko Donbass, na kiasi 3,000 walishiriki katika ujenzi wa mradi wa Magnitogorsk. Katika mwaka wa masomo wa 1927/28, katika miji mikubwa ya Jamhuri ya Shirikisho ya Urusi wawakilishi kutoka jamhuri na majimbo ya kitaifa walihesabika kuwa asilimia 24.6 ya wanafunzi wote wa vyuo vya juu vya ufundi, asilimia 32.5 ya wanafunzi wote katika vyuo vya masomo ya juu ya kiuchumi na asilimia 19.8 – katika vile vya mambo ya kilimo.

Njia nyingine muhimu ya kuwaelimisha maka-

da wa kitaifa ilikuwa ni kuwashirikisha katika kazi ya chombo kikuu cha Serikali na Chama, pia kazi ya shughuli kuu za kiuchumi na taasisi za kisayansi mjini Moscow na makao mengine makuu ya uzalishaji mali na utamaduni. Shule kama hiyo ya kimataifa ya "Kirusi" iliwafunza makada wa kitaifa kwa ajili ya kufanya kazi katika jamhuri zao na majimbo yao.

Mwelekeo muhimu sana katika kupata usawa wa kimatendo hasa miongoni mwa mataifa ulikuwa ni kudhaminia ujenzi chapuchapu zaidi wa kiuchumi na kiutamaduni katika jamhuri na majimbo ya kitaifa, na haya yalifanywa kwa msaada wa sera ya Chama na upangaji wa kisoshalisti. Mathalan, mnamo kipindi cha mpango wa kwanza wa miaka mitano, uzalishaji mali wa viwandani nchini kote uliongezeka maradufu, ilhali katika sehemu za pembezoni mwa nchi zenye kukaliwa na mataifa madogo uliongezeka kwa zaidi ya mara 3.5, na katika Jamhuri za Asia ya Kati – takriban kwa mara 5.

Maendeleo chapuchapu zaidi ya majimbo ya kitaifa yalipelekea kulipunguza haraka kwa kiasi pengo lililokuwako baina ya kiwango cha uzalishaji mali wa viwandani katika majimbo yaliyoendelea zaidi na yale yaliyoendelea haba kiuchumi. Haya yalipatikana kwa njia ya ugawaji upya wa Bajeti ya Taifa. Yatosha kusema kwamba kwa miaka mingi, urari wa bajeti za baadhi ya jamhuri ulikuwa ukipatikana kwa vikubwa sana kutokana na misaada iliyotolewa na Bajeti ya Taifa. Kwa mfano, katika 1924 na 1925, sehemu ya pato lake yenyewe ya Jamhuri ya Kisovieti ya

Kisoshalisti ya Turkmenistan katika bajeti yake ilikuwa haipindukii asilimia 10. Hata jamhuri kubwa kama hiyo ya Ukraina wakati ule ililipia asilimia 40 tu ya matumizi yake ya bajeti kutokana na fedha zake yenyewe. Wakazi wa jamhuri na majimbo yale ambako hali za vifaa zilikuwa ngumu mno walisamehewa kwa miaka mingi–kabisa au kwa sehemu–wasilipe kodi za kilimo na zile za kiraia. Wakati huo huo, bei za ununuzi wa mazao ya kilimo ziliwekwa kwa kiwango kile ambacho kiliwezesha kukuza maendeleo ya uchumi katika majimbo yaliyokuwa yamezorota hapo zamani.

Wakati wa ujenzi uliopangwa wa usoshalisti na utekelezwaji wa mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya miaka mitano mitano, kulichomoza njia mpya za kupanga mahali pa kuingiza nguvu za uzalishaji mali nchini. Mathalan, miradi ya viwanda ilikuwa ikijengwa karibu zaidi na vyanzo vya malighafi, utumiliwaji wa maliasili nyingi zaidi ulikuzwa katika jamhuri zote za kitaifa, na uzalishaji wa kilimo katika majimbo mbalimbali ulikuwa ukiwekwa juu ya msingi mpya na kufuata mielekeo maalumu. Shukrani kwa sera hiyo, makao makubwa ya viwanda yakiwa na misingi yao yenyewe ya nishati yaliundwa katika jamhuri za kitaifa, na makada chungu nzima wa tabaka la wafanyakazi na wasomi wa aina mpya kuelimishwa. Kutokana na mwendo mkubwa sana wa ustawishaji wa viwanda na ujenzi wa makao mapya ya viwanda, mamia ya miji mikubwa na midogo ilikuwa ikichipuka nchini kote (kwa vikubwa sana katika jamhuri za kitaifa), na wakazi wa miji-

ni waliongezeka kwa wingi sana. Nguvu za uzalishaji mali za Dola la Kisovieti lenye mataifa mengi kwa jumla zilikua upesi, na uchumi na utamaduni wa kila jamhuri moja mbali ulichanua ajabu.

Uundwaji wa viwanda vya kisasa katika jamhuri zote na majimbo yote ya kitaifa ulimaanisha mabadiliko makuu katika maisha ya mataifa na makabila mbalimbali. Ukiukaji kwendea katika ustawishaji wa viwanda juu ya msingi wa kisoshalisti ulifanya mengi sana katika kukomesha uzorotaji, kuzidisha vikosi vya makada wa kitaifa, na kukuza utamaduni wa kila taifa. Yote haya yalipelekea kuinua juu sana kiwango cha hali ya maisha na utamaduni cha tabaka la wafanyakazi na wananchi wote wafanyao kazi. Kwa kadiri hali za kutokuwa sawa kitaifa zilivyokuwa zikikomeshwa, viwango vya maendeleo ya kiuchumi vya majimbo yote ya nchini vilikuwa pia vikisawazishwa. Jambo hilo lilifanya isiyumkinike kwa jamhuri yo yote au jimbo lo lote kuzitumia kichoyo fursa za hali zake za kijiografia au uwezo mkubwa zaidi wa kiuchumi.

Yote hayo yaliiwezesha serikali kupeleka sehemu kubwa zaidi ya viingizia mali ya Taifa katika majimbo yale ya nchini na matawi yale ya uchumi ambayo yalihitajika kustawishwa chapuchapu kwa maslahi ya dola zima na mahitaji ya maendeleo ya kisayansi na kiufundi. Mathalan, kulifanywa jitihada mahsusi ili kustawisha mwambatano wa shughuli za kilimo na viwanda katika eneo la sumaki la Kursk, kuunda msingi wa kutoa mafuta na gesi huko Siberia ya Magharibi, kuzitumia maliasili nyingi sana kwa madhumuni ya

uzalishaji mali katika Asia ya Kati na Mashariki ya Mbali, n. k.

Leo, ustawishaji zaidi wa kiuchumi wa kila jamhuri, jimbo na mtaa wategemea juu ya usongaji mbele kiuchumi wa nchi nzima. Mnamo mipaka ya mtando wa kiuchumi ulioko, mwelekeo wa kushughulikia pande maalumu katika uzalishaji mali waimarisha utegemeano wa kiuchumi baina ya jamhuri hizo na, licha ya kuzidisha ufanisi wa uzalishaji mali, unasaidia pia kuyajongeza karibu zaidi mataifa hayo ya kisoshalisti.

Mapinduzi ya utamaduni yaliyoshinda nchini yalikuwa ni sehemu kuu isiyotenganishika ya sera ya Chama iliyolengewa katika kupatikana usawa wa kimatendo baina ya mataifa. Hayakufungika katika upande wa kueneza uongofu tu kwa jumla, bali yaliupa umma wa wananchi wa mataifa yote fursa ya kupata elimu ya kila aina, sayansi na utamaduni, kadhalika yalisaidia kuwavutia wananchi wafanyao kazi washiriki katika wendeshaji wa mambo yote ya serikali, na kumwadilisha binadamu kwa hulka mpya ya kisoshalisti na tabia mpya za kijamii.

Yote haya yalifanya iwezekane mnamo kipindi kifupi sana cha kihistoria kuzigeuza sehemu za pembezoni mwa mamlaka ya zamani ya Urusi yenye mfumo wa kimwinyi nusu kuwa madola ya kisoshalisti yenye viwanda vya kisasa na kilimo kilichostawishwa vilivyo, kuwa jamhuri zilizofikilia kiwango cha juu sana cha maendeleo ya sayansi na utamaduni, ambako kila mtu ameshajua kusoma na kuandika. Umma wa wananchi wafanyao kazi wa jamhuri hizi walipiga hatua kuu

ya kusonga mbele kutoka uhusiano wa zama za kale, wa kimwinyi kwendea katika usoshalisti, pasina kubidi kupitia daraja ya ubepari ya maendeleo ya kijamii. Sehemu za pembezoni mwa nchi, ambazo kabla ya mapinduzi ilibidi ziagize kila kitu kutoka nje, hata sindano, sasa zinasafirisha aina nyingi za bidhaa za viwandani kwendea katika madarzeni kadhaa ya nchi mbalimbali, mkiwemo nchi za kisoshalisti na za kibepari zilizoendelea kwa shughuli za viwanda. Viwango vya ufundi kwenye viwanda vya kisasa katika jamhuri zote ni vya juu sawa na vile vionekanavyo mjini Moscow na Leningrad, na wafanyakazi huko ni wenye ujuzi wa juu vile vile.

Jamhuri yo yote yaweza kutumika kama mfano wazi wa mabadiliko makuu yaliyotukia katika maisha ya wananchi wa Kisovieti tangu wakati wa mapinduzi. Mathalan, mnamo nusu karne iliyopita Uzbekistan haikuwa na wafanyakazi wo wote wa viwandani, na hivi sasa kuna kiasi milioni mbili. Mnamo miaka ya utawala wa Kisovieti, mashirika makubwa ya kiuchumi yapindukiayo 1,300 yameshajengwa katika zaidi ya matawi mia ya shughuli za viwanda, hasa viwanda vya ufuaji madini zilizo za chuma, vya utengenezaji wa mitambo, viwanda vya kemikali, vya mafuta, vya vyombo vya nishati, uchimbuzi wa makaa, gesi na madini, viwanda vya ufuaji chuma, vya utengenezaji wa vitu vya matumizi ya kila siku, vya chakula na vinginevyo. Mnamo muda wa miaka mitano kutoka 1976 mpaka 1980, uzalishaji mali wa viwandani katika jamhuri hiyo uliongezeka kwa asilimia 27.4. Inatengeneza ndege, matrekta,

mashine kubwa za kuchimbulia udongo, mashine za kuvunia pamba na zana za aina ya kipekee.

Ugunduzi wa gesi katika jimbo la Bukhara ulifanya iwezekane kuanzisha tasnia ya gesi ambayo inatoa gesi siyo kwa Asia ya Kati tu, bali pia kwa makao makuu ya shughuli za viwanda huko Ural, ikiiwezesha jamhuri hiyo kuacha makaa.

Mabaliliko makuu yametukia katika kilimo vile vile, ambako hali za maisha na za kazi za wakulima zimebadilika mno pasina kutambulika. Mito na maziwa yaliyofanywa na watu wenyewe na majengo ya aina ya kipekee ya kuzitia hatamu nguvu za maji yalijengwa katika jamhuri hiyo. Mmojawapo wa kurasa za fahari sana katika tarehe ya dola la Kisovieti lenye mataifa mengi ulikuwa ni utanzuaji wa tatizo gumu sana kama lile la ulimaji wa Mbuga za Njaa zisizo na uhai na zinazokaribia kuwa jangwa, ambazo sasa zimekuwa ni sehemu kuu ya kilimo kitoacho mazao mengi sana, yenye mashamba ya rutuba ya ukubwa upatao hekta laki tano.

Uzbekistan ilikuwa tangu zamani ikisifika kwa pamba yake. Katika 1924 utoaji wa mazao ya pamba ulikuwa ni tani 200,000 tu, lakini katika 1980, ilipindukia tani milioni 6.

Kumetukia mabadiliko makuu katika upande wa utamaduni, katika mambo ya kirohoni ya wananchi wa Uzbekistan. Chini ya utawala wa mfalme, asilimia 3.6 tu ya wakazi wa huko ndio waliokuwa wakijua kusoma na kuandika. Hakujakuwa na vyuo vyo vyote vya elimu ya juu wala taasisi zo zote za utamaduni. Leo, adui ujinga ameshapigwa vita kabisa katika jamhuri hiyo.

Kuna shule 9,540 za elimu ya kawaida, vyuo 41 vya mafunzo ya juu, na shule 177 za elimu mahsusi ya sekondari, zote pamoja zikiwa na wanafunzi wapindukiao milioni 4. Jamhuri hiyo pia ina Akademia ya Sayansi yake yenyewe na taasisi 188 za uchunguzi wa kisayansi zikiwa na wachunguzi 28,000. Kuna majumba ya tamasha 25, Jumba la muziki (*filharmonia*), zaidi kuliko klabu 3,500, maktaba 6,000 za kijamii, makumbusho 29, vituo vipindukiavyo 4,000 vya kuonyeshea sinema, na studio za kutengenezea filamu za michezo na zile za habari na uenezaji maarifa. Chini ya utawala wa mfalme wa Kirusi kulikuwa na hospitali 63 zikiwa na vitanda 997 kwenye eneo la sasa la Uzbekistan, na leo, jamhuri hiyo ina hospitali 1,200 zenye vitanda 134,000, zahanati na vituo vya kutoa msaada wa haraka kiasi 2,000, maelfu ya vituo vya siha na manzili nyingine za utibabu zikiwa na madaktari wapindukiao 31,000 na wauguzi na watumishi wengine wa huduma za utibabu 96,000. Jamhuri ya Uzbekistan leo ina wataalamu wengi wenye elimu ya juu na ya sekondari mahsusi kuliko wale waliokuwako katika nchi nzima ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti mnamo mwishoni mwa miaka ya 1920.

Ujengwaji upya wa Tashkent, mji mkuu wa Uzbekistan, uliobomoka kutokana na mtetemeko wa ardhi katika 1966 ambao uliwafanya Wauzbek wahisi kwa dhati yao manufaa ya sera ya Chama cha Kikomunisti na urafiki wa mataifa ya nchi hii ya Kisovieti. Maelfu ya watu waliojitolea kutoka katika Shirikisho la Urusi, Ukraina, Byelorussia, Kazakhstan, Georgia, Lithuania, Mol-

davia na jamhuri zote nyingine za Kisovieti walikwenda Uzbekistan kuujenga upya mji mkuu wa jamhuri hiyo. Moscow ilipeleka treni 15 za vifaa vya ujenzi, Leningrad–8, Ukraina–10, na kadhalika. Kwa gharama za jamhuri za kidugu kulijengwa mji mpya. Mji huo wenye wakazi wapatao milioni 1.5 ulikuwa mkubwa zaidi, wa kisasa zaidi na wa kuvutia zaidi.

Usawa halisi wa mataifa yote, ustawi wao kamili hauyumkiniki isipokuwa katika dola la kisoshalisti tu, ambako mataifa yanashughulika katika ushirikiano wa kidugu, ambako mataifa yaliyosonga mbele zaidi yanatoa msaada wa pande zote kuyapa mataifa yaliyokuwa yamezorota hapo zamani.

WANANCHI WA KISOVIETI– MJUMUIKO MPYA WA KIJAMII NA WA KIMATAIFA WA WATU

Uchomozaji wa wananchi wa Kisovieti kama mjumuiko mpya wa kijamii na wa kimataifa wamaanisha, kwanza kabisa, upatikanaji wa umoja wa kijamii na ushikamano wa matabaka yote, makundi ya kijamii, mataifa na makabila kama ni matokeo ya kimaumbile ya ujenzi wa usoshalisti, yenye kuonyesha tabia mpya kabisa kimsingi za maisha ya kijamii katika hali za usoshalisti ulioendelea.

Mjumuiko huu mpya ulibunika wakati wa kufanyika kwa ujenzi wa usoshalisti na uhuishwaji wa mataifa yote, kwa kadiri viwango vya maendeleo yao vilivyokuwa vikisawazika na kupata usawa wa kimatendo hasa. Mjumuiko huo umetegemezwa juu ya msingi wa kihalihalisi: miliki ya kijamii ya nyenzo za uzalishaji mali, umoja wa mambo ya kiuchumi, kijamii-kisiasa na kiutamaduni, itikadi iliyotegemezwa juu ya mafunzo ya Marx na Lenin na maslahi ya pamoja na malengo ya kikomunisti ya tabaka la wafanyakazi. Ta-

baka la wafanyakazi likiwa ni tabaka lenye ari kubwa zaidi ya umoja wa kimataifa, linatwaa jukumu muhimu katika kuyajongeza karibu zaidi mataifa na makabila yote. Mpango wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti wasema kwamba ufutwaji wa mipambanuo baina ya matabaka na ukuzwaji wa uhusiano wa kijamii wa kikomunisti wapelekea kuwako umoja mkubwa zaidi wa kijamii wa mataifa na kusaidia kuendeleza tabia za kikomunisti za aina moja za utamaduni, maadili na namna yao ya maisha, kadhalika kuimarisha zaidi hali ya kuaminiana na urafiki baina yao.

Ujenzi wa usoshalisti ulileta muundo mpya wa kijamii uliotegemezwa juu ya ukosekano wa uhusiano wa kinyonyaji na uhasama wa kijamii, na haya yameibadilisha hulka yenyewe ya makundi yote ya kijamii na kuyajongeza pamoja karibu zaidi. Tabaka la wafanyakazi nafsi yake limebadilika na kuwa ndiyo nguvu iongozayo katika jamii. Wakulima pia wamebadilika kimsingi, wakipata tabia mpya: ari ya ujima na ujuzi wa kazi ya pamoja, na kufuata njia mpya za kisasa za ukulima zinazoshabihiana na zile za kazi za viwandani. Kijitabaka cha wasomi wa kisoshalisti, mkiwemo wataalamu wa mambo ya sayansi na ufundi, kimeongezeka kwa idadi, na kimekuja kutwaa jukumu muhimu zaidi katika ujenzi wa usoshalisti. Kwa hivyo basi, muundiko wa jamii kwa jumla, na ule wa taifa na kabila, umekuwa ni wa aina moja.

Kuwepo kwa wananchi wafanyao kazi wa mataifa mengi katika kila jamhuri ni zenye umuhi-

mu mkuu katika kuyajongeza karibu zaidi mataifa na kumwadilisha binadamu kwa hulka mpya (mathalan, huko Ukraina, Kazakhstan na Uzbekistan watu wa mataifa na makabila yapindukiayo 100 wanaishi ubavu kwa ubavu na wale wa mataifa ya huko). Mtu mwenye hulka mpya anaadilishwa kwenye miradi mikuu ya ujenzi ya nchini, ambayo inajengwa na kisha kuendeshwa na wawakilishi wa jamhuri zote. Kituo cha Umeme cha Nguvu ya Maji cha Nurek, kwa mfano, kilijengwa na wawakilishi wa mataifa 30, na kile cha Kremenchug huko Ukraina, na wale wa mataifa 41. Kiwanda kikuu cha utengenezaji magari cha Volga sasa kinaajiri wafanyakazi na wataalamu wanaowakilisha mataifa 44, na mahandisi na wafanyakazi wa mataifa zaidi ya 50 wanashiriki katika kukiendesha na kukipanua kiwanda kikuu cha utengenezaji magari cha Kama huko Tataria.

Mapinduzi ya utamaduni na uchanuaji wa utamaduni wa kila taifa wenye kuandamana nayao yalizidisha mwendo wa kudahiliana kwao na kutajirishana, yakiyaweka mafanikio bora kabisa ya utamaduni wa kila taifa sabili kwa mataifa yote mengine ya Kisovieti kama ni hazina ya wananchi wote wa Kisovieti. Upandaji juu wa kiwango cha elimu na utamaduni nchini kote wasaidia kueneza na kupokea mafanikio ya utamaduni ya mataifa yote. Desturi njema kabisa za kila taifa zinajaliziwa kwa maudhui mapya, ya kisoshalisti, zinapatanishwa vizuri na tabia za umoja wa kimataifa wa wananchi wote wa Kisovieti.

Kama Mpango wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti unavyoainisha, maumbo ya kitaifa, halikadhalika na maudhui yao, hayakomai, bali yanabadilika, yanakamilika na kujongeleana karibu zaidi, na kutupilia mbali yote yale yaliyokwisha zake, yenye kuhitilafiana na hali mpya za maisha. Maendeleo ya wananchi wa Kisovieti katika hali ambapo ukandamizi wa kijamii na wa kitaifa unakuwa umeshakomeshwa na mataifa na makabila ya kisoshalisti yanajongeleana karibu zaidi, yanakuwa wakati huo huo ni mwendo wa kuadilika na kukazanika kwa binadamu mwenye hulka mpya, ambaye tabia zake za umoja wa kimataifa zinachanganyika kwa upatanifu na tabia bora kabisa za kitaifa zilizopatikana kihistoria.

Ukuzwaji wa upatanifu wa uhusiano wa mataifa na kutokana nao uchomozaji wa binadamu mwenye hulka mpya na ari ya umoja wa kimataifa unaamuliwa siyo na matangulizi ya kihalihalisi tu, bali pia na sera ya Chama cha Kikomunisti ya uhusiano wa mataifa ya kudhamiria iliyotegemezwa juu ya uchambuzi wa kisayansi.

Chama cha Kikomunisti na serikali ya kisoshalisti zinatoa athari ya bidii na ya utaratibu maalumu juu ya ufanywaji wa maisha ya kijamii kuwa ya kitaifa, zikiupa upeo kamili mwelekeo huu wa kihalihalisi. Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti kimekuwa kikifuata mwongozo wa mpango maalumu wa ujongeleanaji wa mataifa, wa usaidiano mkubwa zaidi baina yao katika maendeleo ya uchumi na wa kukuza upeanaji wa vifaa na johari za utama-

duni. Mashindano ya kufana baina ya timu za wafanyakazi za jamhuri mbalimbali na hatua nyingine kama hizo zinatenda kazi muhimu katika upande huu. Serikali ya Kisovieti imekuwa ikigharimia kwa mpango maalumu hatua za upeanaji wa johari za utamaduni, ikisaidia kutengeneza siku za fasihi na sanaa za mataifa ya kidugu, uonyeshaji nchini kote wa filamu bora za sinema zilizotolewa na studio za mataifa mbalimbali, maonyesho ya picha za kuchorwa, utangazaji wa mafanikio mema kabisa ya utamaduni ya mataifa yote ya Kisovieti kwa kupitia katika televisheni na redio ya Taifa, na tafsiri za maandishi fasihi ya kitaifa katika lugha ya Kirusi na nyinginezo zitumikazo katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti.

Kama matokeo ya jitihada za Chama, tabia zile ambazo ni za namna moja kwa wananchi wote wa Kisovieti zinazidi kutia mizizi zaidi katika mambo ya kijamii ya kisiasa na ya utamaduni, katika kazi ya umma na mwenendo wao wa kila siku. Maadili ya kikomunisti yaliyo kimsingi na ya kimataifa ndiyo yanayofunza kawaida za adabu za uhusiano sawa, wa kidugu baina ya wananchi wote wafanyao kazi, pasina kujali taifa, na kwa hivyo kusaidia kuimarisha jamii ya mataifa mengi.

Kwa hivyo basi, wingi mkubwa kabisa wa wananchi wafanyao kazi wa kila taifa na kabila la Kisovieti zinazidi kutambua kwamba jadi yao ni ile ya wananchi wa Kisovieti kama mjumuiko mpya wa kijamii na wa kimataifa na kuja kuwa na hisia ya fahari kwa kuwa raia wa Kisovieti, hi-

sia yenye kutandaa na kupenya ndani zaidi kuliko hisia za taifa za kawaida za mataifa mbalimbali ya Kisovieti. Fahamu ya kitaifa ya wananchi wote wa mataifa mbalimbali imejazwa maudhui ya umoja wa kimataifa, na upeo wa mawazo yao umepanuka zaidi kwa sababu ya kupokea mafanikio bora kabisa yaliyopatikana kwa kazi na ubingwa wa kusanii wa mataifa yote ya Kisovieti. Malengo na desturi za uzalendo na za umoja wa kimataifa, zilizoendelezwa na kutajirishwa wakati wa ujenzi wa usoshalisti na ukomunisti, zinachanganyika kwa upatanifu katika fahamu ya mataifa hayo ya kidugu. Itikadi ya umoja wa kimataifa wa kisoshalisti ambayo inafuatwa na umma wa wananchi wafanyao kazi inapanua upeo wao wa maoni kuhusu ulimwengu, inawasaidia kupindukia dhana zile za mazoea kama "yangu", "ya taifa langu", na "ya jamhuri yangu", na kuja kuwa na mkabala wa kushughulikia dola zima kwa mambo yote, na kutambua kuhusika kwao katika kazi inayowaambata wananchi wote. Kwa hivyo basi, twaona utekelezwaji kimatendo wa dai la Lenin kwamba Wakomunisti "*haiwapasi* kufikiria taifa lao wenyewe tu, bali yawapasa wayaweke maslahi ya mataifa yote, uhuru wao wa pamoja na usawa wao *juu ya* yale ya taifa lao", na kwamba yawapasa "wapambane *dhidi ya* mtindo wa kupakika mno kwa taifa dogo, kujitenga na kujipiga pande, wazingatie kile kilicho kizima na cha kijumla, wayaweke maslahi ya kibinafsi chini ya yale ya pamoja".

Uundwaji wa mjumuiko huu mpya wa kijamii na wa kimataifa waashiria awamu muhimu na ya

juu zaidi katika ujongeleanaji karibu wa mataifa na ustawi wao, ambao unatokezea kuwa ni pande mbili zenye kutegemeana za mwendo ule ule mmoja wa maendeleo ya mataifa ya kisoshalisti. Jaribio la kutaka kuichambua mienendo hii kwa kutengana au, hata zaidi kwa kuipambanisha, linakuwa si la kisayansi na kwenda kinyume na maongozi makuu ya sera ya Lenin ya uhusiano wa mataifa na ya urafiki baina ya mataifa.

Fikira ya Wasovieti walioungana kama mjumuiko mpya wa kijamii na wa kimataifa haihusiani hata chembe na hiyo dhana iliyobuniwa na wataalamu wa kibwanyenye wa elimujamii kuhusu "taifa la Wasovieti la aina moja". Taifa kama hilo haliko wala halitokuwako kamwe. Wasovieti ni watu wa mataifa mengi. Propaganda ya kibwanyenye imebuni dhana hii ili kujaribu kuuonyesha mwelekeo huo wa kujongeleana kwa mataifa ndani ya dola la Kisovieti kama ni matokeo ya sera ya "kuingiza mila na desturi za Kirusi" inayodaiwa ati inaendeshwa na Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti kwa madhumuni ya kudidimiza kila kitu chenye asili ya kitaifa, kupuuza tabia za mpembuo za kitaifa, desturi, mila na maslahi ya kitaifa, kuzuia ukuzwaji wa utamaduni wa kila taifa moja mbali, na kama hayo.

Dhana hiyo ya "taifa la Wasovieti la aina moja", halikadhalika na maamuzi yasiyothibitika yaliyofanywa kutokana na dhana hiyo dhahiri hayana msingi wo wote. Yanatofautiana wazi kabisa na maisha halisi ya kisasa ya mataifa ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, na maendeleo

ya utamaduni wa kila taifa, na ukweli wa kihistoria wa shughuli za Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti katika upande wa suala la mataifa na uhusiano baina ya mataifa ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti.

Inavyoonyesha, propaganda ya mabwanyenye yategemea jambo hilo kwamba watu katika nchi za kibepari hawajui habari hizo vya kutosha, kwamba katika dola la kibwanyenye hawakushuhudia utanzuaji wo wote wa maana wa tatizo la uhusiano wa mataifa, ilhali majaribio yote ya kuleta "usawazishaji" wa mataifa nchini mwao yanashindwa kukomesha udhuriwaji wa maslahi ya mataifa yasiyoendelea sana.

Ujongeleanaji karibu zaidi wa mataifa chini ya usoshalisti hauwezi na haupaswi kufuta mipambanuo ya kitaifa. Mwelekeo huo umefungamana sana na utowekaji taratibu wa tabia zile zilizokwisha zake na kuchomoza nyingine mpya zilizo za namna moja kwa mataifa yote. Kile kilicho cha namna moja kwa yote hujitokeza kwa kupitia katika kile kilicho cha kipekee kwa kila taifa, ambacho huja kupata tabia mpya na, kikibadilika taratibu, kukaribiana na kile kilicho cha namna moja kwa yote. Hayo yanaonekana wazi hasa katika upande wa utamaduni. Ukaribianaji wa tamaduni za kitaifa haupelekei katika upotezaji wa maumbo yao au tabia zao za kipekee, bali wajitokeza katika kutajirishana, katika kulisaidia kila taifa kuyakomesha yale yaliyokwisha zake na kuzikuza tabia na desturi zile ambazo zalingana na mahitaji ya mataifa mengine vile vile. Mwendo huu hauhusiani hata chembe na usawazishaji au

utowekaji wa tamaduni na tabia za kipekee za kitaifa (kama inavyodaiwa na wanaitikadi wa kibwanyenye), bali kinyume chake, wasaidia kuzikuza kwa ukomo wake tamaduni mbalimbali za kitaifa. Kwa hivyo, mapingamizi yo yote yasiyo ya kimaumbile katika njia ya kujongeleana karibu zaidi yangekinza usongaji mbele wa tamaduni za kitaifa na jamii kwa jumla.

Wakati huo huo, ujongeleanaji karibu zaidi wa mataifa – mwendo wa kawaida na wa kimaendeleo – haufai kuharakishwa kwa njia isiyo ya kimaumbile, kwani kufanya hivyo kwaweza kulidhuru lengo la ujenzi wa ukomunisti. Hiyo ndiyo maana kwa nini magazeti ya Kisovieti yakaukosoa msimamo uliochukuliwa na baadhi ya waandishi na wanahistoria wa Kisovieti ambao walidai kwamba ati katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti tabia za kitaifa za kipekee takriban zimeshatoweka kabisa na kupoteza umuhimu wao, hata imeshakuwa haihitajiki tena kuzizingatia katika kuyajongeza mataifa karibu zaidi na kuyasaidia kuungana. Ndugu fulani wa Tataria, wa Byelorussia, Karelia na Ossetia pia walikosolewa kwa kupendekeza upunguzwaji wa idadi ya shule za kitaifa katika jamhuri hizo.

Wale wanaotaka kuusukuma mwendo wa ujongeleanaji wa mataifa baadhi ya wakati hujaribu kuuhalalisha msimamo wao kwa kulitaja shauri la Lenin lisemalo kwamba lengo la usoshalisti siyo tu kuyajongeza karibu zaidi mataifa, bali pia kuyachanganyisha pamoja. Kweli kabisa, Lenin alitoa shauri kama hilo, lakini kwa maana hiyo tu kwamba mwendo huo wa ujongeleanaji

utapelekea hatimaye katika uchanganyishaji wao.

Wakati huo huo, Lenin alionya kwamba haipasi kuzibabaisha dhana za "ujongeleanaji" na "uchanganyishaji" wa mataifa. Kwa hivyo basi, ujongeleanaji wa mataifa si kama unaruhusu tu, bali pia unakusudia hasa kuhifadhi mipambanuo na tabia za kipekee za kitaifa, ilhali kuchanganyika kwa mataifa wakusudia kwamba mipambanuo ya kitaifa inafutwa na kutoweka kabisa. Lenin alisisitiza tena na tena kwamba ukomeshwaji wa mipambanuo ya kitaifa ni mwendo wa mtataniko na utachukua muda mrefu. Aliwakejeli wale walioamini kwamba mipambanuo hii yaweza kuondoshwa upesi, na kuuita mkabala huo kama ni "uotaji ndoto mtupu". Ukorogaji wa fikira hizi mbili na utiliaji mkazo mno mwelekeo wa kuchanganyika kwa mataifa unatatanisha zaidi uelewaji wa tatizo hili gumu sana.

Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, kama ilivyoandikwa ndani ya Mpango wake, hakiruhusu tabia za kipekee za kitaifa ama kupuuzwa au kukuzwa mno. Upunguzaji wo wote wa umuhimu wa mipambanuo ya kitaifa waweza kupelekea katika ufufuaji wa fikira fupi za kujibagua kitaifa. Ni sera barabara tu ya uhusiano wa mataifa, ambayo yatia maanani tabia za kipekee za kitaifa na kukusudia kusawazisha viwango vya maendeleo, ndiyo iwezayo kudhaminia ujongeleanaji wa kufana zaidi wa mataifa na kuweka msingi wa kudumu kwa urafiki baina yao. Ukuzwaji zaidi wa uhusiano baina ya mataifa, uimarishaji wa urafiki baina yao,

uchanuaji na ujongeleanaji wa mataifa ya kisoshalisti kwa upande wake una athari njema juu ya pande zote za maisha katika jamii ya Kisovieti: uchumi, siasa, itikadi, maadili, utamaduni na maisha ya kila siku.

Nyaraka za Mkutano Mkuu wa 26 wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti zimetaja mafanikio na matazamio ya maendeleo ya mataifa na makabila nchini. Utekelezwaji wa mipango ya maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii kwa miaka ya 1980 utaimarisha hali halisi za kuyajongeza karibu zaidi mataifa. Mipango hii inakusudia uchapuaji mwendo wa kuufanya uzalishaji mali kuwa wa kijamii, kuzidisha ukusanyaji pamoja wa uchumi, kushughulikia pande maalumu na ushirikiano katika uzalishaji mali, kuunda miambatano mikuu ya kimaeneo-kiviwanda na ya baina ya sekta mbalimbali za uzalishaji mali, kutumia kwa pamoja maliasili, na pia kufanya kazi kwa pamoja katika miradi mingine mikubwa. Yote haya yanaimarisha fungamano za kiuchumi baina ya jamhuri zote na umoja wa maslahi ya nchi nzima na yale ya kila jamhuri moja mbali.

Ukuzaji wa umoja baina ya mataifa na makabila mbalimbali utasaidia ukamilishaji wa uhusiano wa kijamii, usawazishaji uliopangwa wa viwango vya utamaduni na hali za maisha ya kila siku, uhamaji kutoka sehemu zenye nguvukazi ya ziada kwendea katika majimbo yaliyostawishwa hivi karibuni, ushirikishwaji mkubwa zaidi wa makada wa kienyeji katika shughuli za uzalishaji mali, na ukuaji wa miji mipya.

Wakati huo huo, Mkutano Mkuu wa 26 wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti umetilia mkazo kwamba nadhari kubwa zaidi na ya pande nyingi yapasa iwekwe juu ya haja na maslahi ya kila mfanyakazi, pasina kujali nasaba yake ya kitaifa. Mathalan, mkutano mkuu huo ulihimiza kuwa na uangalifu mkubwa zaidi kwa wafanyakazi wasio wa kienyeji katika jamhuri ya kitaifa, jimbo au eneo lo lote lile la kitaifa lijitawalalo lenyewe kwa mambo ya ndani (haja ya kuwa na uwakilishi kamili wa mataifa yasiyo ya kienyeji katika idara za Chama na Serikali; pawekwe nadhari kubwa na ya pande nyingi kwa mahitaji yao mahsusi kuhusiana na lugha, utamaduni na maisha ya kila siku; pachukuliwe hatua kutosheleza mahitaji haya pasina kukawia).

Mabadiliko ya kupenya ndani sana ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na yale yanayohusika na mambo ya kirohoni na ya kisaikolojia yamepelekea kuundwa kwa mijumuiko ya wakazi yenye mchanganyiko wa mataifa mengi. Kwa mfano, wakazi wa mataifa yasiyo ya kienyeji wanajumlikia asilimia 25 ya wakazi wote katika jamhuri 10 za Muungano na zaidi kuliko asilimia 50 katika jamhuri nyingi zaidi zijitawalazo wenyewe kwa mambo ya ndani. Kuhusiana na haya, bila ya shaka, kulizuka matatizo fulani fulani.

Lakini, Mkutano Mkuu wa 26 wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti ulieleza: "Maisha yenyewe yanaonyesha kwamba maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii yatukiayo kwa wingi sana katika kila moja ya

jamhuri za Kisovieti yanachapua mwendo wa ujongeleanaji wao karibu zaidi katika kila upande".

Umoja wa Wafanyakazi wa Kimataifa Ndio Msingi na Mtokezo wa Ushindi wa Sera ya Lenin Juu ya Uhusiano wa Mataifa

Sera ya umoja wa kimataifa iendeshwayo kwa uthabiti na Chama cha Kikomunisti, ambayo sehemu yake mojawapo isiyotenganishika ni kupambana na kiburi cha taifa kuu na mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa, ilitenda kazi kubwa sana katika utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa na ushindi wa usoshalisti. Mapambano haya yalikuwa ni muhimu hasa wakati dola la Kisovieti lilipokuwa likiumbika na misingi ya usoshalisti ilipokuwa ikiwekwa.

Mapambano dhidi ya kiburi cha taifa kuu yalikuwa wakati ule ndilo jukumu muhimu katika suala la uhusiano wa mataifa, kwani mtindo wa kienyeji wa kuelekea kujibagua kitaifa ulikuwa mara nyingi ni mjibizo wa sera ya kujitukiza kwa taifa kuu. Mastakimu ya umbele ya wawakilishi wa taifa lililokuwa likitawala hapo zamani yalizidisha uhasama wa kitaifa na kukinza ugawanaji wa wenyeji kwa mujibu wa matabaka yao. Kwa maana hii, kiburi cha taifa kuu kilipepelea mtindo wa kujibagua kitaifa kwa wakazi wa kienyeji na kuwanufaisha wapinga mapinduzi.

Mtindo wa kujibagua kitaifa miongoni mwa wakazi wa kienyeji ukiwa kama ni salio la mkan-

damizo wa kitaifa wajitokeza, kwanza kabisa, katika huko kushindwa kupambanua baina ya maslahi ya kitabaka ya umma wa wananchi wafanyao kazi wa taifa lake mwenyewe mtu na yale ya wanyonyaji, katika kuukuza mno umuhimu wa tabia za kitaifa, katika kujipendelea kienyeji, katika hamu ya kutaka kujifungia mnamo mipaka ya taifa lake mwenyewe mtu, katika kupuuza maslahi ya dola zima. Azimio la Mkutano Mkuu wa Kumi wa CKU (Mab.) lilisema kwamba Wakomunisti kutoka miongoni mwa wakazi wa kienyeji wa kiasilia, ambao wao wenyewe wamewahi kufikwa na masaibu ya mkandamizo wa kitaifa, mara nyingi waliukuza mno umuhimu wa tabia za kipekee za kitaifa, wakiyapuuza maslahi ya kitabaka ya wananchi wafanyao kazi. Hali hiyo ilipelekea kupotoka kutoka ukomunisti kuelekea katika mtindo wa kujibagua kitaifa wa kibwanyenye-kidemokrasi. Uchumi wa kibepari wa kibinafsi ulivyokuwa ukihuika kwa kiasi hivi kwa ukiukaji kwendea katika Sera Mpya ya Uchumi, kulikuwa pia na uhuikaji wa mtindo wa kujibagua kitaifa miongoni mwa wakulima na makundi mengine ya kibwanyenye uchwara. Ufufuaji wa uchumi na ujengaji dola na taifa ulisonga mbele katika hali za mapambano makali ya kitabaka. Wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa na wale wapendeleao kujitenga walifanya juu chini ili kuudhoofisha umoja wa jamhuri za Kisovieti katika pande mbalimbali (wa kiuchumi, wa kifedha na wa kiutamaduni). Wafuasi wa mtindo wa kujibagua kitaifa walijipenyeza ndani ya vyombo vya Chama na Serikali na kujaribu

kuendesha sera ya kuleta utengano, wakiitokeza kama ni sera ya utawala wa Kisovieti. Wakijificha kwa miito ya kitaifa, mamwinyi na mabwanyenye wa kienyeji walikuja juu, wakijaribu kuishushia hadhi Jamhuri ya Shirikisho ya Urusi machoni pa wananchi wafanyao kazi wa jamhuri nyingine na kuwaweka chini ya ushawishi wao.

Jukumu la Chama lilikuwa ni kuendesha mapambano ya hadhari, ya uvumilivu, lakini ya kishupavu dhidi ya mitokezo yo yote ile ya mtindo wa kujibagua kitaifa ambao mara nyingi uligeukia kuwa wa kishari. Bila ya mapambano makakamavu dhidi ya mtindo wa kujibagua kitaifa miongoni mwa wakazi wa sehemu za kienyeji haiyumkiniki kuwaelimisha makada wenye kufuata maongozi ya Marx katika sehemu za pembezoni zikaliwazo na mataifa madogo, kuunda jumuiya madhubuti za Chama zenye uwezo wa kuuvutia umma wa wananchi wafanyao kazi katika ujenzi wa shime wa usoshalisti.

Akikihutubia Kikao cha Kwanza cha Kamati Kuu ya Utendaji ya Urusi Nzima na Baraza la Mawaziri wa Umma tarehe 2 Februari, 1920, Lenin alitilia mkazo hatari kubwa mno ya mielekeo ya kuleta utengano. Huku akiunga mkono uhuru wa kujitawala wenyewe kwa mambo ya ndani na mamlaka ya kiserikali kwa jamhuri mbalimbali, yeye alisema, yampasa mtu siku zote achukulie kwamba mapambano dhidi ya umoja ulioshikamana wa mabeberu wahitajia kuweko muungano imara wa mataifa yote, na majaribio yo yote ya kutaka kuuvunja muungano huu yapasa yaonekane kama ni yasiyoruhusika kabisa, kama ni

uhaini kwa maslahi ya mapambano ya pamoja, kwani ubeberu utauchukulia fursa mgawanyiko wo wote ule ili kuuangamiza utawala huo mpya.

Kwa ushindi wa usoshalisti katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, mwongozo wa umoja wa kimataifa ulishinda vile vile. Matabaka ya kinyonyaji ambayo yalikuwa na maslahi katika ukandamizi wa kitaifa na uhasama baina ya mataifa yameshatokomezwa. Vyanzo vya kiuchumi na vya kisiasa vilivyochipua maoni ya kibwanyenye ya kujibagua kitaifa haviko tena. Usawa wa mataifa yote na raia wote wa Kisovieti unalindwa na sheria za kiserikali, ambazo zimeondosha mapendeleo yo yote ya kitaifa na ambazo zinaadhibu majaribio yo yote ya kuchochelea uhasama baina ya mataifa. Chama cha Kikomunisti na Serikali ya Kisovieti zimekuwa zikitumia nyenzo zote za kiitikadi zilizo nazo katika jitihada kuu ya kuwaelimisha wananchi wafanyao kazi kwa ari ya umoja wa kimataifa wa kisoshalisti na urafiki usiovunjika baina ya mataifa yote.

Kwa jitihada za Chama, mamilioni kwa mamilioni ya wananchi wa Kisovieti wa mataifa na makabila yote wameshafuata mwongozo wa umoja wa kimataifa, ambao hapo kabla ulikuwa ni lengo la kikundi kidogo tu cha Wakomunisti, kama imani ya moyoni na kawaida ya mwenendo wao, jambo ambalo laonyesha mapinduzi halisi katika fahamu ya kijamii.

Lakini hata chini ya hali za usoshalisti ulioshinda kunaweza bado kuwako marudio katika kiburi cha utaifa na mtindo wa kujibagua kitaifa kwa sababu kadhaa zinazotokana na hali halisi

na pia zile za kinafsini.

Kwanza kabisa, marudio kama hayo yanatokana na mabaki ya siku za nyuma. Lenin aliyaona mabaki ya mtindo wa kujibagua kitaifa kama ni yenye kudumu kwa muda mrefu zaidi, kwa sababu mabadiliko katika fahamu ya binadamu, kama kawaida, hubaki nyuma ya mabadiliko katika uhusiano wa kiuchumi na kisiasa.

Mabaki ya mtindo wa kujibagua kitaifa yanadumishwa kwa mila za makarne kadhaa, pamoja na zile zilizozorota na zipingazo maendeleo. Hata leo mtu anaweza bado kukumbana na makadirio yaliyopotoshwa na yasiyo ya kisayansi ya historia na mafanikio ya taifa lake mwenyewe mtu na ya mataifa mengine, kukumbana na mawazo na saikolojia ya kuwa na tabia ya kipekee ya kitaifa na ya mpembuo wa kitaifa ambazo zilipaliliwa na matabaka ya kinyonyaji kwa makarne kadhaa. Fikira fupi za kujibagua kitaifa miongoni mwa sehemu fulani ya wananchi kwa vikubwa hudumishwa na dini, ambayo huwaingiza watu hisia ya kujibagua mbali na wenzao wa dini nyingine na kutopatanishika kamwe kwa imani mbalimbali za kidini. Yote haya yanaweza kutokea hata katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, kwa sababu kabla ya mapinduzi wingi wa wakazi wa nchi hii walikuwa ni wakulima wa hali ya chini, na mataifa madogo mengi yalipitia njia ya maendeleo kutoka uhusiano wa kabla ya ubepari na hata wa zama za kale kwendea katika usoshalisti mnamo kipindi kifupi sana cha kihistoria. Lenin alisema kwamba kasumba za kujipendelea kitaifa na fikira fupi za kitaifa hazina budi

kutoweka pole pole sana, kwani hazitatoweka kabisa mpaka pale ubeberu utakapotoweka katika nchi zilizosonga mbele kiuchumi na mabadiliko makuu yatakapotukia katika msingi mzima wa mambo ya uchumi ya nchi zilizozorota.

Mwendo wa kuyatokomeza yale ya zamani, yaliyokwisha zake na yapingayo maendeleo, pamoja na masalio ya mawazo na hisia za kupakika kitaifa na kujipembua kitaifa na kushika mizizi kwa mawazo na maongozi ya umoja wa kimataifa wa kisoshalisti, saikolojia mpya na maadili mapya unatukia kwa mizozano na migongano.

Ubeberu wafanya juu chini kutaka kufufua fikira fupi za kujibagua kitaifa katika nchi za kisoshalisti, ukieneza mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa ili kuudhoofisha urafiki wa mataifa ya nchi hizo, wajitahidi kuyapambanisha maslahi ya mataifa mbalimbali, kuuchochelea upya uhasama wa zamani baina ya mataifa, ukiyatisha mataifa madogo kwa upotezaji wa uhuru wao, jadi yao, n. k. Majaribio ya kueneza na kuchochelea mtindo wa kujibagua kitaifa ni sehemu isiyotenganishika ya mwongozo wa kibeberu. Hayo yalionekana wazi wakati wa matukio ya 1968 nchini Chekoslovakia. Propaganda ya Uzayuni, majaribio ya kueneza mawazo ya kujipembua kitaifa na kuwa na tabia za kipekee za kitaifa miongoni mwa Wayahudi wanaoishi katika nchi za kisoshalisti ni mfano mwingine wazi. Itikadi ya Uzayuni inakwenda kinyume na maslahi ya wananchi wafanyao kazi, na maongozi ya umoja wa wafanyakazi wa kimataifa. Inatumikia maslahi ya ubeberu tu na vibaraka vyake, kwani

madhumuni makuu ya propaganda ya Uzayuni ni kughafilisha nadhari ya wananchi wafanyao kazi kutokana na misimamo ya kitabaka, kuyapambanisha maoni ya kitaifa na yale ya kitabaka, na kuyawakilisha maslahi ya kitabaka ya mabwanyenye wa Kiyahudi kama maslahi ya kitaifa ya Wayahudi wote. Dini ya Kiislamu inatumiwa kwa njia hiyo hiyo.

Lakini nafasi za kuweza kutokeza kwa mtindo huo wa kujibagua kitaifa katika nchi za kisoshalisti haiwezi kuelezewa kwa mabaki ya siku za nyuma tu pekee au kwa uharibifu wa kiitikadi wa kibeberu, ingawa hayo ni muhimu sana. Mtindo wa kujibagua kitaifa waweza kuchochelewa pia kama matokeo ya shida fulani za ujenzi wa usoshalisti katika nchi yenye mataifa mengi.

Kwenye kikao cha pamoja cha taadhima cha Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, Baraza Kuu (Bunge) la Muungano wa Jamhuri za Kisovieti na Baraza Kuu la JKKSU, kwa kuadhimisha miaka 60 tangu kuundwa kwa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti, ilitiliwa mkazo: "Mabadiliko halisi yaliyotukia mnamo miaka 60 iliyopita katika uhusiano baina ya mataifa, ni ushahidi wa hilo jambo kwamba suala la mataifa, kwa aina hiyo kama lilivyowasilishwa kwetu na mfumo wa kinyonyaji, limeshatanzuliwa kwa kufana, limeshatanzuliwa hatimaye na pasina kurudi nyuma. Kwa mara ya kwanza kabisa katika historia mpangiko wa mataifa mengi nchini umegeuka kutoka kuwa chanzo cha udhai-

fu kuja kuwa ndicho chanzo cha nguvu na ustawi".

Pamoja na hayo ilibainishwa: "Mafanikio katika utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa hayamaanishi hata kidogo kwamba matatizo yote ambayo yanatokana na huo ukweli wenyewe wa maisha na kazi mnamo mipaka ya dola moja lenye mataifa na makabila mengi yameshatanzuliwa kabisa. Jambo hilo yaelekea sana kuwa haliyumkiniki, madhali kunaendelea kuwako mataifa mbalimbali, madhali kungali bado kuna hitilafu za kitaifa. Nazo zitaendelea kuwako kwa muda mrefu, hata zaidi kuliko hitilafu za kitabaka".

Hisia ya utaifa inatenda kazi muhimu sana katika maisha ya sasa ya wananchi wa Kisovieti. Mwendo wa ukaribianaji wa mataifa ni wa mtataniko na wenye kuhitilafiana, na kuna ufungamano wa kidialekiiki, yaani umoja wa kidialektiki, baina ya fikira za uzalendo na umoja wa kimataifa. Uvunjwaji wa umoja huu waweza mara kwa mara kupelekea kuzuka kwa maoni ya kujibagua kitaifa, maoni ya kawaida ya hisia ya utaifa kugeuka kuja kwa mtindo wa kujibagua kitaifa. Mizani baina ya upande wa kitaifa na wa kimataifa, ambao ni tabia hasa ya ujongeleanaji wa mataifa, yaweza kugeuzwa kumili upande ule wa kitaifa, na hapo tena maslahi ya kienyeji kupambanishwa na yale ya dola zima. Kwa maana hii, mtindo wa kujibagua kitaifa unakuwa si siku zote ni ukanyo wa makusudi wa umoja wa kimataifa, bali waweza pia kuwa kama ni matokeo ya uelewaji wa makosa, usiopenya ndani vya kuto-

sha wa uwiano baina ya upande wa kitaifa na ule wa kimataifa.

Mafanikio makubwa sana yaliyopatikana katika maendeleo ya mataifa madogo yanaweza kuchochelea na kupepelea hisia za kujipembua kitaifa endapo hapataeleweka wazi kwamba mafanikio haya ni matokeo tu ya jitihada za pamoja zilizotolewa na mataifa yote. Ulegezaji wo wote ule katika utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa (kuahirika au kuitangulia mienendo iliyokwisha kuwa tayari kihalihalisi) pia wafungulia njia mitokezo ya mtindo wa kujibagua kitaifa.

Mgawanyo wa kazi wa kisoshalisti na ukuaji chapuchapu wa uchumi wahitaji mmiminiko wa daima wa wananchi kutoka jamhuri mbalimbali kwendea katika sehemu za ujenzi mpya. Mwendo huo ni wa kimaendeleo ambao unazidisha ukaribianaji wa mataifa na kusaidia kukuza tabia za kimataifa za pamoja. Wakati huo huo, mwelekeo wa kuingiliana zaidi kwa makundi ya kitaifa waweza kukumbana na majaribio kwa upande wa vyombo vya kienyeji kutaka kuwakweza katika vyeo vya juu makada wenye asili ya taifa la mahali huko kunakohusika, jambo ambalo huleta mtataniko katika uhusiano baina ya mataifa. Kwa kuzingatia mwelekeo huo uliotokezea kihistoria wa kuingiliana kwa makundi makubwa ya wananchi kutokana na mataifa mbalimbali kwenye maeneo ya jamhuri zote za Muungano, ufunzwaji na uelimishwaji wa makada wa kitaifa wa kienyeji yapasa uchanganyishwe kwa weledevu na mkabala wenye tabia ya umoja wa kimataifa kikweli kwa utumiwaji na uelimishwaji wa

makada wa mataifa mengine yote, pamoja na juhudi za kuipiga vita mitokezo yo yote ya mtindo wa kujipembua kitaifa.

Ujenzi wa ukomunisti wahitaji maendeleo ya kufana zaidi ya sekta mbalimbali pamoja na kikamilifu wa hali za kimaumbile na za kiuchumi, na maendeleo ya kiufundi yanakusudia mwelekeo mkubwa zaidi wa kushughulikia upande maalumu wa uzalishaji mali. Katika hali hizi ni muhimu hasa kuwaelimisha makada kwa ari ya kufahamu vilivyo majukumu yanayolikabili dola zima, ukomeshwaji kabisa wa mtindo wa kujibagua kienyeji, na ufuataji vilivyo wa kanuni za uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi.

Lenin alifahamisha kwamba chini ya utaratibu wa miliki ya kijamii ya uzalishaji mali, uchumi wa kisoshalisti hauwezi kuendelea kwa kufana pasina uongozi mmoja mkuu na upangaji mmoja wa pande nyingi. Uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi wazingatia vilivyo majukumu ya kijumla na yale ya kitaifa yaliyo mahsusi. Lakini, haya hayatukii wenyewe kwa wenyewe tu, bali yategemea juu ya shughuli za kimatendo za binadamu, juu ya utekelezaji kwa welekevu wa sera ya Chama, juu ya kazi ya kimatengenezo ya vyombo vya serikali kuu na za mitaani. Uachano wo wote kutokana na kanuni ya uongozi mmoja mkuu wa kidemokrasi, usiseme tena majaribio ya kuyapambanisha maslahi ya kienyeji na yale ya dola zima ni uachano kutokana na maongozi ya Lenin. Chama cha Kikomunisti na Serikali ya Kisovieti zinataka kuhakikisha paweko mizani barabara baina ya mamlaka ya kujitawala na uangalifu

kwa mahitaji ya kienyeji na maslahi ya dola zima, hasa sasa ambapo mapinduzi ya kisayansi na ya kiufundi yanahitaji mgawanyo wa kazi na ushirikiano wa busara zaidi.

Usoshalisti watoa fursa halisi za kuukomesha mtindo wa kujibagua kitaifa na kuimarisha urafiki baina ya mataifa, kitu ambacho ubepari hauwezi kukifanya kamwe. Lakini, katika utumiaji wa fursa hizi, jukumu muhimu kabisa linatwaliwa na sera ya Chama, na shughuli za kila siku za Chama, Masovieti na jumuiya za umma. Mpango na Katiba ya Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti zinamwajibisha kila Mkomunisti kuendesha mapambano yasiyochoka dhidi ya mitokezo yo yote ya mtindo wa kujibagua kitaifa na kiburi cha utaifa, kadhalika kusaidia kuimarisha urafiki baina ya mataifa ya Kisovieti.

Hakuna shaka yo yote kwamba uelezaji wa mapambano dhidi ya uachano wo wote kutokana na maongozi ya Lenin, uadilishaji ovyo wa umma na hasa watumishi wa Chama na Masovieti kwa ari ya umoja wa kimataifa, na mkabala wa kijuujuu tu kwa kampeni ya kueneza mawazo ya urafiki baina ya mataifa, yote hayo yangeweza kupelekea kurejea tena kwa fikira fupi za kujifungia kitaifa. Hiyo ndiyo maana kwa nini Chama kikawa kinaweka nadhari ya daima juu ya mambo yanayofungamana na uhusiano baina ya mataifa, na uadilishaji wa umma kwa ari ya umoja wa kimataifa.

Katika kuyakabili matatizo ya hima ya uhusiano baina ya mataifa, Chama kimekuwa kikipam-

bana na mitokezo yo yote ile ya mtindo wa kujibagua kitaifa na kiburi cha utaifa.

Kwenye Mkutano Mkuu wa 24 wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti katika 1971, wajumbe wengi waliukosoa msimamo uliochukuliwa na baadhi ya wasomi ambao wanapiga ubazazi juu ya heshima waliyo nayo watu kwa historia yao ya zamani na kuhubiri maoni yasiyo ya kitabaka, yasiyo ya uteuzi kuhusu siku za nyuma, na kwa hivyo kusababisha hali za kufufuka kwa fikira fupi za madhara, hasa miongoni mwa vijana. Wawakilishi wa Jamhuri za Kisovieti walisema kwamba mtu haimpasi kuzitukuza mno mila na desturi zilizokwisha zake, wala kuitafsiri historia kutokana na maoni ya kibwanyenye, ya uhange, kadhalika haimpasi kueneza fikira hiyo dhalili ya umoja wa kitaifa chini ya ubepari, kukanya au kuufifiliza msaada mkubwa sana uliotolewa na Warusi na mataifa mengine yote ya Kisovieti kuipa kila jamhuri, au kuipotoa historia ya uchipuaji na ukuaji wa urafiki baina ya mataifa. Mkutano huo uliziita taasisi kuu za uchunguzi, wanasayansi, wanasanaa, waandishi, wanamuziki na vyama vyao kushiriki kwa juhudi zaidi katika kueneza mawazo ya urafiki baina ya mataifa, kutoa taswira adhimu kabisa juu ya masuala ya uhusiano baina ya mataifa, na fasihi na sanaa waziwazi na za kukumbukwa zenye kuonyesha nguvu ya uhai ya sera ya Kisovieti ya uhusiano baina ya mataifa mnamo zama zetu.

Maazimio ya Mkutano Mkuu wa 25 (1976) na nyaraka nyingine za Chama cha Kikomunisti cha

Muungano wa Jamhuri za Kisovieti zimetoa madai makubwa zaidi kuhusu uadilishaji wa ari ya umoja wa kimataifa katika jamii ya kisoshalisti iliyoendelea. Shabaha kuu ya kazi hiyo ni kumsaidia kila raia wa Kisovieti kutambua vilivyo kwamba yeye ananasibiana na taifa la Wasovieti kama mjumuiko mpya wa kijamii na wa kimataifa, kuelewa jukumu la mwambatano mzima wa kiuchumi katika maendeleo ya kila jamhuri moja ya Muungano na nchi yote kwa jumla, ufanyaji wa maisha ya kijamii kuwa ya kimataifa na ujongeleanaji karibu zaidi wa mataifa, kukuza hisia ya kulionea fahari taifa zima la Wasovieti.

Katika kutanzua matatizo makubwa na madogo ya uadilishaji kwa ari ya umoja wa kimataifa, vyombo vya Chama na Serikali vinaweka nadhari mahsusi juu ya masuala kadhaa ya kimsingi: kufafanua barabara yale yaliyo ya kijumla na yale yaliyo mahsusi, ya kimataifa na ya kitaifa katika uhusiano baina ya mataifa, vikitilia mkazo maslahi ya kiserikali ya taifa zima la Wasovieti; mkabala wa kitabaka, wa ki-Chama kwa ukadiriwaji wa siku za nyuma za kila taifa, uenezaji wa kielekevu wa mafanikio ya kisoshalisti, uwasilishaji wa kuyakinisha wa manufaa yaliyoletwa na usoshalisti kwa mataifa na makabila yote, na umuhimu wa usaidiano wa kidugu baina ya mataifa kwa ujenzi wa ukomunisti; na uchanganyishaji wa kampeni, kazi ya maelezo na ile ya wendeshaji, usimamizi na ya kimatengenezo kwa ustawishaji wa mfululizo wa uchumi na utamaduni wa nchi nzima halikadhalika na wa kila taifa.

Chama kinaambatanisha majukumu ya uadilishaji kwa ari ya umoja wa kimataifa na jitihada ya shime zaidi katika kuwasaidia wananchi wa Kisovieti kuwa na kinga dhidi ya mabaki ya maoni ya kujibagua kitaifa, athari ya propaganda ya kibwanyenye ya kujibagua kitaifa na pia dhidi ya mfumo wa miliki ya kibinafsi. Mojawapo la majukumu makuu hapa ni kuwasaidia wananchi wa Kisovieti wawe na mkabala wa kitabaka kwa mitokezo ya utaifa na uhusiano baina ya mataifa na kujifunza kupambanua baina ya uzalendo halisi na ule wa uhange, na pia mtindo wa kujipendelea kitaifa.

Azimio la Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti za Kisoshalisti "Juu ya Ukamilishaji Zaidi wa Kazi ya Itikadi, ya Kisiasa na Uadilishaji" (1979) linatilia mkazo haja ya kukuza miongoni mwa wananchi wote wa Kisovieti hisia ya kuionea fahari nchi ya uzalendo ya kisoshalisti, urafiki wa kidugu usiovunjika kamwe baina ya mataifa ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, kuheshimu hadhi ya kitaifa na utamaduni wa kitaifa na kuwa na maoni yasiyopatanishika kamwe kwa mitokezo yo yote ya mtindo wa kujibagua kitaifa.

Mkutano Mkuu wa 26 wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti uliweka tena nadhari kuu juu ya masuala ya umoja wa kimataifa na uadilishaji wa wananchi wafanyao kazi kwa ari ya uzalendo wa Kisovieti na umoja wa kimataifa wa kisoshalisti. Maazimio ya mkutano mkuu huo yalitilia mkazo kwamba Chama kifuatacho maongozi ya Lenin kimekuwa

na kitakuwa daima kikipambana vikali na aina zote za kiburi cha utaifa au mtindo wa kujibagua kitaifa.

Haja ya kukamilisha zaidi uadilishaji kama huo kwa ari ya umoja wa kimataifa, ya kupambana na mitokezo fulani fulani inayokutikana bado ya mtindo wa kujibagua kitaifa haipunguzi kwa vyo vyote vile umuhimu wa yale yaliyokwisha patikana: umoja wa kimataifa umeshakuwa ndiyo tabia kuu ya Wasovieti kama mjumuiko mpya wa kijamii katika historia, tabia isiyokosekanika kabisa ya namna ya maisha ya kisoshalisti, ikijitokeza waziwazi katika ujenzi wa kikomunisti wa pamoja wa mataifa yote ya Kisovieti, katika kuunga mkono kwao siasa ya nje ya Serikali ya Kisovieti ambayo inashirikiana na nguvu zote zipiganiazo amani, ukombozi wa kitaifa, maendeleo ya kijamii na usoshalisti, dhidi ya siasa ya ubeberu ya kupinga maendeleo.

TAMATI

Mikabala na mikazo katika baadhi ya matatizo yanayotokana na suala la mataifa iliamuliwa kwa ukali wa uhusiano baina ya mataifa katika mamlaka ya zamani ya mfalme wa Kirusi, lakini ilidhihirisha vile vile kwa uwazi zaidi maongozi ya kimsingi ambayo bila yake suala la mataifa haliwezi kutanzuliwa. Umuhimu wenye kuambata pande zote wa njia kwa ajili ya utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa na matokeo yake, hauwezi kuteremshwa chini kwa sababu ya makosa yaliyofanywa na wale ambao iliwabidi waangazie njia katika upande huu au hata kwa upotoshaji wa sera ya uhusiano wa mataifa ambao ulitokana na mtindo wa kuabudu ubinafsi wa kiongozi.

Kati ya kanuni zinazotumika kote kabla ya yote ni haja ya kuzingatia tabia halisi za kipekee za kila taifa kubwa na dogo, shida zilizoko njiani mwa wananchi wafanyao kazi wa kila taifa katika kuelewa umoja wa maslahi yaliyopo kati ya ma-

taifa, haja ya kufanya mageuzi makuu ya kijamii, mkabala wa hadhari na wa uvumilivu kwa masalio ya kitaifa na jitihada za kutafuta mbinu na njia barabara za kuyashinda.

Pamoja na hayo utanzuaji wa tatizo la uhusiano baina ya mataifa ambao unatokana na ushindi wa uhusiano wa kisoshalisti wa uzalishaji mali wahitaji kwamba sera ya uhusiano baina ya mataifa iwekwe chini ya maslahi ya mapambano ya kitabaka. Huku pakihitajika uvumilivu kwa mabaki ya tabia ya kutoaminiana kati ya mataifa, Lenin alitilia mkazo kwamba hairuhusiki kutoa ridhaa zenye kuathiri maslahi makuu ya wafanyakazi. Wanaitikadi wa kibwanyenye wanadai kwamba sharti hili la Lenin ati lilipelekea kupuuza na kuyashushia umuhimu maslahi ya kitaifa, lakini ukweli wa mambo wakanusha kabisa madai haya. Mbali na kukinza maendeleo ya mataifa, mkabala huo wa Lenin, kwa hakika hasa, uliyachapua na kuharakisha utanzuaji wa tatizo la uhusiano baina ya mataifa juu ya msingi wa kweli pekee, nao ni ukomeshaji wa mfumo wa kinyonyaji na kuendesha mapambano yasiyosita dhidi ya mitokezo ya kiburi cha taifa kuu na mtindo wa kibwanyenye wa kujibagua kitaifa. Ili mataifa na makabila yote yaweze kuendelea kwa uhuru na usawa ni lazima paweko hali za kufalia za kijamii-kiuchumi na za kisiasa zilizo huru kutokana na uhusiano wa kinyonyaji. Leo kumeshadhihirika wazi kabisa ufungamano ulioko baina ya utanzuaji wa tatizo la uhusiano kati ya mataifa katika nchi zilizojipatia uhuru wao karibuni na chaguo lao la njia ya maendeleo ya kija-

mii-kisiasa. Lenin alisema kwamba kipimio chenye kuamua kama harakati hizi au zile za ukombozi wa kitaifa ni za kimaendeleo au zenye kupinga maendeleo, katika kila kadhia moja mahsusi ni suala hilo la kama zinasaidia kuimarisha nguvu za kimapinduzi zipingazo ubeberu au zinapelekea katika mfarakano wao, zinatosheleza maslahi ya umma wa wananchi wafanyao kazi au zinalingana na matakwa ya kikundi cha juu cha wanyonyaji, zinatumikia malengo ya ukombozi wa kijamii wa wananchi wafanyao kazi, maslahi ya usongaji mbele wa jamii, au zinatumiwa na ubeberu na wapinga maendeleo wa ndani kwa ajili ya kuzidhoofisha, kwa maslahi ya matabaka ya kinyonyaji. Mitindo ya kuleta mfarakano katika dola la mataifa mengi, ile ya kujitenga mbali na maslahi ya dola zima na mambo ya siasa ya nje, haidhuru vipi azma zake zilivyo, yaweza kuyaletea hasara isiyofidika maslahi ya mataifa yote ya nchini, mkiwemo taifa lile ambalo mitindo hii inazuka miongoni mwake. Mitindo hiyo yaufalia ubeberu tu.

Yatosha kutaja tu hali ya mambo ilivyo huko Ethiopia ambayo ilisababishwa na msimamo wa Waeritrea wanaopendelea kujibagua kitaifa, na hali ya mambo katika majimbo ya India yenye kupakana na China na huko Afghanistan. Katika kila moja ya nchi hizi wapinga mapinduzi wakishirikiana na mabeberu wanajaribu kuyachukulia fursa mapambano yaendeshwayo na mataifa madogo ili kufalia maslahi yao, dhidi ya serikali ya kidemokrasi na utawala wa kimapinduzi.

Sera ya kikoloni ya ubeberu ilipelekea katika

hilo jambo kwamba mataifa na makabila mengi yalijikuta yametenganishwa na kuishi kwenye maeneo ya nchi mbalimbali. Lakini uunganishwaji wao tena hauwezi kupatikana kwa njia ya vita baina ya nchi hizi, kwani hayo yangefalia maslahi ya ubeberu tu. Uunganishwaji wao tena waweza kupatikana kwa kufanya mazungumzo, kwa kueneza demokrasi katika nchi zilizojipatia uhuru wao karibuni, kwa badiliko zaidi la mizani ya nguvu ulimwenguni, kwa udhoofikaji wa nguvu za ubeberu, kwa uwekwaji wa aina ile mpya ya uhusiano baina ya mataifa, ambayo inapiganiwa na nchi za kisoshalisti.

Uzoefu wa nchi hii ya Kisovieti umeonyesha kwamba tabaka la wafanyakazi lishikilialo msimamo thabiti wa umoja wa kimataifa ndiyo nguvu kuu na yenye kuleta muungano imara katika mapambano ya kuwania usawa baina ya mataifa na kuyashinda masalio ya siku za nyuma. Hiyo ndiyo maana kwa nini ukuzwaji wa tabaka la wafanyakazi na uadilishwaji wake kama ndiyo nguvu iongozayo katika mageuzi ya kijamii unakuwa ndilo sharti kuu kwa utanzuaji wa tatizo la uhusiano baina ya mataifa. Msimamo wa umoja wa kimataifa wa tabaka la wafanyakazi la taifa kandamizi kwa mataifa manyonge ni wenye umuhimu mahsusi. Mfano wa tabaka la wafanyakazi la Kirusi, ambao ulitoa msaada mkubwa sana kuyapa mataifa yaliyozorota yakaayo Urusi, ulifuatwa, kwa mwito wa Vyama vya Kikomunisti, na tabaka la wafanyakazi la Ufaransa na Ureno, ambalo lilifanya mengi kuyasaidia makoloni ya zamani ya Ufaransa na Ureno kuinuka

kupigania uhuru wao. Tabaka la wafanyakazi laweza kutekeleza ujumbe wake unaohusiana na umoja wa kimataifa chini ya uongozi wa chama cha kimapinduzi tu ambacho shughuli zake zimetegemezwa juu ya maongozi ya usoshalisti wa kisayansi.

Uzoefu wa dola la Kisovieti na nchi nyingine waonyesha kwamba papo tu chama cha kimapinduzi kikishakuja kuwa ndicho Chama kinachotawala, kinaanza moja kwa moja kuyathibitisha kisheria madai ya mpango wake wa uhusiano baina ya mataifa na kusababisha hali zinazohitajika kwa utekelezwaji wao kimatendo.

"Maongozi Makuu ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Afghanistan", waraka uliotolewa na Baraza la Mapinduzi la Afghanistan mnamo katikati ya mwaka 1980, na ambao ni Katiba ya muda ya nchi hiyo, wadhaminia usawa halisi kwa mataifa na makabila yote ya nchini, makubwa kwa madogo. Yanadhaminiwa fursa sawa kwa kuendeleza lugha, mila, fasihi na utamaduni wao wa aina ya kipekee. Waraka huo unakataza kabisa ubaguzi wa kitaifa, wa lugha, wa rangi au wa kikabila katika kuajiri kazini katika idara za serikali, katika ukadiriaji ukubwa wa pensheni, n.k. Waraka huu umekusudiwa kuunganisha umma mkubwa wa wananchi wafanyao kazi katika kupambana na ubeberu na wapinga maendeleo wa ndani.

Lakini, pamoja na sheria zenye kuthibitisha usawa wa kisiasa wa mataifa yote, panazuka suala kuu la kuyapatia mataifa usawa halisi wa kimatendo. Hili ni jukumu muhimu sana, na kuko-

sa kuliwekea nadhari ya kutosha huenda kukasababisha ugomvi wa kisiasa baina ya mataifa.

Utanzuaji wa tatizo la uhusiano wa mataifa katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti sasa wapata umuhimu mahsusi kwa kuzingatia hilo jambo kwamba suala hili laendelea kuwa ni mojawapo la matatizo yanayohitaji kushughulikiwa kwa hima sana katika matukio ya mambo ulimwenguni. Wanaitikadi wa kibwanyenye wafuatao mielekeo mbalimbali ya kijamii na kisiasa wanakabiliwa na suala hili: vipi kuujibiza "mwito wa kudai uliotolewa na usoshalisti" wakati huo hasa ambapo ugomvi baina ya mataifa katika nchi za kibepari zilizoendelea umekuwa mkali sana, na ambapo wingi mkubwa wa mataifa ya Asia na Afrika umeshajikomboa kutokana na utegemezi wa kikoloni na kupitia kipindi cha uumbikaji wa taifa?

Katika hali hizi, ili kupunguza taathira ya mfano wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti katika kutanzua tatizo la uhusiano wa mataifa, watungaji nadharia na wanasiasa wa kibwanyenye wamekuwa wakifanya juu chini kuupaka matope uzoefu wa nchi ya Kisovieti ili kuyavunga mataifa ya dunia kwamba usoshalisti ati haujaleta kitu kipya cho chote katika uhusiano baina ya mataifa na kwamba suala la mataifa katika Muungano wa Jamhuri za Kisovieti halijasuluhishwa bado (wanaipotoa maana ya sera ya Chama cha Kikomunisti cha nchi hii juu ya uhusiano wa mataifa, pia historia ya utanzuaji wa tatizo hilo, na kudai kwamba ati jitihada za Chama cha Kikomunisti zá kuleta ujongeleano wa mataifa

zinapelekea katika kumezwa kabisa kwa mataifa manyonge ya zamani, n. k.).

Umoja wa kidugu wa mataifa ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti umeupunguza sana upande ule ambao ubeberu ungeweza kuzitumia tofauti zilizoko baina ya mataifa, na hili limekuwa ndilo jambo muhimu lenye kuipa nguvu taathira ya nchi hii ya Kisovieti kwenye uwanja wa kimataifa.

Uvukaji wa usoshalisti kupindukia mipaka ya nchi moja na uundwaji wa jumuiya ya madola ya kisoshalisti yenye mfumo wa kijamii wa aina ile ile moja na malengo ya hatimaye ya pamoja uliashiria daraja mpya katika maendeleo ya utanzuaji wa suala la mataifa. Muungano wa Jamhuri za Kisovieti ulitoa mfano wa mamlaka ya kiserikali ya kitaifa ndani ya dola moja lenye mataifa mengi. Uundwaji wa jumuiya ya madola ya kisoshalisti uliashiria mwanzo wa utanzuaji wa matatizo katika uhusiano baina ya mataifa mnamo mipaka ya mfumo unaoambata madola mengi.

Uundwaji na ukuzwaji wa jumuiya ya madola ya kisoshalisti umeashiria siyo tu upanuaji wa upande wa kuingiza taathira ya umoja wa wafanyakazi wa kimataifa, bali pia ufikiliwaji wa daraja mpya katika maendeleo ya aina mpya ya uhusiano baina ya mataifa, nayo ni umoja wa kimataifa wa kisoshalisti. Nchi zilizomo ndani ya jumuiya ya madola ya kisoshalisti zimekuwa zikiimarisha ushirikiano wao wa kisiasa, ambao umetegemezwa juu ya usawa wa nchi zote, kubwa na ndogo, juu ya mamlaka yao ya kujitawala,

ushikamano wa kidugu na ulinzi wa pamoja wa mafanikio ya usoshalisti dhidi ya minyemeleo ya mabeberu. Zimekuwa zikikuza ushirikiano wa kiuchumi wa pande zote ambao sasa unamithilishwa tabia yake kwa mwelekeo wa uchanganyishaji uchumi wa kisoshalisti uliokusudiwa kusawazisha viwango vya maendeleo yao ya kiuchumi na kuyatumia mafanikio ya mapinduzi ya kisayansi na ya kiufundi na fursa za usoshalisti ndani ya mipaka ya mfumo mmoja wa madola. Ushikamano wa nchi za kisoshalisti ambao umetegemezwa juu ya jitihada zao za pamoja za kuimarisha nguvu ya jumuiya ya madola ya kisoshalisti, unaziwezesha kuwa na athari kuu juu ya matukio ya mambo ulimwenguni, juu ya badiliko la mizani ya nguvu duniani kwa kufalia demokrasi, ukombozi wa kitaifa na usoshalisti.

Ni ushikamano huu ndio wanaitikadi wa kibeberu walioushambulia vikali zaidi kwa sababu umeifanya siasa ya nje ya mabeberu kushindwa vibaya sana. Wakitegemea msaada wa juhudi na wa kufaa sana wa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti na nchi nyingine za kisoshalisti wananchi mashujaa wa Vietnam walipata ushindi mkuu kwa kuwafurusha waingilizi wa Kimarekani na kuiunganisha nchi yao. Ikitegemea ushirikiano wa kidugu wa nchi za kisoshalisti, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Ujerumani imefaulu kutetea na kuimarisha mastakimu yake ya kisiasa ya nje na kuivunja uso mipango ya mabeberu ya kukamia kulipiza kisasi. Ushikamano wa kimataifa wadhaminia uhuru na kujitegemea na pia usongaji mbele wa kijamii kwa Jamhuri ya Cuba.

Wanaitikadi wa kibwanyenye wajaribu kuyashurutishia mataifa hoja hiyo kwamba uhasama baina ya mataifa na sera za ubakuzi kuwa ni za kimaumbile kwa usoshalisti (wakiutafsiri kwa njia hiyo hiyo msaada usiojitakia faida utolewao na Muungano wa Jamhuri za Kisovieti kutokana na msimamo wake wa kuunga mkono umoja wa kimataifa). Wanadai kwamba ati nchi za kisoshalisti zingali zimegawanyika kwa uhasama usiopatanishika kamwe, ambao huenda pengine ukapelekea hata kuzuka vita.

Mafunzo ya Marx na Lenin hayapatani asilani na maoni ya wale wanaoacha maongozi makuu ya kijumla ya mapinduzi ya kisoshalisti. Hilo jambo kwamba kila nchi inabidi ipitie njia yake yenyewe ya kipekee halimaanishi kwamba hakuna tabia kuu za pamoja na kawaida za kimaumbile za aina moja za mapinduzi ya kisoshalisti na ujenzi wa usoshalisti. Kuhusiana na haya, Lenin aliandika katika makala *Ukomunisti wa "Mrengo wa Kushoto" – Ugonjwa wa Kitoto:* "Madhali kunaendelea kuwako mipambanuo ya kitaifa na kidola miongoni mwa mataifa na nchi mbalimbali – nayo itaendelea kuwako kwa muda mrefu sana ujao, hata baada ya kwisha kuwekwa kwa utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi kwa upeo wa dunia nzima – umoja wa mbinu za kimataifa za harakati za kikomunisti za tabaka la wafanyakazi wahitaji siyo uondoshaji wa aina mbalimbali au udidimizaji wa mipambanuo ya kitaifa (ambao kwa sasa ni utoaji ndoto mtupu), bali utumiaji wa maongozi *ya kimsingi* ya ukomunisti ... ambao *ungerekebisha barabara* maongozi

hayo katika mambo fulani fulani *mahsusi*, ungezielekeza barabara na kuzitumia kufalia mipambanuo ya kitaifa na kitaifa-kidola. Kutafiti, kuchunguza, kutafuta, kuagulia na kukikamata kile ambacho ni cha kipekee kitaifa na cha mpembo kitaifa katika *mkabala halisi* ambayo kila nchi inautumilia ili kutanzua jukumu *moja kuu* la kimataifa: ushindi dhidi ya ugeugeu na ung'ang'aniaji kanuni kipofu kwa upande wa wafuasi wa siasa za mrengo wa Kushoto ndani ya harakati za tabaka la wafanyakazi; upinduliwaji wa mabwanyenye; uwekwaji wa utawala wa kipekee wa tabaka la wafanyakazi...–hivyo ndivyo lilivyo jukumu hilo kuu".

Ujenzi wa usoshalisti na uimarishaji wa mastakimu yake ya ndani na ya nje hautenganishiki na mapambano thabiti dhidi ya kila aina ya uyumbaji wa kiitikadi, mtindo wa kujibagua kitaifa, ubadilishaji fikira, jitihada za kuyapambanisha baadhi ya mataifa na baadhi ya vyama vya Kikomunisti na vingine, pia dhidi ya mawazo ya huo uitwao kama "ukomunisti wa kitaifa".

Siasa ya nje ya Muungano wa Jamhuri za Kisovieti na nchi zote nyingine za jumuiya ya madola ya kisoshalisti imetegemezwa juu ya mwongozo wa umoja wa wafanyakazi wa kimataifa.

Nchi zilizo wanachama wa jumuiya ya madola ya kisoshalisti zimekuwa daima zikiendesha siasa iliyotegemezwa juu ya maongozi ya Lenin kuhusiana na mataifa yaliyojichopoa kutokana na mabaki ya utegemezi wa kikoloni kamili au kwa sehemu. Hapa, ushikamano wao wa pande zote na wa kufaa sana na madola machanga ya kitaifa

yanayopigania uhuru wao wa kweli wa kitaifa ni wenye umuhimu mkuu. Nchi za kisoshalisti zimekuwa zikiyachukulia kama ni sawa nazo kabisa, zimeonyesha kuheshimu tabia zao za kipekee na maslahi yao mahsusi na kujizuia kuingilia katika mambo yao ya ndani. Hii yamaanisha ushirikiano kwa maslahi ya kitaifa ya madola haya, kwa manufaa ya mapambano ya pamoja ya kupinga ubeberu. Akijibu swali lililotolewa na mwandishi wa habari wa Kifaransa, hayati Indira Gandhi alitangaza mnamo mwanzoni mwa 1980 kwamba kunapohusika na suala la uhuru au makoloni, Muungano wa Jamhuri za Kisovieti unaziunga mkono nchi zisizofungamana na kambi yo yote ya kivita na zile zilizojipatia uhuru wao karibuni. Nchi za jumuiya ya madola ya kisoshalisti zimekuwa daima zikiunga mkono msimamo wa nchi zilizojipatia uhuru wao karibuni kutaka kuanzisha utaratibu mpya wa kimataifa katika uhusiano wa mambo ya uchumi wenye kufyeka kabisa mirija ya unyang'anyaji ya ubeberu.

Ushirikiano kati ya nchi zinazoendelea na jumuiya ya madola ya kisoshalisti wasaidia kuujalizia na kuutajirisha mwelekeo wa kujitambua kitaifa wa nguvu za kimapinduzi katika nchi hizi kwa maudhui ya umoja wa kimataifa na kuipa siasa ya nchi hizi tabia ya umoja wa kimataifa.

Lakini, ubeberu watumai kuutumia mwelekeo wa kujitambua kitaifa wa nguvu za kimapinduzi katika nchi hizi kwa maslahi yake wenyewe na kujaribu kuutegemea kwa madhumuni ya kuzigonganisha nchi zinazoendelea na madola ya kisoshalisti, na kuzitenganisha.

Wafuasi wa mafunzo ya Marx na Lenin wanatambua kwamba miaka mingi ya mkandamizo wa kikoloni na upondaji wa hadhi yao ya kitaifa na haki za binadamu za kimsingi katika nchi zilizozorota ulipelekea kufufuka kwa fahamu ya kujitambua kitaifa ambayo kama kawaida huwa na tabia ya kujibagua kitaifa. Umuhimu wa kimaendeleo wa mwelekeo huu wa kujitambua kitaifa upo katika hilo jambo kwamba kwenye daraja ya sasa unakuwa umelengewa kwanza kabisa dhidi ya ubeberu na ukoloni.

Lakini wakoloni mamboleo wamekuwa wakijaribu kuitumia mitindo ya kujibagua kitaifa katika nchi zilizokuwa hapo zamani chini ya utawala wa kikoloni na utegemezi wa aina hii au ile kwa matilaba yao wenyewe. Mabeberu wamekuwa wakijaribu kupepelea tuhuma na uhasama miongoni mwa wazalendo wa kimapinduzi kwa wale wanaotetea mwongozo wa umoja wa kimataifa ili kuyabubutua makali ya mwelekeo wa kupinga ubeberu na maudhui ya kidemokrasi ya kijumla ya mtindo wa kujitambua kitaifa na kuutia makali ya kupinga ukomunisti.

Uzoefu waonyesha pia kwamba katika nchi hizo zenyewe zinazoendelea wapinga maendeleo wanafanya juu chini kuutumia mtindo huu ili kuuhujumu mfumo huo mpya.

Gus Hall, Katibu Mkuu wa Chama cha Kikomunisti cha Marekani, alisema kwamba "Huku pakitambuliwa pande za kufalia za mtindo wa kibwanyenye uchwara wa kujitambua kitaifa katika vipindi fulani vya mapambano dhidi ya ubeberu na kuwania ukombozi wa kitaifa, yapasa pia

kuchungua kama kumefanywa jitihada zinazohitajika za kuupiga vita upande wake wa madhara na pia utumiwaji wake na nguvu zipingazo maendeleo, na kama kipindi cha kihistoria cha taathira zake za kufalia kwa ukomo wake hakijapita".

Uchambuzi huu yapasa ufanywe – na unafanywa kwa hakika hasa – na vyama vya kimapinduzi vya kidemokrasi vya nchi zilizojikomboa kutokana na utegemezi wa kikoloni, na vinategemeza siasa yao juu ya uzoefu wa Chama cha Kikomunisti cha Muungano wa Jamhuri za Kisovieti, ambacho kinaangalia kwamba katika nchi hii ya Kisovieti, huku kukichukuliwa hadhari ya kuenzi mapokezi ya utamaduni na mila, wakati ule ule pasije pakahifadhiwa yale yaliyo mabaya, yaliyokonga na yaliyokwisha zake ambayo yanakwenda kinyume na shabaha za maendeleo ya kusonga mbele na malengo ya usoshalisti. Vinategemeza hoja zao vile vile juu ya hilo jambo kwamba uimarishaji wa urafiki na ushirikiano baina ya mataifa wategemea juu ya uendelezwaji wa demokrasi, juu ya kushiriki kwa wingi zaidi kwa wananchi wafanyao kazi wa mataifa yote katika wendeshaji wa mambo ya kijamii na ya kiserikali.

Katika shughuli zao za kimatendo nchi zilizojipatia uhuru wao karibuni zinakumbana na mikabala miwili yenye kutofautiana kwa matatizo ya uhuru wa nchi zao kwa upande wa usoshalisti ulioko kimatendo hasa na ubeberu.

Mizani ya nguvu iliyotokezea ulimwenguni kumili upande wa usoshalisti yapelekea kuweko hali njema sana za kufalia maendeleo ya kiuchumi na

ya kisiasa ya nchi zilizojipatia uhuru wao karibuni. Pamoja na jambo hilo, msaada ziupatao kutoka nchi za kisoshalisti ni wenye umuhimu mkuu, na ukubwa wake ni wa maana sana lakini uliopakika kwa wingi wake kwa sababu ya majukumu magumu yaliyozikabili nchi za kisoshalisti kutokana na haja kuu ya kudhaminia ulinzi wao dhidi ya hatua za kichokozi za mabeberu na katika kudhaminia mabadiliko zaidi katika mizani ya nguvu ulimwenguni kwa manufaa ya usoshalisti. Kuwako kwenyewe kwa nchi za kisoshalisti, misaada na sera yao ni yenye umuhimu mkuu kwa sababu katika hali hiyo ya mambo iliyotokezea sasa ulimwenguni, ubeberu umeshakuwa hauwezi tena – kama ulivyokuwa ukifanya zamani – kuzilazimisha masharti yake, mkiwemo yale ya kisiasa, nchi zinazoendelea. Jambo hili limeziwezesha hizo za pili kufuata sera zao za kujitegemea zenyewe zilizokusudiwa kukuza maendeleo yao ya pande zote, pasina kuacha ushirikiano wa kiuchumi, kiufundi na mwingineo na nchi za kibepari na pasina kuvunja uhusiano kama huo pamoja nazo, mkiwemo uhusiano wao na nchi zilizokuwa zikitawaliwa nazo hapo zamani. Utumiaji barabara wa fursa hizi pasina kutoa ridhaa zo zote za kimsingi za kisiasa wategemea juu ya upevukaji wa kisiasa wa vyama vinavyotawala na viongozi wao, na uwezo wao wa kuona ujanja na upurukushani wote wa sera ya ukoloni mamboleo ya ubeberu na kuzitegemea nchi za usoshalisti ulioko kimatendo hasa.

Hamu ya kukomesha upesi kama iyumkinikavyo hali ya kuzorota iliyorithiwa kutokana na

sera ya kikoloni ya ubeberu ni ya kawaida kabisa, na njia za kutanzua tatizo hilo yapasa pia ziwe za kawaida, na jambo hili kwa upande wake lahitaji kuonyesha upevukaji wa kisiasa na ujuzi mwingi wa kiuchumi kwa upande wa nguvu zinazouongoza mwendo huu, lahitaji kukataa kufanya majaribio ya kuuchapua mwendo wa maendeleo ya nchi inayohusika kwa njia isiyo ya kimaumbile, kurukiza daraja zinazohitajika kwa maendeleo yake.

Ni muhali kukomesha uzorotaji wa nchi fulani kwa kuingiza mashine za kisasa, wataalamu wa kigeni na maduhuli makubwa sana ya fedha, lakini bila ya kufanya mageuzi ya kijamii ya kupenya ndani sana na bila ya kuinua kiwango cha hali ya maisha ya wananchi na cha elimu ya umma. Kitu muhimu katika kutafuta njia za maendeleo ya kitaifa ya kufana ni uwezo wa kustahamili mshinikizo wa ubeberu, kutorudi nyuma kutokana na njia iliyokwisha chaguliwa ya kufuata mwelekeo wa kisoshalisti.

Mabeberu wanazisengenya nchi za kisoshalisti, wakidai kuwa ni marafiki wa mataifa yaliyojikomboa karibuni na watetezi wa Waislamu, na wamekuwa wakiufanyia ubazazi huo mwito wa kudai haki za binadamu. Lakini kati ya haki muhimu zaidi ni ile ya usawa wa mataifa, haki ya kuhifadhi hali zenyewe za kuwako kwao, haki ya kuwa na demokrasi na maendeleo ya kijamii, na hicho ni kitu ambacho ubeberu umekuwa ukikipiga vita kwa kila njia iyumkinikayo, mkiwemo uchokozi wa kivita na vikwazo vya kiuchumi.

Makelele mengi zaidi kuhusu demokrasi, haki

za binadamu, uhuru wa kitaifa na "ulimwengu huru" yamekuwa yakisikika kutoka miongoni mwa makundi ya kibeberu yenye kutawala huko Marekani. Yametumia makelele hayo kufichia vita vyao vya kichokozi dhidi ya wananchi wa Vietnam; kufichia mpinduo wa kiserikali uliofanywa na mafashisti walioiangusha serikali ya halali na iliyochaguliwa kwa njia ya kidemokrasi huko Chile; uchokozi wa kijeshi dhidi ya wananchi wa Afghanistan; kufichia msaada wa pande zote kwa wachokozi wa Kiisraeli dhidi ya nchi za Kiarabu; kufichia uwekwaji wa vituo vya kijeshi vya kila aina vipatavyo 2,500 katika nchi 110; kufichia msaada wa moja kwa moja kuupa utawala wa mabavu wa kijeshi huko Salvador; kufichia majaribio ya kuurejesha tena utawala wa kikundi cha Pol Pot nchini Kampuchea. Kuna mamia ya mifano kama hiyo, na mataifa yaliyohadaiwa au kupotoshwa yapasa yajue hayo ili kutambua kitisho kinachoikabili jamii nzima ya binadamu kutokana nayo. Utawala wa Marekani unachochelea umma kuwa na hisia za kujibagua kitaifa na kiburi cha kitaifa, na ari ya uzalendo wa uhange ili upate kuzitumia dhidi ya mataifa ya Kisovieti na ya nchi nyingine za kisoshalisti za Mashariki ya Kati, Amerika ya Kati na mengineyo. Waenezaji propaganda wa kibeberu haweshi kupiga makelele kuhusu haki za binadamu, huku wakizipuuza haki za mataifa mazima mazima, haki yao ya kujikomboa kutokana na ukandamizi wa kibeberu na tawala za mabavu za kipolisi huko makwao, kuishi kwa uhuru, kukomesha uzorotaji wao na umasikini wao na kupata

fursa ya kufaidia mafanikio yote ya kisasa yaliyopatikana na jamii ya binadamu. Wanapiga makelele kuhusu haki za binadamu, huku wakati huo huo wakitia moyo madhila wanayokutishwa watu wasio weupe katika nchi zao wenyewe, pia wote wale wanaoendesha mapambano dhidi ya unyonyaji, wanaowania demokrasi, haki ya kupata kazi na mahali pa kuishi, kukimiwa uzeeni na kuwa na kauli katika wendeshaji wa mambo ya kijamii.

Nguvu inayokinza njama za ubeberu ni jumuiya ya madola ya kisoshalisti, pamoja na siasa yake thabiti ya kupigania amani, usawa wa mataifa, na kupambana vikali na ukoloni wa kiasilia na ukoloni mamboleo, na kila aina ya mkandamizo wa kijamii na kitaifa. Siasa yao inaungwa mkono na wapenda maendeleo wa nchi zote.

Ucharukwaji wa makundi ya kishari zaidi ya ubeberu, ambao umeifanya hali ya kimataifa kuwa mbaya sana, wahitaji kutoa jitihada nyingi zaidi katika kuimarisha umoja wa nguvu zote zipingazo ubeberu na kwanza kabisa wa jeshi la mbele la kimapinduzi la tabaka la wafanyakazi na watu wote wengine watumiao jasho lao, wahitaji kuzidisha uungaji mkono wa kimataifa kwa wote wale wanaopambana na ubeberu.

Imechapwa katika Soviet Union

KWA MSOMAJI

Progress Publishers watafurahi kupata maoni yako juu ya kitabu hiki, tafsiri yake, nakshi na upigaji chapa wake, na kupokea mashauri yo yote kutoka kwako.

Tafadhali andika kwa anwani: Zubovsky Boulevard, 17, Moscow, USSR.

ИБ №13730

Редактор русского текста *В. Е. Репин*
Контрольные редакторы *С. Ш. Аитова, В. П. Зеленина*
Художественный редактор *Г. Н. Губанов*
Технические редакторы *Д. Я. Белиловская, Л. Ф. Шкилевич*
Корректор *Т. Ю. Болдова*

Сдано в набор 18.09.84. Подписано в печать 15.03.85. Формат 70 × 90 1/32. Бумага офсетная. Гарнитура баскервиль. Печать офсетная. Условн. печ. л. 8,19 Усл. кр. отт. 36,6. Уч.-изд. л. 8,08. Тираж 1870 экз. Заказ № 907. Цена 57 к. Изд. № 38897

Ордена Трудового Красного Знамени издательство «Прогресс» Государственного комитета СССР по делам издательств, полиграфии и книжной торговли.
119847, ГСП, Москва, Г-21, Зубовский бульвар, 17.

Можайский полиграфкомбинат. Союзполиграфпрома при Государственном комитете СССР по делам издательств, полиграфии и книжной торговли.
143200, Можайск, ул. Мира, 93.

Mfululizo wa "Vitabu vya Maarifa ya Kisiasa" ambao umeanza kutengenezwa kwa ajili ya wasomaji wetu, ni sehemu ya mwanzo ya mkusanyiko maalum wa maandishi yaelezeayo masuala ya maendeleo ya kijamii katika zama zetu. Vitabu vilivyomo ndani ya mfululizo huo vinatoa maelezo rahisi ya masuala yahusikayo na mwundiko wa jamii, mwenendo wa kubadilika kwa mifumo ya kijamii ya aina tofauti, halikadhalika tabia muhimu za mapinduzi ya kisayansi na ya kiufundi katika ulimwengu wa leo.

Ifuatayo ni orodha ya "Vitabu vya Maarifa ya Kisiasa":

Plimak Y., Volodin A. *Jinsi Jamii Inavyoendelea.*

Lopata P. *Ukomunisti Kama Mfumo wa Kijamii na Kiuchumi.*

Batalov E. *Nadharia ya Mafunzo ya Lenin Kuhusu Mapinduzi.*

Trepelkov V. *Mchafuko wa Kijumla wa Ubepari.*

Neznanov V. *Kuhusu Njia za Ukiukaji Kutoka Ubepari Kuingia Katika Usoshalisti.*

Pirogov G. *Utaratibu wa Kisoshalisti Ulimwenguni.*

Zotov V. *Nadharia ya Lenin Kuhusu Mapinduzi ya Kuania Ukombozi wa Kitaifa na Zama za Sasa.*

Sobakin V. *Mafunzo ya Marx na Lenin Kuhusu Masuala ya Vita na Amani.*

Kikundi cha Waandishi. *Ubepari, Usoshalisti na Mapinduzi ya Kisayansi na ya Kiufundi.*

Varlamov K. *Uongozi wa Kisayansi wa Jamii ya Kisoshalisti.*

Smirnov G. *Shakhsia Chini ya Usoshalisti.*

Kashlev Yu. *Mapambano ya Kiitikadi Katika Ulimwengu wa Leo.*

Pavlenko A. *Harakati za Kimapinduzi Ulimwenguni.*

Gililov S. *Mkabala wa Lenin Kuhusu Suala la Mataifa.*